

MATUMIZI YA MBINU ZA UFUPISHAJI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII NA

ATHARI ZAKE KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

TASNIFU

YA

JELIMO DORIS

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI CHUO
KIKUU CHA KENYATTA**

APRILI, 2016

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

IKIRARI


Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijatolewa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

JINA

SAHIHI

TAREHE

JELIMO DORIS



21/04/2016

C50/23541/2013

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo.

JINA

SAHIHI

TAREHE

DKT. JACKTONE O.ONYANGO



21.4.2016


IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI

TAREHE

MWL. EVERLYN S. MUDHUNE



21/4/16

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu William Koech na Rael Koech pamoja na ndugu yangu Enock Kemboi na rafiki yangu wa dhati Joshua kwa kunionyesha upendo na kunitia moyo na kuhakikisha nisikose chochote wakati wa utafiti huu. Mungu awabariki sana. Asante sana.

SHUKRANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mungu kwa kunipa uwezo na kunijalia nikamilishe kazi hii. Ningependa pia kuwatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu katika kazi hii: Dkt. Jacktone Onyango na Mwl. Everlyn Mudhune kwa kuniongoza katika kukamilisha kazi hii. Bila ya usaidizi wao na kujitolea kwao kwa dhati, kazi hii haingefikia kiwango ilichofika au hata haingekamilika.

Shukurani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili hasa wale ambao walioongoza masomo yangu ya shahada ya uzamili hadi lengo langu likatimia. Ningependa kuwashukuru Prof. Mbaabu, Prof. King'ei, Prof. Ndungo, Dkt. Wafula, Dkt. Mwihaki, Dkt. Chacha, Dkt. Osore, Dkt. Maitaria, Dkt. Ngugi, Dkt. Arege na Mwl. Gathenji kwa mchango wao.

Nashukuru Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu. Aidha, natoa shukurani kwa wanafunzi wenzangu: Adelaide, Lucy, Tabitha, Winnie, Nasimiyu, Njeri, Grace, Evans, Juma, Judy, Wambua, Elizabeth, Rebecca, Koske na Kehongo kwa kunitia moyo kila wakati. Shukurani maalum ziwaendee Caroline, Chege na Faith wa maktaba ya idara ya Kiswahili.

Shukurani jazila kwa wazazi wangu William Koech na Rael Koech pamoja na ndugu yangu na shangazi yangu Eunice Maiyo na familia yake. Mwisho namshukuru rafiki yangu wa dhati Joshua kwa mahimizo na uvumilivu wake wakati wa utafiti. Ningependa kuwashukuru binamu zangu Faith, Hillary, Ebby na Velarie kwa kunipa furaha wakati wote. Mungu awabariki nyote.

UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Akronimu	Mbinu ya kufupisha maneno ili kuibuka na neno jipya kwa kutumia silabi za mwanzo za kila neno ili kuunda dhana mpya.
Facebook	Ni mtandao wa kijamii unaowezesha watu kuunda akaunti ili kuwasiliana.
Mitandao ya Kijamii	Ni tovuti au programu inayokuruhusu kuungana na marafiki na familia, na kushiriki taarifa, picha na video kupitia kwa mtandao.
Mtandao	Ni mfumo wa kushirikiana kwa kompyuta unaowezesha tarakilishi mbalimbali duniani kuwasiliana kati yazo.
Neticen	Ni jamii ya watumiaji wa lugha mtandao yaani (Netspeak).
Netspeak	Ni lugha maalum inayotumika kwenye mazingira ya kielektroniki.
Twita	Ni mtandao wa kijamii ambao huwezesha watumiaji kutuma na kusoma ujumbe mfupi ulio na takriban maneno 140.
Udondoshaji	Hali ya kuwacha neno fulani au sehemu ya neno ili kufanya kuwa fupi.
Vifupisho	Ni njia ya kutaja au kuandika maneno kwa namna fupi kuliko kawaida.
Wikipedia	Ni kitabu cha mtandao kinachojaribu kukusanya ujuzi wote wa binadamu.

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKITA	Baraza la Kiswahili ya Tanzania
CHAKITA	Chama cha Kiswahili cha Taifa
CHAKIKE	Chama cha Kiswahili cha Kenyatta
IP	Internet Protocal
KBC	Kenya Broadcasting Corporation
KICD	Kenya Institute of Curriculum Development
SWAKO	Kongamano la Kiswahili Colloquium
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TCP	Transmission Control Protocols
TEKNOHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
UTU	Uchanganuzi Tahakiki Usemi

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia suala la **matumizi ya mbinu za ufupishaji katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili**. Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha mbinu mbalimbali zinazotumika katika kufupisha maneno ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao. Katika kufanya hivyo, utafiti huu umechunguza matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii na kuonyesha njia kadhaa ambazo mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia imekuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa lugha ya mtandao huhusu matumizi ya vifupisho, vifupisho hivyo vimebainishwa na athari zake katika lugha ya Kiswahili. Nadharia ambayo imeongoza utafiti huu ni nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU). Nadharia hii hujaribu kueleza uhusiano uliopo kati ya matukio ya kiusemi, siasa, matini, jamii, na utamaduni unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unavyoweza kuathiri matukio katika jamii. Data ya utafiti huu ilipatikana kwenye maktaba na mtandao. Mtafiti ametumia njia ya kimakusudi na sampuli kolezi ili kufikia malengo ya utafiti huu. Data ya utafiti imekusanywa kutoka kwa mitandao mitatu ya kijamii; Facebook, Twita na Wikipedia hasa kwa kuzingatia ujumbe ulioandikwa. Tumekusanya matini ambayo yameandikwa katika lugha ya Kiswahili na hasa yale ambayo yamefupishwa. Matini yaliyokusanywa ni yale ambayo watumiaji wake wametumia mbinu ya akronimu, ufupishaji, kubadilisha na kuchanganya msimbo. Data imechanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi. Uchanganuzi wa data ulizingatia hatua tatu kutegemea malengo ya utafiti. Data ya utafiti huu imewasilishwa kwa njia ya kimaalezo na kwa kutolea mifano katika majedwali. Data iliyochanganuliwa imewekwa katika sura tano tofauti hasa kulingana na maswali na malengo ya utafiti. Maelezo toshelevu yamejumuisha utangulizi na mahitimisho ya kila sura. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa vifupisho vinatumika sana katika mawasiliano ya kimtandao. Jambo hili haliwezi kuepukika wakati huu wa maendeleo ya Ki-TEKNOHAMA. Kwa hivyo, utafiti huu umechangia kuweka wazi matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Pia, utafiti umefafanua namna ya kutumikiza vifupisho katika lugha ya Kiswahili kwenye mitandao ya kijamii. Kwa kufanya hivi, utafiti huu umeonyesha kuwa pana haja ya kubuni kamusi za vifupisho vya lugha ya Kiswahili ambavyo vitatumika katika kutoa mwongozo wa mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii. Mwisho, licha ya athari za vifupisho ambazo zimeainishwa katika utafiti huu, mbinu za kukabiliana na athari hizi zimefafanuliwa ili kuendeleza na kukuza lugha sanifu ya Kiswahili katika ulimwengu wa uvumbuzi wa ki-TEKNOHAMA.

YALIYOMO

Mada ya utafiti	i
Ikirari	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ufafanuzi wa Dhana Muhimu.....	v
Orodha ya Vifupisho	vi
Ikisiri	vii
Orodha ya Yaliyomo	viii

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	5
1.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Malengo ya Utafiti.....	6
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	6
1.6 Upeo na Mipaka.....	8
1.7 Misingi ya Nadharia.....	9
1.7.1 Uchanganuzi Tahakiki Usemi.....	9
1.7.2 Mihimili ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi.....	12
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada.....	14
1.9 Mbinu za Utafiti.....	17
1.9.1 Muundo wa Utafiti.....	17
1.9.2 Mahali pa Utafiti.....	18
1.9.3 Usampulishaji.....	18
1.9.4 Ukusanyaji wa Data.....	19
1.9.5 Uchanganuzi wa Data.....	19
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo.....	20

1.10 Hitimisho.....	20
---------------------	----

SURA YA PILI

MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

2.0 Utangulizi.....	21
2.1 Mtandao wa Kijamii.....	21
2.2 Kitandazi cha Facebook.....	23
2.2.1 Historia Fupi ya Facebook.....	23
2.2.2 Orodha ya Baadhi ya Misamati ya Kiswahili inayotumika katika Facebook.....	25
2.3 Twita.....	32
2.3.1 Historia kuhusu Twita.....	32
2.4 Wikipedia.....	34
2.5 Hitimisho.....	36

SURA YA TATU

MBINU ZA KUFUPISHA MANENO YA KISWAHILI

3.0 Utangulizi.....	37
3.1 Maana ya Lugha Mtandao.....	40
3.2 Sifa Bainifu za Lugha Mtandao kwa Ujumla.....	43
3.2.1 Uunganishaji wa Maneno.....	44
3.2.2 Matumizi ya Akronimu.....	45
3.2.3 Matumizi ya ishara (emoticons).....	46
3.2.4 Matumizi ya Viakifishi vingi.....	47
3.2.5 Udondoshaji.....	48
3.2.6 Matumizi ya Nambari.....	49
3.2.7 Matumizi ya lugha isiyo Sahihi.....	50
3.2.8 Matumizi ya Maneno Machache Huru.....	51

3.3 Mbinu Zinazotumiwa Kufupisha Maneno ya Kiswahili Mtandaoni	51
3.3.1 Ufupishaji: Dhana ya Ufupishaji.....	51
3.3.2 Akronimu.....	53
3.3.3 Ufinyaji.....	53
3.3.4 Ufupishaji Mkato	54
3.3.5 Matumizi ya Nambari na Herufi/Maneno.....	61
3.3.5.1 Nambari 1	62
3.3.5.2 Nambari 2.....	63
3.3.5.3 Nambari 3.....	63
3.3.5.4 Nambari 4.....	64
3.3.5.5 Nambari 5.....	65
3.3.5.6 Nambari 6.....	65
3.3.5.7 Nambari 7.....	65
3.3.5.8 Nambari 8.....	66
3.3.5.9 Nambari 10.....	66
3.3.5.10 Nambari kuchukua Nafasi ya Fonimu.....	67
3.3.6 Kufanya neno kuwa Finyu.....	69
3.3.7 Kubadilisha Silabi/ herufi moja na Herufi nyingine inayokaribiana Kimatamshi.....	70
3.3.7.1 Matumizi ya 'C' badala ya kikanushi 'si'	70
3.3.7.2 Matumizi ya herufi 'G' badala ya 'ji'	71
3.3.7.3 Matumizi ya herufi 'Q' badala ya (kiu).....	72
3.3.7.4 Matumizi ya herufi 'x' badala ya 's'.....	73
3.3.8 Kuchanganya Ndimi/Msimbo.....	73
3.3.8.1 Kuchanganya Nambari na Maneno.....	76
3.3.8.2 Kuchanganya Silabi au maneno ya lugha mbili.....	78
3.4 Utata unaozuka katika matumizi ya Netspeak.....	80
3.5 Sababu za Kufupisha.....	81
3.5.1 Kuokoa muda na kuhifadhi kawi.....	81

3.5.2 Kutumia Idadi Ndogo ya Maneno.....	82
3.5.3 Kupunguza Gharama ya kutuma Ujumbe.....	82
3.5.4 Kuwa Mbunifu.....	83
3.5.5 Upigaji chapa kwa haraka.....	83
3.6 Sheria za Lugha Mtandao katika Mawasiliano.....	83
3.6.1 Sheria ya KK- konsonanti konsonanti.....	84
3.6.2 Sheria ya Kubadilisha Konsonanti.....	84
3.6.3 Kudondosha vokali katikati mwa konsonanti mbili.....	85
3.6.4 Kukubali Mfumo wa Sauti kutoka Lugha nyingine.....	85
3.6.5 Nambari mbili kutokea kwa pamoja.....	85
3.7 Hitimisho.....	87

SURA YA NNE

ATHARI ZA VIFUPISHO AU NETSPEAK KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

4.0 Utangulizi.....	88
4.1 Athari hasi zinazotokana na Lugha ya Mtandao.....	88
4.2 Athari Chanya zinazosababishwa na matumizi ya Vifupisho.....	101
4.3 Hitimisho.....	102

SURA YA TANO

HITIMISHO LA UTAFITI

5.0 Utangulizi.....	103
5.1 Muhtasari wa Utafiti.....	104
5.2 Matokeo ya Utafiti.....	104
5.3 Mchango wa Utafiti.....	109
5.4 Changamoto za Utafiti.....	111
5.5 Utoshelevu wa Nadharia.....	110
5.6 Mapendekezo.....	111
Marejeleo.....	115

Kiambatisho.....122

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Tunaishi katika enzi ambapo teknolojia ya mtandao inazidi kuathiri karibu nyanja zote za maisha. Kwa hakika, karibu kila eneo la maisha ya binadamu katika ulimwengu wa sasa limeathiriwa na mitandao ya kijamii. Si jambo la kupiga chuku tukiungama kuwa lugha ya Kiswahili imetumika katika sekta mbalimbali iwe katika mawasiliano, biashara, masomoni na vyombo vya habari.

1.1 Usuli wa Mada

Mitandao ya kijamii ni aina ya teknolojia ya kielektroniki inayorahisisha mawasiliano na mahusiano ya watu kwenye mtandao na huweza kutokea kupitia kwa matumizi ya tarakilishi au teknolojia ya simu. Mtandao ni mfumo wa kushirikiana kwa kompyuta mbalimbali kote duniani unaowezesha kompyuta hizo kuwasiliana kati yazo. Kupitia mtandao huu watu wanaweza kutembelea tovuti mbalimbali kwa ajili ya shughuli za kila siku kama vile: biashara, masomo, siasa, dini na uchumi (William et al 2009).

Asili ya mtandao ina mizizi katika mwongo wa 1960 wakati Marekani ilihusika katika vita vya maneno au propaganda. Mitandao ilianzishwa wakati wanajeshi walikuwa wanatafuta mbinu za kusambaza habari nchini kote. Mtandao ni mfumo wa ulimwengu wa mitandao ya kompyuta na hutumia itifaki inayokubalika ya 'internet Suite' (TCP / IP) na inayotumikia mabilioni ya watumiaji duniani kote. TCP / IP ni mtandao wa mitandao ambayo ina mamilioni ya mitandao ya kibinafsi, ya umma, ya kielimu, ya biashara, na ya serikali yenye upana wa kimitaa na kiulimwengu.

Kiswahili kimeweza kutumika kama lugha ya mawasiliano na kupiga hatua katika teknolojia hii ya mitandao. Ni bayana kuwa, lugha ya Kiswahili imekuwa lugha ya kimataifa ambayo inasomwa kwenye mitandao. Lugha ya Kiswahili pia ni chombo mwafaka cha kusambaza ujuzi wa kiteknolojia hasa katika maeneo yanayotumia lugha hii barani Afrika (Mohochi 2002).

Utandawazi ulianza kuingia polepole katika lugha ya Kiswahili tangu enzi za utawala wa Kikoloni. Hii ni kwa sababu utawala wa kikoloni uliambatana na kuanzishwa kwa vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, runinga, tovuti na simu ambao uliimarisha utandawazi na Kiswahili kupata matumizi makubwa. Hali hii ilisababisha mabadiliko kadha wa kadha hususan katika lugha ya Kiswahili. Mabadiliko hayo yanaweza kujidhihirisha katika nyanja mbalimbali kama vile; utamaduni, dini, elimu, biashara na utawala. Vyote hivi kwa pamoja vilisaidia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika (Bakita, 2004). Matumizi ya mitandao ya kijamii yameenea kote ulimwenguni na asilimia 67% wanatumia mitandao katika shughuli zao za kila siku (Nielson 2009).

Kulingana na mtandao wa Alexa. Com, nchini Kenya mtandao ambao huwavutia mamilioni ya watu ulitumika kwa mara ya kwanza katika mwaka wa 1993. Kuna mitandao mbalimbali kama vile: Facebook, Twita, LinkedIn, Olx, Blogu na Google. Mitandao ya Facebook, Olx na Twita ndio maarufu sana na hutumiwa na watu mbalimbali kwa shughuli tofauti tofauti kama vile: biashara, utangazaji, elimu na siasa. Katika mwaka wa 2008, mtandao wa Facebook ulikuwa na washiriki milioni mia sita. Kufikia Machi 2013, waliotumia mtandao kote duniani kila siku walikuwa bilioni moja. Kwa upande wa Twita washiriki ni milioni mia tano (Gazeti la Daily Nation 2, 17 Juni 2014).

Lugha ya Kiswahili imepitia mabadiliko makuu katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii. Sababu kuu ikiwa asimilia kubwa ya watumiaji ni vijana ambao wanataka kupitisha ujumbe baina yao kwa haraka iwezekanavyo. Kulingana na Fagan na Desai (2003), asimilia 40% ya wanaotumia mtandao wa kijamii ni vijana wa kati ya miaka 16-18, wakifuatwa na asimilia 35% ambao ni wanafunzi wa vyuo, asimilia ya 15 % ni wale ambao hawajapata elimu na mwisho, asimilia 10% ni watu wazima kutoka miaka 66 na zaidi. Watumiaji hawa wamebuni mtindo mpya kwa kufupisha maneno na kuufanya kuwa maarufu sana miongoni mwao. Lugha hii huitwa lugha mtandao 'Netspeak' na watumiaji wanaitwa 'Neticen'.

Matumizi ya lugha mtandao 'Netspeak' ilianza mwaka wa 1978 kutokana na mawasiliano kupitia mitandao ya kompyuta na ujumbe katika simu (Jagero na Wengine, 2013). Matumizi ya 'Netspeak' inaendelea kukua na hubadilika kila uchao kwa vile ni mbinu rahisi katika kutuma ujumbe. Pia kila siku dhana mpya na mtindo mpya huibuka na utaendelea kuimarika na kusambaa. Matumizi ya akronimu, tanakali za sauti, ishara, na ufupishaji ni mifano ya 'Netspeak'. Kulingana na Crystal (2004:24) lugha mtandao ni aina ya lugha inayodhihirisha sifa za kipekee za mtandao. Mcfedries (2004) vilevile anasema kuwa lugha mtandao ni maneno, misemo, tahajia ya kipekee na sarufi iliyō na sifa za kimtandao na kimawasiliano. Mbali na matumizi ya vifupisho vya kimtandao dhana ya ufupisho pia hutambuliwa katika silabasi ya Kiswahili ya shule za upili (KIE, 2002). Mbinu za ufupishaji hufunzwa katika viwango mbalimbali vya elimu.

Lugha mtandao imebadili maumbo ya maneno kwa sababu ya matumizi ya vifupisho mbalimbali. Hii ni kwa sababu matumizi ya vifupisho hivyo hupunguza urefu wa maneno na

kuepuka urudiaji, ili kuokoa muda na gharama ya kutuma ujumbe. Aina za vifupisho vimeathiri sana lugha ya Kiswahili kwa kuvunja kanuni za hijai na sarufi hivyo kuzuia ukuaji wa lugha. Matumizi ya herufi za mwanzo, ishara na akronimu huongezeka kila uchao katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii.

Matumizi ya vifupisho vya Kiswahili vimekuwepo na kukubalika miongoni mwa wanajamii. Mifano ya tangu jadi ni kama vile: Sanduku la Posta (S.L.P), kama vile (K.V) na kadhalika (N.K). Kuna vifupisho vingine ambavyo vimebuniwa ingawa havijakubalika na jamii pana. Baadhi ya maneno haya ni kama vile neno wakati ambalo huendelezwa hivi (wkt), katika (ktk), matumizi (mtz), sasa (xaxa), kabisa (kbs), pamoja (pa1), lakini (lkn) na sijui (cjui). Wataalamu wengi hawakubaliani kuhusu matumizi ya vifupisho kwa vile mara nyingi havizingatii sheria ambazo zinapaswa kuzingatiwa (Varnhagen et. al. 2009).

Batul (2009), anasema kuwa ufupishaji umejikita sana katika maisha ya vijana, hivyo kuleta madhara makubwa katika matumizi ya lugha mbalimbali zikiwemo lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Matokeo haya yameathiri sana ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Naye Rua (2005), anasema kuwa ufupishaji sio kuondoa herufi za maneno mwishoni mwa maneno pekee bali hujumuisha miundo ya maneno ambayo huondolewa mwanzoni, katikati au sehemu nyingine katika neno moja. Anaendelea kusema kuwa miundo yote ya maneno ambayo ni mafupi kuliko neno asilia ni ufupishaji.

Lugha hii imepata umaarufu kama lingua franka ya Afrika Mashariki na Kati na inatumika kwa wingi katika vyombo vya mawasiliano ya umma kama vile redio, runinga, magazeti, majarida na

mtandao. Kupitia shirika la habari la BBC SWAHILI, Kiswahili kimekuwa lugha ya nne kutumika na watu kupitisha maoni yao kwenye mitandao ya kijamii hususan Twita. Kiingereza kikiwa lugha ya kwanza, Kiarabu ya pili, Kihispania ya tatu ikifutwa na Kiswahili.

1.2 Suala la Utafiti

Lugha mbalimbali kote ulimwenguni zimepitia mabadiliko makuu na sababu kuu ni matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii. Lugha ya Kiswahili haijapiga hatua katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii kama ilivyo lugha ya Kiingereza. Utafiti wetu umeshughulikia mbinu zinazotumika kufupisha maneno ya Kiswahili na athari zake katika lugha ya Kiswahili. Imeshughulikia mitandao ya kijamii ambayo hutumia lugha ya Kiswahili hasa katika utangazaji wa habari, mawasiliano ya kawaida, shughuli za kiakademia na biashara. Hata hivyo wanaotumia mitandao sana ni vijana wanaotaka kutuma ujumbe haraka na kwa urahisi na hivyo wameunda lugha yao ya mtandao inayoitwa lugha mtandao au ‘Netspeak’. Lugha mtandao imeathiri sana lugha zote iwe Kiswahili au Kiingereza; hii ni kwa sababu watumiaji wengi wanafupisha maneno ili kurahisisha mawasiliano yao na kutuma ujumbe kwa urahisi na hata kupunguza gharama ya kutuma ujumbe wao. Vilevile wanaotumia vifupisho wanataka kutumia maneno machache ili kuokoa muda wa kuandika maneno mengi kwa wakati mmoja.

Utafiti wetu unahusu matumizi ya mbinu za ufupishaji katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili kwa vile tafiti nyingi hazijafanywa katika sehemu hii. Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi imetumika katika utafiti huu kwa sababu namna matumizi ya lugha katika matini ni jambo muhimu sana. Kwa hivyo, utafiti huu umedhamiria kujaza pengo lililoachwa na watafiti wa awali na kuikuza lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii.

Utafiti huu umeshughulikia mitandao mitatu ya kijamii: Facebook, Twita, na Wikipedia. Ili kuafiki malengo haya, matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii itajadiliwa. Mbinu za ufupishaji zinazotumika katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili zitabainishwa.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umejibu maswali matatu:

1. Kiswahili kinatumika vipi katika mitandao ya kijamii?
2. Ni mbinu zipi zinazotumika kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii?
3. Vifupisho vya kimtandao vina athari gani katika lugha ya Kiswahili?

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo matatu:

1. Kujadili matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii.
2. Kubainisha namna mbinu za ufupishaji zilivyotumika katika mitandao ya kijamii.
3. Kuchunguza athari za vifupisho vya kimtandao katika lugha ya Kiswahili.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kuna sababu kadha ambazo zimetufanya kuchagua mada hii: Kwanza imetokana na kuzuka kwa teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao ambayo imekuwa maarufu sana katika matumizi yake. Teknolojia hii ya mitandao ya kijamii ni jambo geni sana kwa hivyo inastahili kutafitiwa. Kulingana na shirika la utangazaji la BBC, Kiswahili ni lugha ya nne katika matumizi ya

mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii, Kiingereza kikiwa lugha ya kwanza, Kiarabu ya pili, Kihispania ya tatu na lugha ya Kiswahili ikitamatisha katika orodha hii.

Sababu ya pili ni kuwa, Kiswahili hakijahusishwa sana katika mitandao ya kijamii kama ilivyo lugha ya Kiingereza. Kuna juhudi ambazo zimefanywa ili kuhusisha Kiswahili katika mitandao kama vile kuundwa kwa istilahi za Kiswahili katika kitandazi cha Facebook. Vilevile katika mwaka wa 2009 Facebook ilizinduliwa katika lugha ya Kiswahili na ikaitwa *Sura Kitabu*. Mitandao ya kijamii imeleta manufaa kwa wanajamii na kwa hivyo mtafiti atachunguza mitandao ya Facebook, Twita, na Wikipedia, kwa sababu Kiswahili hutumika sana katika mitandao hiyo. Mitandao ya kijamii pia imetumika sana katika sekta ya elimu na utangazaji. Teknolojia hii ya mtandao imejikita katika ujuzi wa lugha inayotumika katika mawasiliano na huwa inasambazwa kupitia lugha husika. Tarakilishi na simu ni vipengele muhimu vya utandawazi kwa sababu huunganisha watu wengi kote ulimwenguni kupitia mtandao. Sababu ya tatu ni kuwa lugha ambayo hutumika katika mawasiliano ya kimtandao ni lugha ya ufupishaji. Hii hutokana na sababu kuwa asimilia kubwa ya watumizi ni vijana ambao wanataka kuwasilisha ujumbe haraka iwezekanavyo na mawasiliano baina yao huwa ya papo kwa hapo.

Mitandao ya kijamii ni jambo ambalo haliwezi kuepukika kabisa katika maisha ya watu hasa katika enzi hizi ambapo teknolojia imeenea sana na kuathiri sekta zote za maisha. Tafiti zilizofanywa kuhusu mada hii bado ni chache, kwa mfano kuna watafiti kama vile Kamau (2005), aliyeshughulikia matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi na katika utafiti wake aligusia kidogo tu kuhusu injini pekuzi ya mtandao. Naye Moraa (2012) ameshughulikia matumizi ya Kiswahili katika mradi wa *Microsoft East Africa*. Alibainisha mbinu zilizohusika katika uundaji

wa msamiati katika mradi huo. Aidha, alichunguza jinsi mbinu ambazo zilitumika zimechangia katika kukikuzi na kukiendeleza Kiswahili kama lugha ya teknolojia. Utafiti wetu umeshughulikia mitandao ya kijamii itumiayo Kiswahili, mbinu za ufupishaji wa maneno ya Kiswahili (Netspeak) katika mitandao ya kijamii na athari za ufupishaji katika lugha ya Kiswahili.

1.6 Upeo na Mipaka

Hivi sasa Kiswahili kinaendelea kutumika katika miradi mingi ya tarakilishi ya mtandao kama vile mradi wa kugeuza matini ya Kiswahili hadi usemi na mradi wa injini pekuzi ya Kiswahili katika mtandao (Google), na matumizi ya Kiswahili katika mradi wa *Microsoft East Africa*. Mitandao ya kijamii ni mingi sana kama vile: *Olx, LinkedIn, Myspace, Twita, Facebook, Whatsapp, Blogu, Google* na *Mdahalishi*. Utafiti huu hata hivyo, umeshughulikia mitandao mitatu ya kijamii: Facebook, Twita na Wikipedia. Tulijikita katika mbinu za kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao hii. Vilevile tumechunguza namna mbinu za ufupishaji zinavyokiuka kanuni na sheria za kuunda maneno ya Kiswahili hivyo kuangalia athari za mitandao ya kijamii katika lugha Kiswahili.

Mitandao hii iliteuliwa kwa misingi ya kuwa na matumizi mengi ya Kiswahili. Vilevile lugha ya Kiswahili inayotumika katika mitandao hii ni ufupishaji kwa sababu watu wanataka kutumia maneno machache kutuma ujumbe kwa haraka ili kupunguza gharama. Tumeshughulikia mtandao wa Facebook kwa vile ni maarufu nchini Kenya; na pia watu wengi wamejiunga na mtandao huu kwa shughuli za mawasiliano ya kila siku. Mtandao wa Twita ndio mtandao ambao umebainika kutumia ufupishaji sana kama njia ya kipekee ya kuwasiliana (Tweetnet, 2011).

Wikipedia ni mtandao wa wataalamu mbalimbali, na Kiswahili kinachotumika pale kimeimarika sana ikilinganishwa na mitandao mingine. Vilevile tumechunguza namna ambavyo wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu wanatumia vifupisho na kulinganisha na wale ambao kiwango chao cha elimu hakijaimarika sana. Kategoria hii ya watumiaji ilituliwa ili kuelewa iwapo wanafuata kanuni za kuunda vifupisho hivyo vya kimtandao au la. Vilevile tumechunguza athari za vifupisho vya kimtandao kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu athari za kifonolojia na kimofolojia hujitokeza. Kimofolojia vifupisho vimemeathiri mpangilio na uundaji wa maneno kwa mfano, watumiaji wengi wanachanganya nambari na maneno ili kuunda sentensi. Kifonolojia vifupisho vimeathiri matamshi ya maneno kwa sababu watumiaji wanadondosha sauti moja na kuingiza sauti ambayo ni karibu sawa na ya kwanza kimatamshi au kuchukua silabi kutoka lugha ya Kiingereza na kufanya zitamkike kama za Kiswahili. Katika mitandao hii tuliangalia matini za watumizi ambayo yameandikwa.

1.7 Msingi wa Nadharia

1.7.1 Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU)


Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU). Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha katika matini ni jambo muhimu sana katika nadharia hii. Nadharia hii iliasisiwa na Norman Fairclough (1989), na hushughulikia masuala ya lugha na utamaduni wa jamii, inachunguza miktadha ya kijamii kwa kutazama lugha kama uzoefu wa wanajamii. Iliundwa kwa lengo la kutumiwa katika isimujamii. Ilitumika kuchanganua lugha na namna inavyotumika kubainisha utabaka unavyodhihirika miongoni mwa wanajamii. UTU huonyesha lugha kama kifaa muhimu katika shughuli za kijamii ambayo husaidia katika ufafanuzi wa maana katika jamii kwa kujadili mabadiliko yanavyotokea kijamii na kitamaduni.

Nadharia ya UTU ilichimbuka kutokana na isimu jadilifu ambayo ilianzishwa katika Chuo Kikuu cha *East Anglia* katika miaka ya 1970. Wanaisimujamii walikuwa wakilithamini kwa uchache suala la utabaka wa kijamii na mamlaka. Mtazamo huu uliasisiwa mwanzo huko Lancaster school of linguists na Norman Fairclough. Ruth Wodak (2002) pia ametoa mchango mkubwa katika utafiti wa nadharia hii.

Fairclough alibuni nadharia yenye mihimili mitatu ya kutafiti mazungumzo ambapo lengo lake ni kubaini aina tatu tofauti za uchambuzi: Uchambuzi wa matini ya lugha (simulizi au andishi), uchambuzi wa uzungumzaji (mchakato wa utoaji matini, usambazaji na utumizi) na uchambuzi wa mijadala ya matukio kama shughuli za utamaduni wa jamii.

Uchanganuzi Tahakiki Usemi huweza huonyesha maana ya lugha kama zao linalotokana na uhusiano baina ya muktadha na utamaduni wa kijamii. UTU hutumia lugha katika kudumisha mahusiano ya kijamii na ya lugha husika inapochukuliwa kama mchakato wa kijamii. Uchanganuzi wa usemi hudhihirisha michakato mitatu, matini, miktadha na mahusiano.

(1.1) Kielelezo cha muundo wa usemi



Kwa mujibu wa Fairclough (1989: 25)

Katika kielelezo hiki matini huwakilisha matamshi, maandishi, au lugha ishara. Matini ni zao katika mchakato wa uzalishaji na ni rasilimali katika mchakato wa ufasiri. Michakato ya uzalishaji na michakato ya ufasiri huathiriwa na hali za kijamii. Usemi kwa hivyo huhusisha matini, mahusiano na miktadha. Katika uchanganuzi, mchanganuzi lazima basi kuchanganua uhusiano kati ya matini, mahusiano na miktadha.

Kulingana na Fairclough (1989) na Haliday (2004), uchanganuzi usemi ni sehemu ya Tahakiki Usemi na hakuna mchakato unaokamilisha uzalishaji bila kuzingatia namna mchakato huo unavyoathiri masuala ya kijamii. Nadharia ya UTU inapodhihirisha lugha kama uzoefu wa kijamii ina maana kuwa lugha hudhibitiwa na vikwazo vinavyopatikana katika jamii wala sio vya kiisimu.

Wodak na Meyer (2001), wanasema kuwa Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU) huchunguza mahusiano angavu na yasiyo angavu yanayohusiana na nguvu, uwezo, itikadi na ubaguzi ambayo hudhihirika kupitia usemi. Usemi ni kule kujieleza kwa kutumia maneno; ni jina linalopewa maumbo ya lugha yanayozidi sentensi moja (Brown na Yule 1981).

Kulingana na Van Dijk (1993), UTU huweza kutumiwa katika uchunguzi wa kiisimu, kisimiotiki na usemi. UTU huchunguza dhana ya utawala ambayo huendelezwa na usemi. Anaendelea kusema kuwa, UTU huchukulia matini kuwa maandishi au usemi, picha, filamu, tangazo, muziki au chochote kile kinachoweza kuchanganuliwa. Kwa mujibu wa Crystal (1997), Uchanganuzi Tahakiki Usemi huonyesha uhusiano uliopo kati ya matukio ya kiusemi, siasa, jamii na utamaduni hasa kuambatana na vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii.

1.7.2 Mihimili ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi

Fairclough (1989) anapendekeza mihimili ambayo usemi huundwa na kuendelezwa.

(a) **Muundo wa jamii**, muundo wa kijamii hutegemea vikwazo vya kijamii ambavyo ni, tabaka, hadhi, cheo, umri, kabila na jinsia. Wodak (2002) anasema kuwa usemi ni matini andishi yanayofaa kuwakilishwa kimatamshi.

(b) **Utamaduni**, huhusu imani, mila, desturi na asasi za kijamii zinazomtambulisha mwanajamii. Yale tusemayo nyumbani au mahali popote pale hutegemea hali yetu ya kijamii na nafasi zetu katika jamii.

(c) **Usemi** huhusu maneno na lugha inayotumika kubainisha sifa zetu, mahusiano baina ya watu, mfumo wa maarifa na imani. Usemi (matumizi ya lugha) huunda au hujenga jamii.

(e) **Ufafanuzi**- mhimili huu hujikita katika miliki za matini yaani ni nani humiliki matini hizi? Kumaanisha kuwa matini huelekezwa na kumilikiwa na hata kudhibitiwa na miundo ya kijamii na masharti ya utamaduni. Matumizi yoyote hupata maana kwa kuzingatia mahusiano ya miktadha ya kijamii kama utamaduni.

(f) **Fasiri na Fasili**- ufasiri hujihusisha na uhusiano kati ya matini na mahusiano. Katika ufasiri michakato tambuzi ya washiriki huchanganuliwa. Ufasili hushughulika na uhusiano kati ya mahusiano na muktadha wa jamii ambapo jamii huamua michakato ya uzalishaji na ya ufasiri na athari zake.

(g) **Viwango vya uchanganuzi**- Viwango hivyo ni pamoja na matini yenyewe, michakato ya usemi inayohusu kubuni, kuandika, kuongea, kusoma na kusikiliza. Muktadha huhusu miktadha mipana ya kijamii, ambayo huathiri usemi na michakato yake (Fairclough, 1989).

(h) **Itikadi** hurejelea umbo la kijamii na namna ambayo matumizi ya ishara hutumika katika jamii. Hii ni kwa sababu itikadi ni muhimu katika Uchanganuzi Tahakiki Usemi kwa vile huanzisha na kudumisha uhusiano wa utawala usio sawa. Vilevile UTU huchunguza namna lugha hutumiwa katika upatanishi wa itikadi katika asasi zote za kijamii. Itikadi ni taaluma inayohusu namna maana huundwa na kuwasiliswa kwa kutumia njia tofauti tofauti.

(I) **Dhima ya lugha katika uchanganuzi**, uchanganuzi hutumia matamshi na maandishi kama umbo la kijamii. Uchanganuzi usemi huelezwa kama tendo la kijamii kwa vile hushughulikia uhusiano wa kilahaja baina ya wanajamii. Katika utafiti huu tutatumia mihimili miwili: muundo wa usemi na viwango vya uchanganuzi.

Muundo wa usemi hutegemea vikwazo vya kijamii kama vile umri, tabaka na cheo. Mhimili huu umetusaidia kwa sababu usemi ni matini andishi yanayofaa kuwakilishwa kimatamshi na huathiriwa na vikwazo vya kijamii kama vile tabaka, cheo umri na jinsia. Kwa hivyo kupitia kwa tabaka la vijana ambao ni wengi katika jamii imebainika kuwa vifupisho vinatumika kwa wingi. Vifupisho vinatumika sana kwa sababu ya kutaka kujiweka katika tabaka fulani na pia kwa ajili ya kuokoa muda na kupunguza gharama ya kutuma ujumbe.

Mhimili wa viwango vya uchanganuzi huchunguza uhusiano uliopo baina ya viwango vitatu vya uchanganuzi: matini yenyewe, michakato ya usemi inayohusu kubuni, kuandika, kuongea, kusoma na kusikiliza na jamii kwa ujumla ambayo hutumia michakato hii. Mhimili huu umetusaidia kuchunguza uhusiano uliopo kati ya vifupisho, michakato ya usemi na jamii kwa sababu vifupisho ni matini ambayo yamerekodiwa kupitia maandishi na huwakilisha matendo na imani zetu. Matini vilevile ni elementi ya matukio ya kijamii ambayo huleta mabadiliko ya kitajriba, imani, mielekeo na thamani. Kwa hivyo, nadharia hii kwa ujumla ilitusaidia kuchunguza namna vifupisho vinavyoundwa na kutumika katika jamii.

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Kwa mujibu wa Khayesi (2002) aliyechunguza matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi, TEKNOHAMA ni kiungo muhimu sana cha utandawazi. Kwa hivyo matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi yataingizwa kikamilifu katika TEKNOHAMA. Hivi basi lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika ambayo kwa kweli ina nafasi bora zaidi ya kuwa lugha ya utandawazi barani Afrika. Utafiti wake ni muhimu kwetu kwa vile unarejelea matumizi ya Kiswahili katika

teknolojia kama ulivyo utafiti wetu. Tofauti ni kuwa wake umejikita katika tarakilishi na wetu kwenye mitandao ya kijamii.

Crystal (2004:10), katika kitabu chake *'Language and Internet'* amezungumzia kwa ujumla nafasi ya lugha kwenye mtandao na athari za mtandao katika lugha. Amejadili matumizi ya vifupisho vya kimtandao katika lugha ya Kiingereza na utafiti wetu huhusu mtandao katika lugha ya Kiswahili. Maandishi haya yatatufaa kwa upande wa athari za mitandao kwa lugha ya Kiswahili na vilevile katika matumizi ya lugha mtandao ambayo ni kiini cha utafiti wetu.

Kuna tafiti zilizofanywa kama vile: Kamau (2005) aliyeshughulikia matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi, alizungumzia mradi wa *Microsoft East Afrika*, mradi wa kugeuza matini za Kiswahili hadi usemi na kwa ufupi injini pekuzi ya Google. Naye Moraa (2012), akashughulikia matumizi ya Kiswahili katika *mradi wa Microsoft East Afrika* hasa mbinu za kuzalisha istilahi za Kiswahili katika mradi huo. Vilevile Maina (2013), katika Makala ya Chakita alizungumzia makundi ya lugha na fasihi katika Facebook. Utafiti wetu ni tofauti na wao kwa sababu tumeshughulikia kwa undani mitandao tatu ya kijamii hivyo utafiti wao umeboresha utafiti wetu.

Batul (2009) katika utafiti wake anaeleza kuwa lugha mtandao 'Netspeak' ina athari zake katika lugha mbalimbali hasa katika enzi hizi ambazo asimilia kubwa ya vijana wanatumia mitandao ya kijamii. 'Netspeak' imeathiri sana matumizi ya lugha ya Kiingereza. Anaendelea kusema kuwa tafiti nyingi hazijashughulikia athari za lugha mtandao katika lugha mbalimbali. Utafiti wake ulitufaa kwa vile tumeshughulikia athari za mitandao ya kijamii katika lugha ya Kiswahili. Pia utafiti wetu umezingatia athari za 'Netspeak' katika lugha ya Kiswahili.

Kaplan na Haelein (2010), wanafafanua kuwa mitandao ya kijamii inakuwezesha kuunda na kubadilisha habari kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Wanaendelea kusema kuwa mitandao ya kijamii inaweza kuwekwa katika kategoria mbalimbali kama vile:

- a) Miradi ya shirika kama vile Wikipedia.
- b) Blogu kama vile Twita
- c) Maudhui jumuiya kama vile Kamera za mitandao na Google
- d) Mitandao kama vile Facebook na Mdahalishi

Kati ya mitandao hii utafiti wetu utachunguza matumizi ya Kiswahili katika aina tatu za mitandao kama ilivyotajwa katika swala la utafiti.

Mutembei (2011) ametafiti kuhusu kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: tafakari kuhusu isimujamii. Utafiti wake utatusaidia kuboresha utafiti wetu kwa sababu ameangazia baadhi ya njia za kuunda vifupisho katika arafa za simu. Utafiti wetu ni tofauti na wake kwa sababu amezungumzia juu ya namna Kiswahili kinavyotumika katika simu bali wetu umeshughulikia matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao.

Utafiti wa Jagero, Mohochi na Indede (2013) umejadili kuhusu matumizi ya Kiswahili katika matini ya Blogu na athari zake katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Walitumia nadharia ya Uchambuzi Usemi Jadilifu. Walibaini kuwa washiriki wa Blogu wanatumia vifupisho, maneno yasiyo sanifu, sarufi isio sahihi, kuchanganya misimbo, ubadilishaji misimbo na matumizi ya tahajia yasiyo sahihi. Hivyo kuwa na athari chanya na hasi katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili.

Wameshughulikia matini ya kisiasa. Tofauti na wao walioshughulikia matini ya kisiasa pekee, utafiti wetu umerejelea matini ya Kiswahili katika mitandao tuliyotaja hapo juu hasa kubainisha mbinu mbalimbali za ufupishaji na athari zake katika lugha ya Kiswahili.

Naye Gikambi (2014) katika makala ya SwaKO ameshughulikia 'Mgeni njoo mwenyeji atambe'-athari za Facebook, Twita na Kamera ya mtandao katika vyombo vya habari vitumiavyo Kiswahili. Vilevile ameangalia kama Kiswahili kimekuzwa na kuendelezwa au kudidimizwa katika majukwaa haya. Makala yake iliaangazia kipengele cha kipekee cha simu za mkononi na jinsi zinavyochangia katika matumizi ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari hasa majukwaa ya Facebook na Twita. Utafiti wetu ni tofauti na wake kwa vile imeangalia jinsi mbinu za ufupishaji wa maneno ya Kiswahili inavyotumika katika mitandao ya kijamii na iwapo inadunisha lugha ya Kiswahili au la bali siyo katika vyombo vya habari.

Kwa ujumla utafiti wetu umeshughulikia matumizi ya mbinu za ufupishaji katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili, tumebainisha matini yenye maneno yaliyofupishwa katika mtandao wa Facebook, Twita na Wikipedia. Hii ni kwa sababu mitandao hii ni maarufu sana na hutumiwa na watu wengi. Vilevile tumebainisha kuwa mbinu za kufupisha maneno ya Kiswahili hazizingatii sheria na imepotosha lugha ya Kiswahili.

1.9 Mbinu za Utafiti

1.9.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo, kwa vile umeegemea maelezo na kutolea mifano katika majedwali.

Data iliyochanganuliwa imewekwa katika sura tofauti hasa kulingana na maswali na malengo ya utafiti. Maelezo toshelevu yamejumuisha utangulizi na mahitimisho ya kila sura.

1.9.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu umejikita maktabani na kwenye mtandao. Maktabani, usomaji na upekuzi mpana wa vitabu, majarida, magazeti hasa gazeti la *Taifa Leo* na tasnifu zinazohusiana na mada hii umefanywa. Vilevile tumesakura mtandao ili kusoma yale yaliyoandikwa kuhusu mada na kudondoa vifupisho. Zoezi hili limetuwezesha kung'amua dhana za kimsingi, kuelewa kwa kina mihimili ya nadharia iliyotegemewa katika uchanganuzi wa data. Aidha usomaji huu umempevusha mtafiti kuhusu mapitio ya maandishi kuhusu mada na kumsaidia kupata data muhimu iliyohitajika katika utafiti huu.

1.9.3 Usampulishaji

Usampulishaji umefanywa kwa njia ya kimakusudi na kolezi. Uteuzi wa sampuli kimakusudi unahusu uteuzi wa moja kwa moja wa sampuli yenye sifa lengwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli makusudi hutokana na uteuzi wa kimakusudi ambapo mtafiti huchagua vipengele ambavyo hutumiwa kama sampuli kuwakilisha kikundi cha watu. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kutumia watu, vitu, hali au tabia ambazo zina taarifa inayohitajika kwa kuzingatia malengo ya mtafiti. Wanazidi kueleza kuwa mbinu hii inaweza kuambatana na matumizi ya mbinu nyingine ili kupata sampuli halisi. Hii ni kwa sababu dhana ya ufupishaji hufunzwa katika shule za upili na vyuo vikuu. Mtafiti aliteua kimakusudi mitandao ya kijamii ambayo inatumia Kiswahili kama vile: Facebook, Twita na Wikipedia kutoka kwa sampuli kubwa ya mitandao iliyoweza kuzalisha data mwafaka kwa utafiti huu. Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ni usampulishaji faafu ambayo kulingana na Mugenda (2013) hutumika katika tafiti ambazo masuala yanayotafitiwa ni ya kijumla na mtu yeyote wa kawaida anaweza kuchangia. Hii ni kwa sababu mitandao ni mingi lakini si yote

imeandikwa kwa Kiswahili au ina matumizi ya Kiswahili. Sampuli kolezi pia imetumika katika kuchagua matini ya Kiswahili yaliyofupishwa katika lugha ya Kiswahili. Pia matini ambayo tumechunguza yametuwezesha kubaini kuwa watumiaji wengi hufuata kanuni na sheria za kuunda vifupisho hivyo vya kimtandao.

1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Data imekusanywa kwa kusoma tasnifu, majarida, magazeti hasa gazeti la *Taifa leo*, na vitabu ili kupata yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi. Pia tulisakura mtandao ili kusoma makala yanayohusiana na mada. Vifaa vya kukusanyia data ni pamoja na kalamu na karatasi, tarakilishi, mtandao na simu.

Data ya utafiti imekusanywa kutoka kwa mitandao mitatu ya kijamii; Facebook, Twita na Wikipedia hasa kwa kuzingatia ujumbe ulioandikwa. Maneno ya Kiswahili yaliyofupishwa yamekusanywa. Tumekusanya matini ambayo yameandikwa katika lugha ya Kiswahili na hasa yale ambayo yamefupishwa kuanzia Januari hadi Feburari 2015. Matini yaliyokusanywa ni yale ambayo watumiaji wake wametumia mbinu ya akronimu, ufupishaji, kubadilisha na kuchanganya msimbo. Baada ya kukusanywa, data imeainishwa kwa njia ya maelezo, ufafanuzi na kwa kutolea mifano katika majedwali.

1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data ya utafiti imeainishwa kulingana na malengo ya utafiti na jinsi Kiswahili kinavyokuzwa na kuendelezwa katika mitandao ya kijamii kufikia sasa. Data ya utafiti imechanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi. Uchanganuzi wa data umezingatia hatua tatu kutegemea malengo ya utafiti. Hatua ya kwanza

imehusu namna Kiswahili kimetumika katika mitandao ya kijamii. Hatua ya pili imebainisha namna mbinu za ufupishaji zimetumika na hatua ya tatu imehusu athari za vifupisho katika lugha ya Kiswahili ambapo tumetumia vigezo vya kifonolojia na kimofolojia. Kigezo cha kifonolojia kimetumika kwa vile vifupisho huathiri matamshi ya maneno ya Kiswahili. Kigezo cha kimofolojia kimetumika kwa sababu vifupisho vimeathiri mpangilio na uundaji wa maneno katika Kiswahili.

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na kwa kutolea mifano. Maelezo yamebainisha vifupisho mbalimbali vya maneno ya Kiswahili vinavyotumiwa sana katika mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia. Vilevile tumechunguza athari za vifupisho hivyo katika lugha ya Kiswahili. Data iliyochanganuliwa imewekwa katika sura tofauti hasa kulingana na maswali na malengo ya utafiti. Maelezo toshelevu yamejumuisha utangulizi na mahitimisho ya kila sura.

1.10 Hitimisho

Kwa ujumla utafiti huu umeangazia mambo ya kimsingi yanayojenga usuli wa utafiti, vipengele muhimu vya utangulizi kama vile swala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

SURA YA PILI

MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, mada ya utafiti huu ambayo ni mbinu zinazotumika kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha zilibainishwa. Katika sura hii matumizi ya Kiswahili katika mitandao mitatu ya kijamii; Facebook, Twita na Wikipedia ilishughulikiwa.

Lengo la sura hii ni kufafanua namna Kiswahili kinavyotumika katika mitandao ya kijamii. Hulenga vilevile kuchunguza nafasi ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia. Kadiri siku zinavyokwenda, na jinsi matumizi ya teknolojia mpya ya mawasiliano yanavyoongezeka katika jamii mbalimbali, ndivyo matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao yanavyozidi kupanuka. Mitandao ya Kijamii ya Kielektroniki imeweza kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili kwa sababu ujumbe huwafikia watu wengi kwa haraka sana.

2.1 Mtandao wa kijamii

Mtandao wa kijamii ni tovuti au programu inayokuruhusu kuungana na marafiki na familia, na kushiriki taarifa, picha na video. Kuna mitandao mingi ya kijamii kama vile: *Facebook*, *Wikipedia*, *Google+*, *Twita* na *LinkedIn*. Tovuti hizi ni baadhi ya mitandao mikubwa kabisa kwenye mtandao. Kuna zaidi ya watu bilioni moja kwenye Facebook, Wikipedia ina zaidi ya watumiaji bilioni nne na Twita ina zaidi ya watumiaji milioni 500. Mitandao ya kijamii mingi inakuruhusu kurekebisha mipangilio yako au kudhibiti maelezo yapi unayoshiriki, jinsi unavyoyashiriki, na unayeshiriki naye.

Utandawazi huweza kusaidia kuongeza msamiati wa lugha. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazopokea maneno kutokana na matumizi yake kwenye utandawazi hususan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, siasa, kijamii na uchumi. Kwa mfano, kuna matumizi ya istilahi nyingi za kimtandao za sayansi na teknolojia ambayo hutumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Hapo awali lugha ya Kiswahili haikupewa nafasi katika mitandao ya kijamii kwani ilionekana kama lugha isiyo ya kimtandao. Kwa hivyo, lugha kama vile Kiingereza zilipewa hadhi ya juu na hata kutumiwa katika shughuli mbalimbali za kimtandao. Matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii yalianza kuimarika mwaka wa 2007. Kiswahili hutumika katika mitandao ya Facebook na Twita kama nyenzo za mawasiliano. Kupitia mifumo mbalimbali mtandaoni kama vile mitandao ya kijamii, watumiaji wana uwezo wa kujenga maudhui, kuchapisha maelezo, kuwasiliana na kununua au kuuza bidhaa na kushiriki huduma mbalimbali. Katika sehemu nyingine za dunia, mitandao ya Kijamii inatumiwa kama vifaa vya kufundishia masomo mbalimbali. Hii ni kwa sababu walimu na wanafunzi wa lugha ikiwemo lugha ya Kiswahili hutumia mitandao hii katika shughuli zao za kiakademia.

Mitandao ya kijamii ina manufaa na madhara, na kwa hivyo unapoanza kuunda na kupakia maudhui mtandaoni, chukua muda kufikiri kuhusu unachoshiriki na madhara yake kwa watu wengine na hata kwa lugha ya Kiswahili. Unachokichapisha na maudhui unayopakia yatakuwakilisha mtandaoni. Hii pia inajulikana kama sifa ya tarakilishi. Ili kujiunga na mitandao yoyote ile, lazima utumie programu huria iliyo na msimbo chanzo ambao lugha huandikwa kwayo. Vivinjari vya mtandao kama vile, Chrome na Firefox ni mfano wa programu za

programu huria ambazo unaweza kugeuza kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kama vile:

- Wikipedia- kamusi huru
- Google- injini pekuzi ya Google
- Blog – blogu

Kupitia juhudi hizi za kimtandao umedhihirika kuwa lugha ya Kiswahili haijaachwa nyuma sana katika matumizi yake. Wataalamu mbalimbali wanafanya juhudi ili kuimarisha matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia.

2.2 Kitandazi cha Facebook

2.2.1 Historia Fupi ya Facebook

Facebook ni mtandao wa kijamii, ambao unatokana na jina la Kiingereza linalomaanisha kitabu. Mtandao huu ulianzishwa nchini Marekani kwa ajili ya wanafunzi ili kuwasaidia katika kuwasiliana na kutambuana. Ilianzishwa na Mark Zuckerberg ambaye kwa wakati huo alikuwa mwanafunzi wa saikolojia katika Chuo Kikuu cha Harvard. Ilizinduliwa Februari 2004 na kuitwa Facebook ambalo lilikuwa jina la karatasi iliyokuwa ikitumiwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza kujisajili. Facebook ilianzishwa kwa ajili ya wanafunzi wa chuo kikuu cha Harvard, lakini baadaye ilipanuka hadi vyuo vingine vya Boston, Ivy League, na Stanford. Hatua kwa hatua mtandao huu uliungwa mkono na wanafunzi kwa kuongeza usaidizi wao kabla ya kufunguliwa katika vyuo vikuu vingine, na hatimaye kufikia kila mmoja mwenye umri wa miaka 13 na zaidi. Facebook kwa sasa inaruhusu mtumiaji yeyote ambaye ametimiza miaka 13 ili kujisajili kama mtumiaji.

Hanson (2007) anasema kuwa wanafunzi 1200 wa shahada ya kwanza katika chuo kikuu cha Harvard katika muda wa masaa 24 walikuwa wamejisajili. Baada ya mwezi moja, nusu ya idadi ya watu walikuwa wamejiunga na Facebook na mnamo Agosti 2005 mtandao ulipewa jina la Facebook.com. Mtandao huu ulikuwa umeenea hadi katika taasisi za elimu na kila mtu aliyekuwa na anwani pepe alijisajili kufikia Septemba 2006. Kwa sasa, mtandao huu ni huru kujiunga nao kwani utahitajika tu kujaza fomu ambayo mtumiaji anaunda ukurusa wa kibinafsi. Ukurasa wa kibinafsi unakuwezesha kujiunga na marafiki, kuhariri na pia huonyesha maelezo ya kibinafsi.

Facebook kwa kawaida hutumiwa kuhifadhi mawasiliano yasiyo rasmi, kubadilishana picha na video. Watumiaji wa Facebook wanaweza kujiunga na matukio mbalimbali kama vile ya kiusomi, familia, burudani na ya kisayansi. Kupitia kwa mtandao huu unaweza kupata habari za hivi punde, kuuza bidhaa mbalimbali kupitia lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kupata habari za kisiasa, kielimu na kijamii kote ulimwenguni.

Tarehe 15 Juni mwaka wa 2009, Facebook ilizinduliwa kwa lugha ya Kiswahili na kuitwa '*Sura Kitabu*' na mradi huu umewawezesha watumiaji kutumia Kiswahili katika kurasa zao. Waanzilishi wa mradi huu wa '*Sura Kitabu*' wanasema kuwa walianzisha mradi huu kwa lengo la kuhifadhi, kukuza lugha na kuifanya kuwa maarafu miongoni mwa vijana ambao ni asilimia kubwa ya watumiaji katika jamii. Mradi huu vilevile ulianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wazungumzaji wa Kiswahili milioni 110 kote ulimwenguni. Facebook kama aina ya mtandao wa kijamii inaendelea kuwa maarufu sana katika nchi za Kiafrika na imesaidia wale ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili hasa vijana ambao ni wasomi.

Unaweza kutumia Facebook kupitia kwa simu ya mkono au tarakilishi. Matumizi ya simu si ghali sana yakilinganishwa na tarakilishi. Nchini Kenya, mtandao huu hutumiwa kusambaza picha na kujiunga na marafiki na hasa mliosoma pamoja. Lugha ambayo hutumiwa ni ya mkato na isiyo rasmi. Nchini Kenya lugha ambazo hutumiwa sana ni Kiingereza, Kiswahili, sheng na lugha za kwanza. Lugha za sheng na lugha za kwanza hutumiwa ili kuficha ujumbe. Wale ambao hawaelewi lugha za kwanza huchanganya au hutumia Kiswahili na Kiingereza.

Zaidi ya watu milioni nne wamejiunga na mtandao wa Facebook kwa sababu ya umaarufu wake katika mawasiliano. Asimilia kubwa ya wale wanotumia mtandao huu ni vijana wa kati ya umri wa miaka 18 na 34. Kati ya watumiaji hawa, asimilia 65% ni wanaume na 35% ni wanawake. Tangu kuzinduliwa kwa *Sura Kitabu*, Kiswahili kimekuzwa katika mtandao huu (Nekesa, 2010). Jambo hili limewawezesha watumiaji kutumia lugha ya Kiswahili katika kurasa zao. Sura Kitabu ilizinduliwa kwa lengo la kufanya lugha ya Kiswahili kuwa maarufu. Jambo hili limekidhi mahitaji ya wale ambao wangependa kujiunga na mtandao huu lakini hawana umilisi wa lugha ya Kiingereza. Pia ilizunduliwa kwa nia ya kuwafikia wazungumzaji wa Kiswahili zaidi ya milioni 110 kutoka mataifa mbalimbali.

2.2.2 Orodha ya Baadhi ya Misamiati inayotumika katika Kiswahili Facebook

Lugha ya Kiswahili ambayo inatumika katika mtandao wa Facebook ni ile inayotafsiriwa moja kwa moja kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Kwa mfano:

Jedwali (2.1)

English Facebook Page	Ukurasa wa Kiswahili Facebook
Add picture	Ongeza picha
Advert	Matangazo
Account settings	Mipangilio ya Akaunti
Activity log	Rekodi ya shughuli
About	Kuhusu
Applications	Vitumizi
Application	Program
Blockings	Zuia
Comment	Toa maoni
Community policy	Viwango vya jamii
Check in	Ingia
Change language	Badilisha lugha
Create page	Buni ukurasa
Data policy	Sera ya matumizi ya data
Edit	Hariri
Edit profile picture	Hariri picha ya wasifu
Email	Barua pepe
Events	Matukio
Family members	Wanafamilia
Favorites	Vipendavyo
Find friends	Tafuta marafiki
Followers	Wanaokufuatilia
Games	Michezo
General	Jumla
General account settings	Mipangilio muhimu ya akaunti

Gender	Jinsia
Home	Nyumbani
Help center	Kituo cha msaada
Help and settings	Usaidizi na Mpangilio
Information we receive and how it's used	Maelezo tunayapokea jinsi yanavyotumika
Logout	Ondoka
Like page	Penda ukurasa
Menu	Menyu
Most Recent	Ya hivi karibuni zaidi
More friends	Marafiki zaidi
Name	Jina
News feeds preferences	Mapendeleo ya Taarifa
Network	Mtandao
Notification	Taarifa
Notes	Vidokezo
Normal	Kawaida
Offers	Matoleo
Payment	Malipo
Password	Neno siri
Pokes	Midukuo
Political views	Maoni ya kisiasa
Post a profile picture	Sambaza picha
Post	Chapisha
Photos	Picha
profile	Umbo
Professional skills	Ujuzi wa kikazi
Privacy and shortcuts	Njia ya mkato za Faragha

Privacy	Faragha
Refresh	Zima gumzo
Relationship status	Uhusiano
Religious views	Mitazamo ya kidini
Report a problem	Repoti tatizo
Save changes	Hifadhi mabadiliko
Search	Tafuta
See more stories	Tazama Arifa zote
Security	Usalama
Support dashboard	Dasibodi ya usaidizi
Share	Sambaza
Status update	Sambazia hadharani
Statement of right and responsibilities	Taarifa ya Haki na majukumu
Terms and Policies	Masharti na Sera
Terms you agree to when you use Facebook	Masharti unayoyakubali wakati unapotumia Facebook
Text messages	Utumiaji wa ujumbe maandishi
Timeline and Taggings	Kalenda ya matukio na utambulishaji
Top	Rudi juu
Turn off chats	Onyesha upya
Username	Jina la mtumiaji
What's not allowed and how to report abuse	Yasiyoruhusiwa na jinsi ya kuripoti matumizi mabaya

Katika ukurasa wa Facebook, mashirika ambayo hutumia lugha ya Kiswahili hutumia mtandao huu kuhifadhi utafiti na kazi mbalimbali za Kiswahili ili kufikia umma na wapenzi wa Kiswahili kwa muda mfupi. Kwa mfano, mradi wa SwahiliHub ni Kitovu cha Kiswahili uliyoanzishwa

mwaka wa 2012 na ni mradi wa kampuni ya Nation Media Group unaoendeshwa na magazeti yake makuu ya Kiswahili *TAIFA LEO* la Kenya na *MWANANCHI* la Tanzania. Ni kitovu kikubwa sana cha Kiswahili kote ulimwenguni. Mtandao huu unawaunganisha wasemaji, wasomi, wapenzi wa Kiswahili, wakareketwa wa Kiswahili, walimu na wanafunzi na hata taasisi za Kiswahili katika tovuti ambayo ni Kitovu cha Kiswahili. Kwa hivyo, huwezesha watumiaji wa Kiswahili kusakura na kusoma ili kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

SWAHILIHUB

Kitovu cha Kiswahili

Mradi wa:




MWANANCHI
LIPESHENI

Lugha ya Kiswahili imetamba katika nyanja za teknolojia ya habari na mawasiliano. Kitandazi cha Facebook hutumiwa na mamilioni ya watu kuwasiliana. Wahusika huwa na akaunti za kibinafsi au akaunti za makundi. Mojawapo ya maeneo ambapo Kiswahili kinatumika sana kwenye Facebook ni katika makundi ya mijadala kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya

makundi haya yameibuka kutokana na vipindi maarufu redioni nchini Kenya, mathalani Bahari ya Lugha (Radio Citizen), na Nuru ya Lugha (Radio Maisha).

Washiriki huuliza maswali ambayo hujibiwa kwenye vipindi hivi, mengine hujibiwa na wanachama wa makundi hawa kwa mtindo wa mdahalo. Makundi mengine ni juhudi za watu binafsi, kama vile Umbuji na Ulimbwende wa Lugha ya Kiswahili, Michapo Uswahilini, Msasa wa Lugha na Fani Husika, Jamvi la Fasihi na mengineyo.

Pia kupitia kwa Nembo ya Facebook, shirika la utangazaji la BBC Swahili, ni shirika ambalo limekuza lugha ya Kiswahili. Ni idhaa na mtandao ambao huwawezesha watu kutoa maoni yao kupitia kwa lugha ya Kiswahili kwa hivyo lugha ya Kiswahili husikilizwa na kuendelezwa na wengi kupitia maswali na maoni katika lugha ya Kiswahili. Kuna vipindi mbalimbali ambavyo huwakilishwa kupitia lugha ya Kiswahili kwa mfano: vipindi vya redio na televisheni vyote hutumia lugha ya Kiswahili. Shirika la BBC limeendelea sana kwani hutumia Kiswahili katika kurasa zake za Facebook. Jambo hili limeliwezesha kusambaza Kiswahili kote ulimwenguni kwa sababu ni shirika la Kimataifa.



Sabahi Online Kiswahili ni mtandao uliunganishwa na mtandao wa Facebook ambao hutumiwa kuendeleza lugha ya Kiswahili katika pembe za Afrika. Vilevile wachapishaji mbalimbali

wanauza vitabu tofauti tofauti vya Kiswahili kupitia mtandao huu wa Facebook hivyo kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Pia magazeti kama vile Taifa Leo huwa na kurasa zao katika mtandao wa Facebook.

Kuna mashirika mbalimbali ambayo yanaendeleza lugha ya Kiswahili kupitia mtandao huu kama vile KBC na Citizen. Vyama mbalimbali kwa mfano, CHAKITA na CHAKIKE na taasisi kama TATAKI zimeweza kuunda kurasa zao katika lugha ya Kiswahili ili kuendeleza mijadala mbalimbali kuhusu lugha. Vilevile kuna vyama vya wanafunzi wa shule za upili, vyuo na vyuo vikuu ambavyo hushughulika na maswali mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi wanatuma maswali mbalimbali huku wapenzi wa lugha ya Kiswahili hujadili maswali hayo na kuwapa majibu mwafaka.

Kwa mfano, kuna kikundi kwa jina **Najivunia kukijua Kiswahili, lugha ya Mama** katika mtandao wa Facebook na washiriki wanatumia kikundi hiki kujifunza, kuuliza maswali na kupata majibu katika lugha ya Kiswahili. Kikundi hiki kina zaidi ya washiriki 1000 na hushughulikia maswala kuhusu lugha na fasihi. Kikundi hiki hulenga kujadili nafasi ya fasihi ya Kiswahili kwenye zama hizi mpya za mawasiliano ambapo teknolojia ya mitandao ya kijamii imefanywa kuwa jukwaa kubwa kabisa la mawasiliano ya kila siku. Vyombo vya kisasa vya kielektroniki vinatumika kama nyenzo za mawasiliano kwa lugha na fasihi ili kufikia hadhira kubwa zaidi.

2.3 Twita

2.3.1 Historia kuhusu Twita

Mtandao wa Twita ulianzishwa Machi 2006 na Jack Dorsey, Evan Williams, Biz Stone na Noah Glass na kuzinduliwa Julai 2006. Mtandao huu ulisambaa sana na ukawa maarufu ulimwenguni kote. Kufikia mwaka wa 2012, watumiaji walikuwa milioni 100 na mwaka huo waliweza kutuma “Tweets” zaidi ya milioni 30 kila siku. Mwaka wa 2013 mtandao huu ulikuwa umeimarika zaidi na kuwa kati ya mitandao 10 maarufu hadi ukaitwa ujumbe mfupi wa mtandao. Kufikia Desemba 2014 mtandao huu ulikuwa na washiriki zaidi ya milioni 500. Jambo ambalo limefanya mtandao huu kuwa maarufu zaidi ni kule kuanzishwa kwa mradi wa simu ambao ni rahisi kujisajili na pia gharama yake si ghali sana.

Katika sekta ya elimu, Twita inatumiwa kama njia ya mawasiliano na chombo cha kujielimisha hasa katika vyuo na vyuo vikuu. Vilevile inatumiwa kama mbinu ya kukuza maingiliano baina ya wanafunzi hasa kwenye mihadhara mikubwa. Utafiti uliofanywa kuhusu matumizi ya Twita ulibaini kuwa matumizi ya mtandao huu katika mihadhara ya vyuo vingi imesaidia wanafunzi kuwasiliana baina yao na wanaidara, imekuza masomo yasiyo rasmi na kuwezesha wanafunzi kujumuika katika kujibu maswali mbalimbali na kuimarisha matokeo yao.

Ni mtandao wa kijamii ambao huwawezesha watumiaji kutuma na kusoma ujumbe ulio mfupi wenye kiwango cha maneno 140. Watumiaji ambao wamejisajili kwa mtandao huu wanaweza kusoma na kutuma ujumbe mfupi unaoitwa ‘Tweets’ lakini wale ambao hawajisajili husoma ujumbe pekee bila kutuma. Watumiaji vilevile wanaweza kujiunga na mtandao wa Twita kupitia mfumo wa mtandao, ujumbe mfupi au program za simu.

Twita ni kama shajara ya mtandao na huwezesha mazungumzo ya pande mbili ambayo hufanya wazungumzaji kutoa maoni yao. Mbinu ya kutuma ujumbe mfupi ni njia ya kipekee ya kuweza kuwasiliana na watumiaji wengine (Tweeter.net, 2011). Nchini Kenya, zaidi ya watu milioni moja na nusu wamejiunga na mtandao huu. Wamejiunga na mtandao huu kwa sababu wanataka kufupisha ili kurahisisha mawasiliano.

Nchini Kenya mtandao huu hutumiwa katika sekta ya utangazaji, biashara, elimu na shughuli za mawasiliano ya kawaida. Kwa vile vifupisho hutumiwa sana katika mtandao huu, lugha ya Kiswahili imekuzwa kwa kiasi kidogo sana. Kwa mfano, kuna mashirika ya utangazaji wa habari kama vile televisheni na redio ambayo hutumia lugha ya Kiswahili katika mijadala yao.

Watumiaji wa Kiswahili wamezua mijadala mbalimbali iwe ya lugha au fasihi na wale ambao hushiriki hutumia 'tweets' kuwasilisha ujumbe wao. Kwa mfano, washiriki huweza kuuliza maswali wataalam wa Kiswahili na kupata majibu kupitia kwa kurasa za Twita. Kwa mfano, kuna kurasa katika mtandao wa Twita kama vile **Swahili @ useful Swahili** ambazo zimeanzishwa ili kukuza lugha ya Kiswahili. Kupitia kwa ukurasa huu, wasomi wa Kiswahili hutafsiri baadhi ya maneno ya Kiingereza hadi Kiswahili. Pia mtumiaji yeyote aliye na ugumu fulani katika kutafsiri neno, huomba usaidizi kutoka kwa wanaoelewa dhana hiyo ambao humtumia jibu kupitia 'tweets'.

Makampuni mbalimbali ya uchapishaji hutangaza aina ya vitabu vya Kiswahili walivyonavyo kupitia mtandao huu, jambo hili huwawezesha watumiaji kupata vitabu kwa haraka na hivyo

kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kurasa za Kiswahili ni kama vile @Swahili_Methali ambao hushughulika na aina za methali. Unachohitajika kufanya ni kufuata katika Twita.

2.4 Wikipedia

Wikipedia ni mtandao katika tovuti ambao hujumuisha makala ambayo hupatikana katika lugha mbalimbali, Kiswahili kikiwa miongoni mwazo. Mtu yeyote huweza kuhariri makala yanayowekwa katika tovuti hizi kila wakati kwa kuongeza na hata kuondoa mambo mengine. Wikipedia ya Kiswahili ni kamusi elezo huru inayoandikwa na watu wengi kwa pamoja. Tovuti yenyewe ina maana kuwa kila mmoja anaweza kubadili yaliyomo katika ukurasa kwa kubonyeza kitufe cha hariri. Unaweza hariri kila ukurasa ambao haujakingwa. Ilianzishwa Januari mwaka wa 2001 na mpaka sasa ina majarida ya Kiswahili zaidi ya milioni tatu. Kiswahili kimekuzwa na kuendelezwa kwa kiasi kikubwa katika mtandao huu.

Unaweza kuhariri makala yoyote, kutoa makosa ya lugha, kutohoa maneno na kuendeleza na kukuza makala kwa kuandika kwa ufupi au kwa urefu na hata kusanifisha ukurasa. Wikipedia kwa Kiswahili ni toleo la kamusi elezo katika lugha ya Kiswahili iliyoanzishwa mnamo tarehe 8 Machi na kufikia sasa kuna zaidi ya makala yapatayo 29,000 na yanayoendelea kuongezeka kila siku. Maendeleo haya yameifanya Wikipedia (kamusi huru) kuwa katika nafasi ya 91 kote duniani. Kuna makala ya fasihi, lugha, isimu jamii, isimu tarakilishi, vitabu vya hadithi, majarida na mengine mengi.

Katika Afrika na visiwa vyake Wikipedia ya Kiswahili ndiyo ya nne kwa idadi ya makala yote na ndiyo ya pili kati ya lugha za Niger Kongo kuvuka kiwango cha makala 1,000 na pia ni ya pili katika Afrika kuvuka kiasi cha makala 10,000. Mtandao wa Wikipedia si wa manufaa kwa lugha ya Kiswahili pekee bali kwa lugha zote; hii ni kwa sababu tafiti nyingi zinahifadhiwa na kurekodiwa pale ndani kwa hivyo kuepusha athari za kupotea kwa matini.

Kuingizwa Kiswahili katika mtandao wa Wikipedia ni hatua kubwa inayoonyesha kwamba, Kiswahili kinaendana na hali ya utandawazi ambapo watu wamekuwa wakipata taarifa ambazo zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Hufanya watu wengi hususan wanaojua Kiswahili kusoma makala mbalimbali katika mtandao na kupata habari kwa kina. Kuwepo kwa kamusi za lugha katika tovuti ambazo huwezesha watu kujifunza lugha kupitia njia ya mtandao hukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Mtandao huu wa Wikipedia husaidia kuhifadhi tafiti nyingi hivyo kuwarahisishia wasomi wa Kiswahili kazi ya kutafuta makala fulani.

Mradi huu umeleta manufaa kwa kiwango cha juu hususan katika kuikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili hasa kupitia kwa msamiati. Hii hutokana na sababu kuwa waandishi mbalimbali wanaoshiriki katika uandishi wa makala katika mtandao wa Wikipedia huweza kujadiliana kuhusu jinsi ya kupata tafsiri ya maneno tofauti kutoka lugha tofauti hadi lugha ya Kiswahili. Kutokana na sababu hiyo basi lugha ya Kiswahili imewezeshwa kupata maneno ambayo yanaweza kusanifishwa na kuwa msamiati rasmi unaokubalika katika lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla mitandao wa Facebook, Twita na Wikipedia imeweza kukuza na kuendeleza Kiswahili kwa kiasi hata kama vifupisho vinatumiwa sana. Matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii yamewawezesha wapenzi wa Kiswahili kuweza kusoma na kusikiliza habari na vipindi mbalimbali katika lugha ya Kiswahili hususan kutoka maeneo mengi ulimwenguni.

2.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia historia ya mitandao mitatu ya Facebook, Twita na Wikipedia na ilibainika kuwa Kiswahili kimehusishwa kwa kiasi kikubwa katika matumizi yake. Kiswahili hakijapitwa na mabadiliko ya teknolojia ya mitandao ya kijamii. Sura ya tatu itajadili maana ya lugha mtandao au Netspeak, sifa zake, mbinu ambazo zimetumiwa kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao mitatu, sababu za ufupishaji, sheria za ufupishaji na kuangalia utata unaozuka kutokana na ufupishaji.

SURA YA TATU

MBINU ZA KUFUPISHA MANENO YA KISWAHILI

3.0 Utangulizi

Baada ya kujadili mitandao ya Facebook, Twita na Wikipedia na historia na maendeleo ya Kiswahili katika mitandao ya mawasiliano, sura hii imejikita katika kufafanua mbinu zinazotumika kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Lengo la sura hii ni kujadili lugha mtandao au Netspeak, sifa zake kwa ujumla, mbinu zinazotumiwa na washiriki kufupisha maneno ya Kiswahili, sababu za kufupisha na utata unaozuka katika matumizi ya lugha mtandao (Netspeak). Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi itatuongoza katika kuchanganua matokeo ya utafiti huu.

Kama wasemavyo Wodak na Weyer (2001), Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU) huchunguza mahusiano angavu na yasiyo angavu yanayohusiana na nguvu, uwezo, itikadi na ubaguzi ambayo hudhihirika kupitia usemi. Usemi ni kule kujieleza kwa kutumia maneno na ni jina linalopewa maumbo yanayozidi sentensi moja. Usemi huweza kutumiwa kuimarisha nguvu na maarifa na pia kujikinga na kukosoa.

Van Dijk, (1993) anasema kuwa Uchanganuzi Tahakiki Usemi huweza kutumiwa katika uchanganuzi wa kiisimu, simiotiki na usemi na huchunguza dhana ya utawala ambayo huendelezwa na usemi. Hueleza vile usemi unavyoweza kutumiwa na kundi fulani kama vile wasomi, vijana au taasisi, ili kudhihirisha ubaguzi katika nyanja za kisiasa za kijamii, kitabaka, kirangi au kijinsia.

Vifupisho hutumiwa kuleta ubaguzi katika jamii kwa sababu watumiaji wanataka kuficha siri zao na kujiweka kwenye tabaka fulani. Ubaguzi huu huendelezwa kupitia kwa usemi na watu walio na uwezo wa kisiasa, kielimu na nafasi katika jamii. Nguvu za usemi hudhihirika wakati kundi lililo na uwezo linapomiliki lingine (Van Dijk, 2001). Vifupisho hutumika sana na vijana ambao ndio wengi katika jamii zetu, vifupisho vimebuniwa na hutumiwa sana katika kuokoa muda na husambazwa kutoka sehemu moja hadi nyingine na hivyo kurahisisha mawasiliano yao.

Fairclough na wengine (1999) wanasema kuwa, lugha ya kutoa habari haikosi mapendeleo kama vile vifupisho vinavyotumiwa na vijana walio wengi katika jamii kuficha ujumbe na kuzua mambo mapya katika jamii. Hii ni kwa sababu UTU huchukuliwa kuwa kiungo msingi cha uchanganuzi wa matini. Kumaanisha kuwa matini huwa katika uchanganuzi wa usemi na maswala mengine huzunguka usemi kama vile utoaji, upokezi, ufasiri na tendo. Nadharia hii imetufaa kwa sababu matini ya kimtandao itachunguzwa na UTU huchukulia matini kuwa maandishi au usemi, picha, filamu au tangazo na chochote kile kinachoweza kuchanganuliwa (Van Dijk, 2008).

Katika utafiti huu, matini yaliyochanganuliwa ni mawasiliano ya kimtandao ambayo hutumiwa sana katika mawasiliano ya kawaida. Lengo kuu ni kutathmini na kubainisha mbinu mbalimbali zinazotumiwa kufupisha maneno ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao. Kama wanavyosema MC Gregor na wengine (2003) kuwa UTU huweza kusaidia wasomi kufasiri ujumbe na maana ya maneno yaliyosemwa na kuandikwa. Maneno tunayoongea hupata tafsiri yake kutokana na misingi yetu ya kijamii, kisiasa na kihistoria kwa hivyo kupitia UTU, usemi

huchunguzwa ili kupata maana fiche. Vifupisho mbalimbali vya kimtandao hutumiwa ili kuficha ujumbe.

Katika mazungumzo yote ya wanajamii, maongezi ni mojawapo na hakuna usemi unaokamilisha uzalishaji na ufasili bila kuzingatia jinsi usemi huo unavyoathiriwa na maswala ya kijamii (Fairclough, 1989). Mazungumzo yanapotokea hudhihirisha hisia walizonazo wanajamii kuhusu kinachosemwa katika miktadha ya jamii hiyo. Kupitia kwa vifupisho vya kimtandao wanajamii wanawasiliana kwa kutumia ujuzi wa kiisimu na ule wa kimahusiano walio nao. Wazungumzaji na wapokezi wa ujumbe hutumia vifupisho ili kurahisisha maelewano baina yao. Sababu ni kwamba wanaotumia vifupisho lazima wawe na tajriba pana kuhusu dhana fulani ili mawasiliano yakamilike. Lakini neno fulani linapofasiriwa vibaya huweza kuleta utata wa kimawasiliano.

Mhimili wa fasili na fasiri ni jambo muhimu katika nadharia hii. Hii ni kwa sababu namna tunavyofasiri na kufasili vifupisho hutegemea muktadha na mahusiano ya kijamii. Mambo hayo mawili yanafaa katika kukamilisha maana ya kinachokusudiwa. Vifupisho vitabainika waziwazi kwa kuzingatia kinachosemwa na kinachokusudiwa kwa vile lugha ni kipengele cha utamaduni na huzua kinachokusudiwa kutokana na mpangilio wake (Dijk, 1983). Kwa hivyo matumizi ya lugha huathiri mtazamo na msimamo wa wanajamii na wanachofikiria. Kutokana na lugha hii ya kufupisha watumiaji wanaweza kuficha siri, kudhalilisha wenzao na kutaniana kutokana na maana zinavyojengeka akilini mwao.

Muundo wa usemi hutegemea vikwazo vya kijamii kama vile umri, tabaka na cheo. Mhimili huu pia umetuongoza kwa sababu usemi ni matini andishi yanayofaa kuwakilishwa kimatamshi na

huathiriwa na vikwazo vya kijamii kama vile tabaka, cheo umri na jinsia. Kwa hivyo kupitia kwa tabaka la vijana ambao ni wengi katika jamii inadhihirika kuwa vifupisho vinatumika kwa wingi. Vifupisho vinatumika sana kwa sababu ya kutaka kujiweka katika tabaka fulani na pia kwa ajili ya kuokoa muda na kupunguza gharama ya kutuma ujumbe. Kwa ujumla nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi huchukulia lugha kama tendo la kijamii na huchukulia vilevile muktadha wa usemi kuwa muhimu.

3.1 Maana ya Lugha Mtandao (Netspeak)

Lugha mtandao 'Netspeak' ilizuka ulimwenguni kote kutokana na maajilio na athari za mapinduzi ya kielektroniki kufuatia matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwa kutumia kompyuta katika jamii zetu. Katika lugha ya Kiswahili 'Netspeak' ni lugha mtandao. Ni lugha ambayo ni nyepesi kubadilika na yenye muundo unaowezesha mawasiliano kufanyika kwa haraka. Ilizuka kutokana na matumizi ya ujumbe mfupi katika simu (Werry, 1996). Lugha mtandao ni mbinu mpya ya kielektroniki ya mawasiliano ambayo imeibuka na hutumiwa kimataifa (Baron, 2001). Lugha hii imeenea zaidi hata kuliko teknolojia kuumanisha kuwa lugha mtandao ndio maarufu sana katika matumizi yake na kila uchao inabainika kuwa maneno mapya ya kimtandao yanazidi kuzuka na kuenea kotekote. Lugha mtandao imekuwa lingua franca ya kimtandao na hutumika sana katika mawasiliano. Imeweza kuathiri nyanja zote za maisha kama vile biashara, elimu, utangazaji wa habari na mawasiliano yasiyo rasmi. Pia ni mbinu mpya ya kielektroniki ya mawasiliano ambayo imeibuka na hutumiwa kimataifa (Crystal, 2006). Ni msamiati wa kimtandao na hujumuisha idadi kubwa ya matumizi ya maneno na virai. Lugha hii imezuka na hutumika sana katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine.

Kulingana na Hudson (2000), chanzo cha mabadiliko ya lugha mtandao ni kuonyesha maana mpya, wanajamii wanapobadilika hata maneno katika lugha hubadilika. Anaendelea kusema kuwa sifa za uwazi ndizo huwezesha watu kuunda maneno mapya katika lugha ili kuonyesha mambo mapya, matukio na mawazo mbalimbali.

Kulingana na Kinsella (2010) anaeleza kuwa hadi sasa, wataalamu mbalimbali wameshindwa kupata dhana mwafaka ya kufafanua lugha mtandao. Wengine hueleza lugha mtandao kuwa ni vishazi ambavyo vimefupishwa au ni maneno ambayo yamebadilishwa kifonetiki, kiishara au matumizi ya akronimu ili kutoa maana zaidi kwa watumiaji. Kwa hivyo lazima pawe na uelewa kati ya watumiaji wa lugha hii. Sababu hii ndio inayopelekea mtumiaji yeyote wa lugha mtandao awe na ufahamu wa ujumbe huo, maana yake na jinsi inavyotumiwa. Lazima awe na tajriba pana kuhusu lugha hii ili kukamilisha mawasiliano na ujumbe uliokusudiwa uweze kueleweka bila utata wowote.

Lugha mtandao vilevile siyo maneno ambayo yamefupishwa pekee bali pia vishazi vilivyoongezewa maneno. Hivi sasa lugha hii imelinganishwa na lahaja kwa sababu watu wanaoelewana kilahaja huitumia katika mawasiliano ya kawaida. Lahaja hii sana sana hutumiwa na vijana. Pia lugha mtandao au 'Netspeak' ni aina ya lugha ambayo hukua katika mazingira ya kielektroniki na huainishwa kama lugha isiyo rasmi. Kwa mujibu wa Crystal (2006) lugha mtandao ni aina ya lugha ya kielektroniki ambayo hutumika katika maongezi, maneno bayana, www, blogu na ujumbe mfupi katika simu. Anasema kuwa wale watumiaji wa lugha hii huitwa 'Netizen' kutoka kwa neno la Kiingereza 'Net' na 'Citizen'. Anaendelea kueleza kuwa lugha

mtandao ni sifa ngeni ambayo hujumuisha lugha ya mazungumzo, lugha andishi na sifa za kielektroniki.

Kulingana na Nekesa (2010) lugha mtandao huwa na sifa za usemi na uandishi na huathiri na hutegemea aina nne za lugha moja: lugha ya maandishi, kusoma, mazungumzo na kusikiza. Hii ni kwa sababu lugha hii iliundwa mwanzo kwenye umbo andishi ya lugha na imeathiri lugha kimazungumzo na kimaandishi katika maisha halisi. Kwa hivyo tofauti iliyopo baina ya lugha mtandao au 'Netspeak' na lugha mazungumzo katika maisha halisi ilizuka kabla lugha ya mtandao na imefanywa kama lugha mazungumzo. Mwingiliano huu huhusu mpangilio wa maneno katika sentensi, matumizi ya ufupishaji wa kitenzi au kuongeza viambishi tamati vya vitenzi kwa maneno asilia za Kiswahili.

Urban Dictionary wameeleza kuwa lugha mtandao ni namna ya kufupisha maneno na hali ya kubadilisha herufi moja ya neno na herufi nyingine au ishara kwa lengo la kuokoa muda, upigaji chapa kwa urahisi, kupunguza idadi ya maneno na kupunguza gharama ya kutuma ujumbe. Upigaji chapa kwa haraka husababisha makosa ya kimaandishi au kitahajia na makosa hayo hukubalika katika mawasiliano ya kimtandao. Makosa ya tahajia yamekuwa jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao na jambo hili limekuwa maarufu sana hadi kukaibuka lugha mpya iitwayo taipografia. Lugha hii huwawezesha watumiaji kutumiana matini fupifupi zenye mchanganyiko wa maneno nambari, hivyo kuibuka na lugha tofauti na inayozoeleka miongoni mwao.

Crystal (2001) anasema kuwa kuna utata na ni vigumu kueleza kwa ufasaha na kikamilifu maana ya lugha mtandao. Hata hivyo anasema kuwa itaendelea kukua na kuimarika na hivi karibuni itahusishwa na sifa zake zitafanywa kuwa kanuni na sheria za kimtandao na hata kufanywa kuwa miongoni mwa lugha ambazo zinatumiwa katika jamii zetu na hata kuundiwa kamusi.

Crystal (2008a; 2008b) katika makala yake, aliyoyaita *Texting* au ujumbe mfupi anasema kuwa umatinishaji ni jambo jipya kabisa ambalo sasa linaelekea kupata lugha yake. Anaelezea kuwa katika umatinishaji, lugha mpya aliyoiita *textspeak* inakuwa kwa haraka hasa miongoni mwa vijana.

Kwa maoni yangu lugha mtandao au 'Netspeak' ni aina ya lugha ya mkato ambayo imezuka na kukua katika mazingira ya kielektroniki na hutambulika kwa sifa zake za kimtandao kama vile matumizi ya akronimu, vifupisho, udondoshaji, uunganishaji na matumizi ya herufi na nambari. Ni lugha ambayo hutambuliwa na hutumiwa na kundi fulani la watu katika jamii na watumiaji hutumia sana ili kuficha siri au kwa matumizi ya tasfida. Tofauti uliopo kati ya lugha mtandao na sheng ni kuwa, lugha mtandao ni lugha andishi ambayo imezuka katika mazingira ya kielektroniki na hutumika ili kurahisisha mawasiliano. Sheng huwa ni lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha watu kujitambulisha na hususan huwa ni lugha ya mazungumzo.

3.2 Sifa Bainifu za Lugha Mtandao/ Netspeak kwa Ujumla

Lugha mtandao kwa ujumla una sifa mbalimbali ambazo zinadhihirika kupitia matumizi yake kwenye mawasiliano ya kimtandao. Sifa hizi hubainika katika lugha mbalimbali kama vile

Kiingereza, Kiswahili na lugha zingine. Jambo hili limeweza kuonyesha kuwa lugha mtandao ni lugha ambayo inaendelea kukua na ni kama lugha zingine ambazo imeshuhudiwa.

Kulingana na Varnhagen na Wengine (2009), mawasiliano ya kielektroniki hasa ya maandishi kama vile matumizi ya ujumbe mfupi, gumzo na maumbo mengine ya mawasiliano ya kielektroniki yana sifa sawa za kimtandao. Washiriki wa kimtandao wameunda lugha mpya ya mawasiliano ya ufupishaji, akronimu na uakifishaji. Njia mkato zinazotumika katika mawasiliano ya kimtandao na ambazo zimedhihirika kuwa sifa za lugha mtandao ni kama vile ufupishaji, matumizi ya akronimu, kuchanganya nambari na herufi, matumizi ya herufi kubwa katikati ya maneno, udondoshaji na matumizi ya tahajia za kipekee. Matumizi ya ishara za kipragmatiki kama vile ishara, maneno yanayodhihirisha hisia na matumizi ya viakifishaji vingi au kutovitumia ni njia za kipekee zinazotumiwa katika kuwasiliana kwenye mitandao ya kijamii. Sifa hizi za lugha mtandao ni kama zifuatazo.

3.2.1 Uunganishaji wa Maneno

Ni sifa ya lugha mtandao ambayo maneno mawili huunganishwa pamoja ili kuunda neno jipya. Hutumika sana katika mawasiliano ya kimtandao ili kuunda maneno mapya ambayo ni mafupi. Mtumiaji anaweza kuunganisha maneno mbalimbali kutoka lugha tofauti hasa za sheng, Kiswahili, Kiingereza na lugha za kwanza. Kwa kawaida katika lugha ya Kiswahili, uunganishaji husisha maumbo ambayo tayari yamo katika lugha husika, na kuzaa maneno ambatani. Mbinu hii kwa kawaida huchukua maneno mawili yenye maana ya kimsingi na kuyaambatanisha kuunda neno geni. Mbinu hii ni tofauti sana katika mawasiliano ya kimtandao kwa sababu watumiaji wanapotumia maneno ambayo yanaambatana na viakifishi, wao hudondosha viakifishi

na kuunganisha maneno mawili ambayo yangeandikwa tofauti ili kuhifadhi nafasi. Uunganishaji vilevile huweza kuhusisha silabi tamati ambao sehemu ya kwanza ya neno na ile ya pili ya neno tofauti huchukuliwa na kuunganishwa upya ili kuunda neno tofauti. Mifano:

Jedwali (3.1)

Uunganishaji	Maneno sahihi
Kwivo	Kwa hivyo
Kwkweli	Kwa kweli
Motomoto	Moto! Moto!
Sai	Saa hii

3.2.2 Matumizi ya Akronimu

Mbinu hii, maneno huundwa kwa kuunganisha vijisehemu vya maneno katika maelezo marefu ili kuunda neno jipya lenye dhana tofauti. Huhusisha kuunganisha herufi za mwanzo za maneno katika kirai ili kuunda neno jipya. Kulingana na Bauer (1983), akronimu ni mbinu ya kubuni maneno mapya kwa kutumia herufi za mwanzo. Naye Danica (2013) anasema kuwa, ni uundaji wa maneno mapya kwa kuunganisha herufi za mwanzo, katikati na mwisho ili kuunda kirai. Hutumika kwa sababu watumiaji wanataka kupunguza idadi ya maneno. Katika mawasiliano ya kimtandao huitwa ujumbe mfupi. Mifano

Jedwali (3.2)





Ufupishaji	Maneno kamili
Deree	Dereva
Mat	Matatu

3.2.3 Matumizi ya ishara (emoticons)

Ishara ni sifa moja ya lugha mtandao na mara nyingi huwakilishwa na picha za nyuso. Mawasiliano ya kimtandao kupitia maandishi hayana uwezo wa kuonyesha ishara za kimwili na sauti. Kwa hivyo, ili kufidia upungufu huu watumiaji wameweza kuibuka na njia za kutumia ishara ili kudhihirisha hisia mbalimbali za mwili kupitia kwa mawasiliano yasiyo ya mdomo. Ishara hizo hutumiwa ili kuonyesha hisia mbalimbali za uso, miondoko ya macho na ishara za mikono na kichwa. Ishara hizi hudokeza mielekeo na fikira za watumiaji (Danica 2013). Huhusisha pia matendo ambayo hueleza au hudhihirisha hisia na sauti au kuonyesha ishara za furaha, huzuni, idhini, kukataa na kushangaa (Mann & Stewart, 2000). Hii ni mbinu ya kuunganisha alama za viakifishi pamoja na nambari ambazo huwakilisha hisia kwa njia ya maandishi (Danica, 2013).

Kwa maoni yangu matumizi ya ishara ni hali ya kuunganisha alama za uakifishaji na tarakimu au nambari ili kuunda ishara za furaha, mshangao, chuki, hofu na wasiwasi kwa mfano,

Jedwali (3.3)

Ishara	Maana ya ishara
	Kuonyesha uso wenye machozi
	Uso usio na furaha
	Kuonyesha uso wenye mshangao
	Kuonyesha mzaha/ dhihaka



Uso wenye furaha

Katika taaluma ya isimu, ishara ni dhana ambayo hutokana na uunganishaji wa maandishi, alama za uakifishaji pamoja na nambari ili kuonyesha ishara. Huhusisha maneno mawili kutoka lugha ya Kiingereza: 'Emotion' - hisia na 'Icon' - taswira ambayo huweza kuelezwa kisemiotiki.

Chandler (1997) anasema kuwa semiotiki ni taaluma ya ishara na kulingana na Ferdinand de Saussure ishara hugawika katika sehemu mbili: umbo ishara na dhana ambayo ishara humaanisha. Kwa hivyo neno andishi huweza kutumiwa kama ishara. Ishara hutumiwa sana katika mawasiliano ya kimtandao kuonyesha uso wenye furaha, huzuni na utani. Kuna macho mawili katika ishara hiyo na mdomo. Watu wanaweza kufasiri matumizi ya taswira hizo za kimtandao tofauti kwa hivyo mtumiaji lazima awe anaelewa maana yake kwa vile ishara si taswira na inaweza kutafsiriwa vingine.

3.2.4 Matumizi ya Viakifishi vingi

Watumiaji wa lugha mtandao hawatumii viakifishi hasa wanapoandika ujumbe au wao waweza kutumia viakifishi vingi kuashiria jambo fulani. Viakifishi hubainisha namna waandishi wanavyosawazisha lugha andishi na lugha mazungumzo na wanazingatia viakifishi ili kuepuka utata na wengine hawazingatii kabisa ili kurahisisha upigaji taipu (Baron, 2010).

Mbali na viakifishi, idadi za ishara zimeongezeka sana na hii imechukua nafasi ya viakifishi.

Watumiaji wanachanganya alama za viakifishi, jambo hili si la kawaida kwa mfano, matumizi ya

kituo (...) au urudiaji wa alama (,,,). Urudiaji wa viakifishi huashiria msisitizo na hisia. Wengine hutumia alama za viakifishi moja kwa moja mwishoni mwa sentensi na mbinu hii hutumika sana katika mawasiliano yasiyo rasmi. Viakifishi zaidi ambavyo vinatumika sana katika mawasiliano ya kimtandao ni kama vile:

Jedwali (3.4)

Viakifishi	Alama
Kistari	---
Alama za kunukuu	“””””””””
Koloni
Ving'ong'o	”””””””””
Koma	”””””
Vishangao	!!!!!!!!!!!!
Viulizi	??????????????
Alama za dukuduku
Vituo

Matumizi ya herufi katikati mwa neno na maneno yenye hisia hutumiwa kubainisha au kueleza maana na pia hutumiwa kwenye matini ili kuepukana na matumizi ya maelezo marefu. Watumiaji vilevile wameibuka na mtindo wa kutumia herufi kubwa katikati mwa neno au katika sentensi nzima ili kusisitiza jambo fulani.

3.2.5 Udondoshaji

Massamba na wenzake (2009) wanaeleza udondoshaji kama utaratibu wa kutoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi. Udondoshaji wa maneno katika mawasiliano ya kimtandao ni maarufu sana. Hii ni kwa sababu kupitia kwa udondoshaji maneno yanafanywa

kuwa mafupi ili kuchukua nafasi ndogo. Utafiti huu umedhihirisha kuwa, kiwango kikubwa cha maneno ambayo hudondoshwa ni vitenzi ili kuepukana na urudiaji na sentensi ndefu ndefu.

Kimani Njogu na Wengine (2006) wanasema kuwa udondoshaji ni hali ya kipashio cha neno; irabu, konsonanti au silabi, kutoweka kabisa katika mazingira maalum. Katika lugha ya Kiswahili inaonekana kwamba aghalabu irabu inapodondoshwa huwa ni kwa sababu ya kutaka kuvunja mfululizo au mfuatano wa irabu au konsonanti katika neno ili kudhibiti muundo wa silabi. Lakini watumaji wa kimtandao wanadondosha tu ili kukidhi mahitaji yao. Wao hudondosha irabu ili kurahisisha matamshi na hivyo kuharakisha mazungumzo au mawasiliano yao kimaandishi.

Mfano (3.5)

Udondoshaji	Neno kamili
Ktb	Kitabu
Nn	Nani

3.2.6 Matumizi ya Nambari

Matumizi ya nambari pia hutumiwa sana katika mawasiliano ili kubadili maneno ambayo yanafanana kimatamshi au kukaribiana kisauti. Watumiaji wa kimtandao wameibuka na njia nyingine ya kudondosha fonimu/ sauti fulani katikati, mwanzoni au mwishoni mwa neno na nafasi yake kuchukuliwa na nambari. Wanatumia nambari ili kurahisisha upigaji chapa wa ujumbe, kuokoa muda na kupunguza gharama. Hii ni kwa sababu kwenye mawasiliano ya kimtandao, watumiaji hawataki kupoteza muda wowote kwa sababu mawasiliano ni ya moja kwa moja. Jambo jingine ambalo lilibainika ni kuwa, nambari hutumiwa kubadili maneno ambayo yanafanana kimatamshi au kukaribiana kisauti.

Mfano (3.6)

Neno na nambari	Neno kamili
Kwa 7bu	Kwa sababu
Kua3	Kuathiri

3.2.7 Matumizi ya Lugha isiyo Sahihi

Lugha inayotumika katika mawasiliano ya kimtandao ni lugha isiyo rasmi. Sababu kuu ikiwa watumiaji wanapuza kanuni na sheria ambazo zimeundwa ili kuongoza lugha yoyote ile. Matumizi ya lugha isiyo sahihi katika mawasiliano ya kimtandao hasa mitandao ya kijamii huongezeka kila uchao. Sababu inayopelekea kufanya hivyo ni kuwa, wanataka kuwasilisha ujumbe haraka iwezekanavyo na kujibiwa papo kwa hapo. Wanatumia lugha kiholela kwa minajili ya kutimiza haja yao ya kuwasilisha ujumbe wenye maana sio lugha. Hawazingatii mpangilio wa konsonani- vokali, sarufi na hijai. Katika taaluma ya kimofolojia kuna sheria ambazo zinafuatwa ili kuunda sentensi fulani lakini watumiaji wa kimtandao wanakaidi sheria hizo. Kwa kawaida wao huchukua nambari ambayo inafanana na fonimu moja kimatamshi. Kwa mfano

Jedwali (3.7)

Lugha isiyo sahihi	Maana kamili
Xaxa	Sasa
N4mb4ri	Nambari
Ckuji	Siji
N3na	Nena

3.2.8 Matumizi ya Maneno Machache Huru

Sifa ya kutumia maneno ambayo ni huru inadhihirika waziwazi katika mawasiliano ya kimtandao. Watumaji wanafupisha maneno bila kufuata kaida na sheria zinazoongoza kila lugha. Kwa mfano, ilibainika kuwa asimilia 90% ya maneno ambayo yameundwa katika mitandao ya kijamii ni yale ambayo hayafuati mpangilio wa konsonanti na vokali. Wao wanaweza kuunda neno ambalo lina mfuatano wa konsonanti mbili au zaidi au kudondosha vokali iliyo katikati ya konsonanti. Vilevile wanafupisha maneno kutokana na kuathiriana kisauti au kukaribiana na hata wanaweza kuchukua neno kutoka lugha moja ambalo linatamkika sawa na neno lingine kutoka lugha nyingine. Kwa mfano, maneno ya Kiingereza yanatoholewa na kufanywa yatamkike kama ya Kiswahili ili kutosheleza mahitaji ya watumiaji.

3.3 Mbinu Zinazotumika Kufupisha Maneno ya Kiswahili Mtandaoni

3.3.1 Ufupishaji: Dhana ya Ufupishaji

Lugha ya Kiswahili tayari ina maelezo ya dhana inayotaka kutumika lakini watumiaji wa mtandao wanapenda kufupisha ili kuipa dhana fulani jina fupi zaidi. Maneno yale ambayo huelezwa kwa dhana ndefu wao hufupishwa ili yatamkike kwa haraka na kuokoa muda. Ufupishaji ni hali ya kufanya dhana iliyo na maelezo marefu kuwa mafupi ili kueleweka na kusomeka kwa urahisi. Ufupishaji wa maneno umekuwepo katika lugha ya Kiswahili na umekuwa ukifunzwa katika viwango mbalimbali vya elimu. Pindi tu mitambo ya kielektroniki ilipozuka, hususan mitandao ya kijamii, kuna mabadiliko makuu katika lugha ambayo hutumika.

Kulingana na Ingo (2003), ufupishaji ni njia maarufu ya kuunda maneno na hufanana kwa kiasi fulani na uchanganyaji msimbo kwa vile zote mbili huwa ni muungano wa sehemu tofauti za maneno. Ufupishaji wa maneno katika mawasiliano ya kimtandao hauongozwi na sheria zozote.

Watumiaji wamezua mtindo/ mbinu mpya ambayo imeweza kurahisisha mawasiliano baina yao. Mbinu hii imeibuka hivi karibuni kwa sababu watumiaji wa kimtandao wanataka kufanya neno ndefu kuwa fupi ili kuwasilisha ujumbe haraka iwezekanavyo. Hii ni kwa sababu maneno marefu huchukua muda mrefu kutajwa na kuandikwa na watumiaji wa lugha na hivyo basi yanastahili kufupishwa. Ufupishaji huu huegemea utumiaji wa akronimu. Matumizi ya ufupishaji yameshuhudiwa na ni maarufu sana katika mawasiliano ya kimtandao ili kurahisisha mawasiliano ya kawaida. Mawasiliano ya kimtandao huwa ni mawasiliano ya kimuhtasari. Hatuna budi kwa hivyo kushuhudia matumizi ya mbinu mpya ya mawasiliano ambayo ni ufupishaji.

Mhimili wa viwango vya uchanganuzi, ulituongoza katika sura hii. Kwa sababu huchunguza uhusiano uliopo baina ya viwango vitatu vya uchanganuzi: matini yenyewe, michakato ya usemi inayohusu kubuni, kuandika, kuongea, kusoma na kusikiliza na jamii kwa ujumla ambayo hutumia michakato hii. Mchakato uliozingatiwa ulikuwa wa kusoma na kuandika vifupisho vya kimtandao hasa kwa kubainisha mbinu mbalimbali zilizotumiwa kubuni vifupisho hivyo na maana zake. Mhimili huu umetusaidia kuchunguza uhusiano uliopo kati ya vifupisho, michakato ya usemi na jamii kwa sababu vifupisho ni matini ambayo yamerekodiwa kupitia maandishi na huwakilisha matendo na imani zetu. Matini vilevile ni elementi ya matukio ya kijamii ambayo huleta mabadiliko ya kitajriba, imani, mielekeo na thamani. Kwa hivyo nadharia hii kwa ujumla imetusaidia kuchunguza namna vifupisho vinavyoundwa na kutumika katika jamii.

Lugha mtandao katika Kiswahili ina sifa zifuatazo: haizingatii kanuni ya konsonanti na vokali (KV), ufupishaji wa maneno hudhihirika, sarufi isiyo sahihi na matumizi ya tahajia isiyo sahihi.

'Netspeak' ya Kiswahili huzingatia muundo wa konsonanti, konsonanti na konsonanti (KKK). Hii ni kwa sababu wanaotumia lugha hii wanataka kusambaza ujumbe kwa haraka na pia kutumia maneno machache katika maandishi yao. Lugha ambayo hutumiwa sana katika mitandao ya Facebook, na Twita ni lugha ya mkato. Kuna aina mbalimbali za mbinu ambazo hutumiwa kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii kama vile:

3.3.2 Akronimu

Ni uundaji wa maneno kwa kutumia herufi za mwanzo za maneno au kuchanganya herufi za kwanza za maneno na kishazi (Bodomo, 2009). Akronimu ni aina ya ufupishaji au ni mojawapo ya kikundi cha ufupishaji. Ufupishaji huu huundwa kutokana na sehemu za kwanza za herufi ya kishazi au neno. Aghalabu huwa ni sehemu za maneno ambazo huwa ni herufi binafsi za maneno au kishazi au kipande cha neno au jina. Ni aina ya uundaji wa maneno ambayo huwekwa katika kategoria ya kuchanganya maneno. Kwa mfano:

Jedwali (3.8)

Akronimu	Maana kamili
Tkk	Toa kitu kidogo
Tlb	Toa lunch bwana

3.3.3 Ufinyaji

Kulingana na Bieswanger (2007), ufinyaji ni hali ya kuchanganya maneno mawili ambayo huleta idadi ndogo ya herufi za neno bila kutamka maneno yote mawili kwa pamoja. Ni hali ya

kupunguza idadi ya maneno kwa kuleta pamoja sehemu fulani za maneno. Pia ni kuacha sehemu fulani ya herufi au silabi na kuleta pamoja herufi za kwanza na za mwisho ili kuunda neno jipya.

Jedwali (3.9)

Ufinyaji	Maana kamili
Baadayez	Tuonane baadaye
Kila kitu's	Kila kitu sawa
Jamaaz	Jamaa wangu
Sukumaz	Sukuma wiki's

3.3.4 Ufupishaji Mkato

Watumiaji hulenga kufupisha neno, sentensi au kifungu cha sentensi ili mhusika aweze kutumia maneno mengi iwezekanavyo kwa kutumia nafasi ndogo yaani anafanya mawasiliano ‘marefu’ kwa kutumia maneno machache. Ufupishaji huu ni ule ambao haujakubalika na kufanywa rasmi katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu katika lugha ya Kiswahili kuna vifupisho vingine ambavyo vimekubalika na hata kuingizwa katika kamusi na hukubalika katika matumizi yake. Mara nyingi huhusu herufi ambazo huchukuliwa kutoka kwa kishazi au neno. Vilevile ufupishaji ni kuacha kifungu cha ndani au kuondoa sehemu ya neno kabisa. Kwa mujibu wa Ingo 2003 maana katika neno huweza kubadilika kutokana na muktadha na namna mtu fulani anafasiri dhana hiyo.

Vifupisho hutumika ili kutotamka au kutoandika maneno yote; wakati mwingine hutumiwa ili kuokoa muda, nafasi na hata kuficha siri na baadhi ya makundi ya watu katika jamii. Watumiaji wanaweza kuibuka na mitindo tofauti ya kuunda vifupisho vya kimtandao kwa mfano, wengine

huchukua herufi za mwanzo na mwisho ili kuunda maneno. Huwa na maana zaidi ya moja kutegemea muktadha kwa hivyo watumiaji wanapokezana ujumbe lazima wawe na tajriba ya kuweza kung'amua kwa undani neno fulani kutegemea muktadha. Kwa mfano:

Jedwali (3.10)

Udondoshaji	Maneno kamili
K.v	Kama vile
K.m	Kwa mfano
Bd	Bado
Uku	Huku
Fpi	Ufupi

Lakini ufupishaji wa kimtandao ni ule ambao hutumiwa sana na haujakubalika katika lugha ya Kiswahili na watumiaji hutumia kwa lengo la kuokoa muda na nafasi katika kutuma ujumbe mfupi kwa simu au katika mitandao ya Kijamii. Udondoshaji ni ufupishaji wa maneno kwa kuacha sehemu zingine.

Jedwali (3.11)

Lugha Mtandao	Maneno kamili
Swa	Kiswahili
Hosi	Hospitali
Mresh	Mrembo
Daro	Darasani

Katika mifano hii ni wazi kuwa sauti zingine zinadondoshwa na wakati mwingine watumiaji wanachukua silabi tatu au mbili za mwanzo ili kufanya neno hilo kuwa fupi. Kwa mfano, katika

neni *Swahili*, herufi za kwanza tatu ‘Swa’ huchukuliwa ili kuokoa muda na kuokoa nafasi na kuandika maneno machache kwa wakati mmoja.

Katika mbinu hii, neno hufupishwa kabisa na vifungu vichache hutumika. Wakati mwingine watumiaji wanaondoa irabu na pahali pake kuchukuliwa na konsonanti au vokali hudondoshwa na kubakiza konsonanti tu. Kwa hivyo, watumiaji hudondosha vokali pekee ili konsonanti isalie pekee. Ufupishaji huundwa kwa kuchukua herufi za mwanzo kutoka kwa mfuatano wa maneno mengi ili kuunda neno jipya. Huweza kuandikwa kwa kutumia aidha herufi ndogo au kubwa na huweza kutamkwa kwa kutaja herufi mojammoja.

Jedwali (3.12)

Lugha mtandao	Neno kamili
Zte	Zote
Msc	Msichana
K.m	Kama
Mch	Mchana
Kbs	Kabisa
Lkn	Lakini
Lzm	Lazima
Sbb	Sababu
Bb	Baba
Vp	Vipi
Ksh	Kesho
Lbd	Labda
Mtz	Matumizi

Ktk	Katika
Ktk	Kutoka
Mi	Mimi
Mzk	Muziki
Ktbu	Kitabu
Flani	Fulani
Jmb	Jambo
Bna	Bwana
Mko	Muko
Sa	Sasa

Aina nyingine ya ufupishaji ni pale ambapo watumiaji wanadondosha herufi moja au mbili. Mara nyingi vokali hudondoshwa kwenye kishazi ili kupunguza idadi ya maneno. Mara kwa mara watumiaji huwacha herufi au fonimu ambazo wanahisi kuwa hazina maana yoyote na neno huweza kuwasilishwa vyema bila kupoteza maana yake. Wanaamini kuwa fonimu hiyo itapoteza muda wao wanapoandika. Maneno ambayo huweka alama ya ufupishaji wanaipuuza na kukutanisha silabi ili kuunda neno moja.

Katika udondoshaji wa maneno vipengele muhimu kama vile viambishi vinavyodhihirisha njeo hudondoshwa na vipengele vya kileksimu kama vile nomino na kitenzi kuachwa. Udondoshaji wa irabu moja au mbili katikati mwa konsonanti hubainika katika vitenzi hasa vinavyodhihirisha njeo mbalimbali kama vile- me,-li,-tu, na -ta (Bodomo, 2009). Upunguzaji na udondoshaji wa silabi au fonimu ni jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao. Zoezi hili haliwezi kuathiri ufasiri na ulewaji wa ujumbe. Mifano:

Jedwali (3.13)

Udondoshaji wa vokali 'a'	Neno kamili
Ntaka kuamka	Nataka kuamka
Ankuja	Anakuja
Ntkunywa	Nitakunywa
Wancheza	Wanacheza
Aje	Niaje!
Unfnya kazi	Unafanya kazi
Sna	Sana
Haw	Hawa
Zko	Zako
Nja	Naja

Ni bayana kuwa katika lugha ya Kiswahili kuna vifupisho ambavyo vimekubalika na hutumika katika shughuli rasmi lakini ufupishaji wa kimtandao ni ule ambao haukubaliki kabisa katika lugha ya Kiswahili.

Jedwali (3.14)

Udondoshaji wa vokali 'e'	Kishazi kamili
Tumenda	Tumeenda
Amlia	Amelia
Wamcheza	Wamecheza
Nimshangaa	Nimeshangaa

Jedwali (3.15)

Udondoshaji wa vokali ‘I’	Kishazi kamili
Alnchukiza	Alinichukiza
Nlkunywa	Nilikunywa
Ntakuja	Nitakuja
Ntakosa	Nitakosa
Hvyo	Hivyo
Nlmshow	Nilimshow
Nko	Niko
Vle	Vile

Jedwali (3.16)

Lugha kimtandao	Kishazi kamili
Kua – kiyeyushi ‘w’	Kuwa
-enu	Yenu
Ndio – kiyeyushi – ‘y’ au ndo- ‘iy’	Ndiyo
-api	Wapi

Udondoshaji wa fonimu katika maneno ya Kiswahili ni jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao. Uchunguzi uliofanywa unathibithisha kuwa, watumiaji wengi wa mtandao wanadondosha sauti /h/. Sauti ya koo/ glota hudondoshwa katika maneno kwa kuwa sauti hiyo ni mwigo na maana huweza kuwakilishwa bila fonimu hiyo. Hivyo sauti/ fonimu ikitokea katika lugha ya Kiswahili kwenye mtandao huwa inadondoshwa ili kufanya neno kuwa fupi. Jambo lingine ambalo ni bayana ni kuwa sauti ‘h’ ya ukanushi haidondoshwi kwa vile ikidondoshwa

maana katika neno hubadilika kabisa. Kudondosha konsonanti au herufi ya kwanza katika neno kwa mfano:

Jedwali (3.17)

Udondoshaji wa konsonanti 'h'	Neno kamili
-Ivi	Hivi
-Iyo	Hiyo
-Apo	Hapo
-Aya	Haya
-Ilo	Hilo
-Ili	Hili
Anaitaji	Anahitaji
-Uko	Huko
-Izi	Hizi
-Aki	Haki

Mara nyingi maneno ambayo yanadondoshewa sauti/fonimu katika lugha ya Kiswahili ni vitenzi. Imebainika kuwa, katika vitenzi vya Kiswahili, vokali ambazo huja hasa katikati mwa konsonanti mbili huachwa au hudondoshwa, hii ni kwa sababu wanapodondosha vokali katikati mwa konsonanti ujumbe utawasilishwa na anayepokea ataelewa bila kutatizika au kupoteza maana zake. Mara nyingi watumiaji wanapodondosha kikwamizwa, wanafanya hivyo kwa sababu wanaamini kuwa katika ujumbe herufi ambazo wanadondosha hazitamkiki kwa hivyo maana katika neno huweza kukamilika na kueleweka bila kuwepo kwa herufi hizo.

3.3.5 Matumizi ya Nambari na Herufi/Maneno

Mutembei (2011) anasema kuwa, katika lugha mtandao yaani 'Netspeak' watu huwasiliana kwa kutumiana matini fupi fupi zenye mchanganyiko wa maneno na nambari, na hivyo kuunda lugha tofauti na iliyozoeleka katika jamii nyingine. Matumizi ya nambari katika neno au kishazi huwekwa katika sehemu mbalimbali za neno kwa mfano, watumiaji wanaweza kuweka mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa neno au katikati mwa neno ili kuchukua pahali pa silabi ambayo inatamkwa kama nambari. Matumizi ya nambari ni jambo maarufu sana katika mawasiliano ya mtandaoni hasa katika mitandao ya kijamii ya Facebook, Twita, 2Go, Geep na kadhalika. Hii ni kwa sababu hutumiwa sana kutokana na namna tunavyotamka au hutumiwa ili kuchukua nafasi ya tahajia fulani au kuchukua nafasi ya sauti fulani inayosikika sawa kimatamshi na neno fulani. Matumizi ya nambari na maneno au fonimu huchukua sura mbili: kudondosha maneno na kutumia nambari pekee au wanachukua nambari kutoka lugha nyingine hasa ya Kiingereza na kubadilisha na maneno ya Kiswahili.

Udondoshaji huu una sura mbili; sura moja ni kudondosha maneno na kutumia nambari pekee kama ilivyo katika maneno 'tu' na 'nane', maneno hayo yamedondoshwa na katika nafasi yake kuna nambari ambazo huchukua nafasi ndogo zaidi na hivyo kutoa nafasi kuandika ujumbe mrefu ukitumia nafasi finyu. Nambari hutumiwa badala ya neno fulani kwenye neno linalotamkika kama jingine. Matumizi ya nambari kwenye matini ni njia maarufu inayotumiwa kufupisha maneno ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao. Hii ni kwa sababu maneno mengi ya Kiswahili yana silabi zaidi ya tano kwa hivyo, ni njia mwafaka ya kuokoa muda na kuandika maneno mengi kwenye ukurasa mdogo. Watumiaji wanapounda vifupisho kwa kubadilisha maneno marefu na mahali pake kuchukuliwa na maneno yenye silabi chache au

nambari huwa wameafiki lengo lao. Silabi au nambari hutumiwa kuwakilisha maneno ambayo yana ukuruba wa karibu kimatamshi na neno lingine.

Matumizi ya nambari hudhihirika hasa pale ambapo mtumiaji anabadilisha nambari fulani na herufi ambayo hufanana au kukaribiana kimatamshi. Kwa mfano, nambari ambayo inafanana na neno kimatamshi inatumiwa ili kufanya neno hilo kutamkika kama inavyotakikana na kuwasilisha maana. Wahusika hutumia nambari kuwakilisha neno zima au sehemu ya neno ili kuunda neno jipya ambalo huwakilisha maana sawa na neno la kwanza. Sura ya pili ni ile ambapo wanachukua nambari kutoka lugha nyingine hasa ya Kiingereza na kubadilisha na maneno ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili ambayo yanatamkika kama ya Kiingereza hasa kama nambari fulani hutumiwa. Tazama mifano ifuatayo: matumizi ya nambari ya kwanza na maneno katika sentensi. Mtumiaji hudondosha maneno na nafasi yake kuchukuliwa na nambari kwa mfano:

3.3.5.1 Nambari 1

Kupitia kwa nambari ya kwanza watumiaji wanachukua sehemu ya neno ambalo linatamkwa hususan kutoka kwa lugha ya Kiingereza na kuifanya itamkike kama neno la Kiswahili.

Jedwali (3.18)

Lugha mtandao(nambari moja na maneno)	Maana fafanuzi
Si uninunulia kal	Si uninunulia kamoja
Tuko pal au 2ko pal	Tuko pamoja

Katika neno kamoja mzizi imedondoshwa na pahali pake kuchukuliwa na nambari moja.

3.3.5.2 Nambari 2

Jedwali (3.19)

Kuchanganya nambari ya pili na maneno	Maana fafanuzi/ sentensi kamili
2	Tu
Ki2	Kitu
2ko tu	Tuko tu
22 tu2	Tumbili tuwili
Ki2a	Kimbilia
2neza	Tunaweza
U2pate	Utupate
Ku2ma	Kutuma
Ma2si	Matusi

Katika mifano hapo juu, imedhihirika kuwa watumiaji wanabadilisha silabi 'tu' na kugeza kuwa nambari ya Kiingereza two. Mtumiaji anajua kuwa neno 'tu', hapo haliwezi kubadilishwa (kuambishwa) kuwa ni nambari (2) ambapo nambari ya pili (neni) linabadilishwa na kuwa ni nambari (2) ili kufanya neno kuwa fupi na hivyo kuwa na nafasi zaidi kwa kuandika maneno mengi. Suala muhimu kwao ni maana.

3.3.5.3 Nambari 3

Imetokana na namba ya Kiingereza *three* kumaanisha neno la Kiswahili 'thiri' Kama kawaida ya kaida za lugha mtandao. Ufupishaji wa namba, tafsiri na hata udondoshaji wa baadhi ya herufi ni jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao. Kwa mfano:

Jedwali (3.20)

Nambari 3 na maneno	Maana fafanuzi
Ma3	Matatu
Mwa3ka	Mwathirika
nilia3ka	Niliathirika
Ma3	Mathree

3.3.5.4 Nambari 4

Nambari nyingine ambayo hutumika katika mawasiliano ya kimtandao, ni 'nne' (4) ambapo pia tafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hutumika. Hii imeonekana kwa wingi katika mawasiliano kuhusu muziki wa kizazi kipyua. Katika kufupisha watumaji husema kuwa: *k4ka4ka* (kufokafoka) na hata katika tanakali za sauti neno *fofofo*. Herufi 'fo' za Kiswahili zimetamkwa kama nambari *four* ambayo inatoka lugha ya Kiingereza na kuandikwa 4. Kwa kufanya hivi, mtumiaji, ametumia nambari, ametafsiri, amechanganya lugha na kufupisha urefu wa neno kwa wakati mmoja.

Jedwali (3.21)

Namba 4	Maana fafanuzi
444	Mtoto alilala fofofo
Ku4ka4ka	Kufokafoka

3.3.5.5 Nambari 5

Nambari *tano* haibadiliki sana katika lugha mtandao. Watumiaji huitumia kama ilivyo katika Kiswahili. Jambo ambalo wanafanya ni kubadilisha tu na nambari ili kupunguza urefu wa neno.

Jedwali (3.22)

Nambari 5	Maana fafanuzi
Juma5	Jumatano
Naomba shilingi500	Shilingi mia tano
Mku5	Mkutano
Mfua5 wa maneno	Mfuatano
Mwamba5	Mwambatano

3.3.5.6 Nambari 6

Watumaji wanafupisha neno *sita* la Kiswahili kwa kubadilisha na nambari 6.

Jedwali (3.23)

Nambari Sita	Maana fafanuzi
6ki maneno yako	Sitaki maneno yako
Mama ali66	Mama alisitasita alipokuwa akizungumza
6 ha	Sitaha
Nili6 kabisa	Nilisita kabisa

3.3.5.7 Nambari 7

Wanadondosha neno *saba* na kubadili na nambari saba kama inavyotamkwa katika Kiswahili.

Jedwali (3.24)

Ufupishaji wa nambari saba	Maana fafanuzi
Kwa 7bu	Kwa sababu
7to	Sabato
Kundi la 77	Sabasaba
Moto uli7bisha hasara mno	Moto ulisababisha hasara mno
7hi	Sabahi

3.3.5.8 Nambari 8

Nambari *nane* ni nadra sana katika matumizi yake. Katika neno *tuonane* ndilo neno pekee ambalo linaweza kugeuzwa kuwa nambari, neno hili lina kategoria mbili za namba, moja likiwa tafsiri ya neno la Kiingereza *two* ambalo linatumika na nyingine ni neno *nane* linalobaki katika Kiswahili.

Jedwali (3.25)

Namba nane	Maana fafanuzi
2o8 kesho	Tuonane kesho

3.3.5.9 Nambari 10

Nambari nyingine ambayo hutumika katika mawasiliano ya kimtandao ni nambari *kumi*. Nambari hili ni nadra sana katika matumizi yake. Kwa hivyo, watumiaji huchukua *ten* kutoka katika lugha ya Kiingereza na kuifanya itamkike kama ya Kiswahili. Wao huchukua maneno ya Kiswahili ambayo huaanza kwa *ten-* na kugeuza kuwa nambari. Jambo hili huwafanya kufupisha maneno ya Kiswahili na kuyaandika kwa haraka. Kwa mfano:

Jedwali (3.26)

Namba kumi	Maana fafanuzi
10a	Tena
10geneza	Tengeneza
10da	Tenda
10ga	Tenga

3.3.5.10 Nambari kuchukua Nafasi ya Fonimu

Wakati mwingine watumiaji wanabadilisha fonimu na nambari. Kwa mfano, nambari '4', hubadilishwa na kuwa fonimu 'a', na fonimu 'e' kuwa nambari '3'. Mara nyingi jambo hili hutokea pale ambapo watumiaji wanatumia maneno yasiyo na maadili. Baron (2001) aliweka aina hizi za maneno kwenye kategoria ya lugha mtandao; anasema kuwa ni matumizi ya maneno yanayodhihirisha ukosefu wa adabu au ufidhuli. Mtumiaji anapotumia maneno hayo huwa anajaribu kuonyesha hisia zake iwe ni kukasirika au kutaniana. Mann na Steward (2000) wanaeleza kuwa, 'flaming' au maneno haya yasio na adabu hutumiwa katika mawasiliano ya kielektroniki hasa baina ya watumiaji kuonyesha ufidhuli.

Mfumo mpya maalum wa kiothografia umedhihirika katika mawasiliano ya kimtandao. Mfumo huu ni ule ambao hutumia nambari badala ya tahajia. Watumiaji wanachukua nambari ambayo inakaribiana na fonimu fulani kimaandishi. Kwa mfano:

- 6- b
- 1- i
- 5- s

- 4- A
- 3- e

Mbinu hii hutumika mara nyingi kuficha matumizi ya maneno machafu na yasiyo na adabu,

Jedwali (3.27)

Matumizi ya nambari 4 badala ya 'a'	Maana kamili
M4t4mshi	Matamshi
M4l4y4	Malaya
S4s4	Sasa
We ni M4t4ko	Wewe ni matak

Pia fonimu 's', watumiaji wakati mwingine huandika kama nambari 5 na fonimu 'e' kama 3. Hii ni kwa sababu kuandika nambari ni rahisi kuliko herufi na huficha ufidhuli katika ujumbe. Nambari 3 hutumiwa badala ya fonimu 'e' ili kufanya neno fulani kuwa lenye adabu. Pia hutumiwa kuonyesha ubunifu wa hali ya juu na kwa ajili ya kujifurahisha.

Jedwali (3.28)

Matumizi ya nambari 3 badala ya herufi 'e'	Maana fafanuzi
Sh3nzi	Shenzi
S3x	Sex

Matumizi ya '6' badala ya 'b'	Maana fafanuzi

Si alinyam6a	Si alinyamba
Matumizi ya '1'badala ya 'I'	Maana fafanuzi
M4v1 ya kuku wewe	Mavi ya kuku wewe

Kuchanganya nambari na fonimu kwa ujumla ni jambo ambalo linatumika sana. Jambo muhimu kwa watumiaji ni kupitisha ujumbe kwa haraka na kuandika maneno machache kwa wakati mmoja. Maneno ambayo hufikiriwa kuwa hayana adabu au ni machafu hugeuzwa kwa kutumia nambari badala ya fonimu ili kupunguza aibu na hata kutoathiri hisia za watumiaji wengine au mpokeaji wa ujumbe.

3.3.6 Kufanya neno kuwa Finyu

Kifonolojia maneno ya Kiswahili huwa yanafuata kanuni au mpangilio wa konsonanti na irabu, kwa hivyo watumiaji wanaweza kuandika maneno kulingana na sauti au jinsi sauti fulani zinavyokaribiana na kuathiriana kimatamshi au kubadilisha sauti moja na nyingine. Hivyo hutumia hijai zisizo sahihi na kuupuuza mpangilio wa kifonolojia. Wanafanya hivyo ili kupunguza urefu wa idadi ya maneno hivyo kuokoa muda. Kwa mfano, watumiaji huongeza silabi 'z' mwishoni mwa neno ili kufanya neno kuwa finyu.

Jedwali (3.29)

Kuongeza mwishoni mwa neno 'z'	Maana fafanuzi / kudhihirisha uwingi
Mamaz	Hurejelea akina mama
Mamboz	Salamu kwa watu wengi
Sukumaz	Kumaanisha tunakula sukuma wiki kila siku

Shidaz	Shida nyingi
Baadayez	Tuonane baadaye

3.3.7 Mfumo wa Kukopa Silabi kutoka Lugha Nyingine

3.3.7.1 Matumizi ya 'C' badala ya kikanushi 'si'

Sheria au kaida nyingine ambayo watumiaji wanatumia sana katika mitandao ya kijamii ni ile inayoruhusu matumizi ya 'sauti' kutoka lugha moja katika mfumo wa sauti ya lugha nyingine. Matumizi haya yanaweza kuambatana na nambari au bila nambari na bado yakaleta maana. Lugha ya Kiswahili haina sauti ya 'C' kama inavyotamkika katika Kiingereza. Uchanganyaji huu, unaivuta sauti hii ili itamkike katika Kiswahili kama 'si' ili kuleta maana. Wakati mwingine herufi 'C' hutumiwa kwa niaba ya kikanushi 'Si' yaani kisarufi mofimu ya ukanushi 'SP' huandikwa kwa kutumia herufi 'C' ili kupunguza urefu wa maneno kwa mfano:

Jedwali (3.30)

Herufi c badala ya si	Maneno kamili
Cna sahani	Sina sahani
Cji	Siji
C ujipange tuondoke	Si ujipange tuondoke
Cjui	Sijui
Kiac	Kiasi
Kiema	Kisima
Co	Sio

Ucngizi	Usingizi
---------	----------

Vilevile matumizi mengine ya herufi ‘C’ badala ya ‘SI’ hubainika pale ambapo watumiaji huitumia kuwakilisha kikanushi au kuonyesha tendo fulani au kauli ya kuuliza swali. Kwa mfano:

Jedwali (3.31)

C [si] [zi]	Maana fafanuzi
C ujipange 2mlipe kesho	Si ujipange tumlipe kesho?
C twende ama?	Si twende ama?
C twende 2gnice	Si twende tujifurahishe
C nge ku sms	Si nge kuandikia arafa
Cnaweza	Sininaweza
Ucnmmalize	Usinimalize

3.3.7.2 Matumizi ya herufi ‘G’ badala ya ‘ji’

Washiriki wa kimitandao wakati mwingine wanapofupisha, wanachukua herufi ya Kiingereza **G** na kuitumia kwa niaba ya silabi ya Kiswahili **Ji**. Wanaivuta herufi **G** ya Kiingereza na kufanya itamkike kama ya Kiswahili. Watakuwa wamefupisha neno kwa sababu silabi ya Kiswahili ina herufi mbili na wanapotumia ya Kiingereza huwa tu ni silabi moja. Hivyo watakuwa wametimiza haja yao ya kufanya neno fulani kuwa fupi. Mifano:

Jedwali (3.32)

Matumizi ya herufi 'G' badala ya 'ji'	Maneno kamili
G- tetee	Jitetee
Nagvuna kuwa mkenya	Najivuna kuwa mkenya
G- na	Jina
G -G letu au G-ji	Jiji letu
G-bu ni	Jibu ni?
Nimeumia G-cho	Nimeumia jicho
G-fungulie akaunti	Jifungulie akaunti

3.3.7.3 Matumizi ya herufi 'Q' badala ya (kiu)

Wakati mwingine watumiaji katika mitandao ya kijamii wanapowasiliana wanabadilisha neno **KIU** na herufi **Q** hasa katika Kiswahili. Hii ni kwa sababu kimatamshi sauti hizo zinafanana na kukaribiana. Hata hivyo herufi **Q** haipatikani katika konsonanti za Kiswahili lakini washiriki wa lugha hii wameibuka na kuweka kwenye matumizi katika mawasiliano yao. Wanafanya sauti **Q** ya Kiingereza itamkike kama ya Kiswahili. Wanapotumia herufi **Q** pekee ambayo ni silabi moja watakuwa wametimiza mahitaji yao ya kupunguza neno la Kiswahili **KIU** ambalo lina silabi mbili. Lazima mtumiaji asome silabi **Q** kama inavyotamkika katika Kingereza ili maana ya neno ikamilike. Kwa mfano:

Jedwali (3.33)

Herufi Q badala ya (kiu)	Maana fafanuzi
Mtoto ana Q	Mtoto anakiu

Yule binti amebeba Q no	Yule binti ana ki uno kikubwa
Lahaja yetu ni ya Q nguja	Lahaja yetu ya Ki unguja
Q nzi	Ki nzi
Silabi ni q ngo cha neno	Silabi ni ki ungo cha neno
Riwaya ya Q	Riwaya ya Ki u

3.3.7.4 Matumizi ya herufi 'x' badala ya 's'

Mara nyingi watumiaji wanaweza kutumia sauti ambayo inaathiriana na nyingine kimatamshi.

Kwa mfano:

Jedwali (3.34)

Matumizi ya herufi 'x' au 'z' badala ya 's'	Neno kamili
Xaxa	Sasa
Xawa	Sawa
Xaa hii	Saa hii
Waxee	Wazee
Xambaza	Sambaza
Xema	Sema

3.3.8 Kuchanganya Ndimi/Msimbo

Kuchanganya msimbo ni mbinu ambayo hutumiwa na asimilia kubwa ya watu. Hii ni njia moja kuu ambayo ni maarufu katika mitandao ya kijamii. Mbinu hii hubainika waziwazi katika kategoria ya ufupishaji. Msimbo ni utaratibu wa mawasiliano unaohusu uteuzi wa msamiati na

maumbo ya sentensi. Utaratibu huu unajumuisha namna mbalimbali za kuwasilisha ujumbe na maana. Msimbo huwasilisha ujumbe na maana katika miktadha na kaida zilizokubalika na watu wenye ujuzi wa matumizi yake (Mc Mahon 1994). Katika kuwasilisha ujumbe na maana, washiriki huchanganya msimbo kuambatana na tajriba zao.

Kuchanganya msimbo ni uchopekaji wa kiungo cha lugha moja kwa moja kwa lugha nyingine. Kiungo kinachoambatishwa huweza kuwa neno, kauli au sentensi. Katika hali hii, matini yanayodhihirisha mwambatano wa lugha mbili au zaidi (Wamitila 2003). Ushahidi ambao unajitokeza katika mawasiliano ya kimtandao iliyoshughulikwa ni kuwa, mbinu hii ya kuchanganya msimbo inahusu matumizi ya uwili lugha ambapo lugha mbili zinatumiwa katika hadhi sawa na hutumiwa pale ambapo washiriki wanataka kufinya neno fulani ili kuokoa muda, nafasi na gharama ya kutuma ujumbe.

Msimbo ni mifumo wa ishara zinazotumiwa katika mawasiliano. Watu huchanganya msimbo kwa mfano, Kiingereza na Kiswahili kwa nia ya kuwatenga wazungumzaji wengine ama kuwahusisha watu zaidi kwenye mazungumzo. Pia watumiaji wa kimtandao hutumia lugha hizi ili kuonyesha hisia zao kwa wapokezi ambazo huweza kuwa za kirafiki, mzaha, kuchukiza, kukejeli na kadhalika. Kuchanganya msimbo hutumiwa sana na watu wa umri fulani hasa vijana kujitambulisha na pia kusesitiza jambo fulani.

Kuchanganya msimbo kumeelezwa na Richard na wengine (1985) kama uchopekaji wa maneno au sehemu ya neno ya lugha moja katika usemi wa lugha nyingine. Maoni haya yanaoana na yale ya Pfaff (1979) aliyesema kuwa, kuchanganya msimbo ni dhana inayojumuisha kubadilisha

msimbo. Anatambulisha aina tatu za kuchanganya msimbo ambazo ni: uambishaji wa kiungo, uchopekaji wa maneno ya kigeni katika sentensi na uchopekaji kati ya sentensi na nyingine. Appel na Muysken (1987) wanasema kuwa kuchanganya msimbo hutumiwa na wazungumzaji ili kutimiza aina zifuatazo za uamilifu: kurejelea, kueleza, kujitambulisha, kupendeza, kuokoa muda na kuonyesha hisia. Kuchanganya msimbo katika mawasiliano ya kimtandao hutumia maneno kutoka lugha ya Kiingereza na Kiswahili, Kiswahili mara nyingi hutangulia Kiingereza. Matumizi ya maneno ya Kiingereza hata hivyo, yamezidi matumizi ya lugha zingine kwa kiasi kikubwa.

Kulingana na King'ei (2010), kuchanganya msimbo ni kuingiza maneno yasiyo ya Kiswahili katika sentensi ya Kiswahili. Hali hii hutokea pale ambapo mzungumzaji huamua kuwa na misimbo au 'ndimi' zaidi ya moja katika usemi mmoja. Anaendelea kusema kuwa, mazingira ya uchanganyaji msimbo yanaweza kuhusisha lahaja za lugha moja.

Kwa mujibu wa Muysken (2001), uchanganyaji msimbo ni hali zote ambapo kipengele kimoja cha kileksika na sehemu ya kisarufi kutoka lugha mbili tofauti huchanganywa pamoja au hutokea kwa pamoja katika sentensi moja. Kuchanganya msimbo hutokea katika mazingira ya mazungumzo hasa pale ambapo watu wenye umilisi wa zaidi ya lugha moja wanapobadili msimbo kutoka lugha moja kwenda nyingine kwa mujibu wa taratibu za mabadiliko katika lugha. Naye Hymes (1974) anaelezea uchanganyaji msimbo kuwa ni matumizi ya lugha mbili au zaidi zinazogusa sentensi zaidi ya moja, au hata mitindo tofauti ya lugha. Bokamba (1989) anaeleza kuchanganya msimbo kuwa ni kuchanganya maneno, makundi ya maneno au sentensi kutoka katika mifumo miwili tofauti ya kisarufi na kwa kuvuka mipaka ya sentensi katika lugha.

Mbinu hii hutumika sana katika mawasiliano ya kimtandao, kama inavyobainika wakati watumiaji wanachanganya lugha tofauti ili kupunguza idadi ya maneno, kuokoa muda au kuandika maneno mengi kwenye nafasi ndogo. Mara nyingi wanapochanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili, wanafupisha kwa kuanza na fonimu za Kiswahili zikifuatwa na Kiingereza. Kuchanganya msimbo ni maarufu sana miongoni mwa vijana katika matumizi yake kwenye mitandao ya kijamii. Hii ni kwa sababu wanaochanganya msimbo wanataka kurahisisha upigaji chapa wa ujumbe kwa hivyo wanabadili maneno marefu sana kutoka kwa lugha ya Kiswahili na nafasi zake kuchukuliwa na maneno ya Kiingereza. Wengi wao huamini kuwa maneno kutoka lugha ya Kiingereza huwa na silabi funge na fupi kuliko za Kiswahili. Jambo hili la kuchanganya msimbo limekidhi mahitaji yao ya kuokoa muda na gharama ya kutuma ujumbe. Kuna mbinu mbili ambazo hutumiwa sana hasa katika kuchanganya msimbo:

- Kuchanganya nambari na maneno
- Kuchanganya silabi au maneno ya lugha mbili

3.3.8.1 Kuchanganya Nambari na Maneno

Mtumiaji anachanganya nambari katika Kiingereza na kufanya kuwa za Kiswahili kwa mfano, namba mbili (2) inaitwa *two*, ambayo inatamkika 'tu' kwa matamshi ya Kiswahili. Nambari ya Kiswahili 'nane' (8) haibadiliki kimatamshi, na hivyo inaambatanishwa katika herufi 'o' ya Kiswahili ili kufanya neno liwe 'tuonane' - 2o8. Mifano zaid ni:

Jedwali (3.35)

Kuchanganya msimbo	Maana fafanuzi
--------------------	----------------

Tulimwona 2kimo	Tulimwona mbilikimo
Ni2mie	Nitumie
2li3a	Tulitatua shida
Kikundi cha 77	Kundi cha sabasaba
2o8	Tuonane
22	Tumbili

Neno lingine ambalo linatokea lakini kwa nadra ni la nambari *moja* ambalo watumiaji wanachukua neno la Kiingereza *one* na kuliweka katika nambari ya Kiswahili kimatamshi yaani '*wani*' kwa mfano neno kuwania- 1a

Jedwali (3.36)

Nambari 1	Maana fafanuzi
Tuna1a	Tunawania
1dia alikuwa anacheza	Wandia alikuwa anacheza
Ji1	Jione

Kuchanganya msimbo hasa wa maneno na nambari ni kama udondoshaji; hii ni kwa sababu ukubwa na urefu wa maneno unapungua na hivyo kufanya nafasi kuwa kubwa zaidi, ili kuweza kuandika maandishi mengi zaidi hivyo basi kuokoa muda na kupunguza gharama.

3.3.8.2 Kuchanganya Sauti au Maneno kutoka Lugha Mbili

Mtumiaji anachanganya lugha mbili yaani Kiingereza na Kiswahili na nambari ili kufupisha maneno. Watumiaji wanapochanganya au kubadili kutoka lugha moja hadi nyingine wanataka kuunda sentensi ambayo ni fupi ili kuokoa muda, nafasi na kuandika maneno mengi kwa muda mfupi. Mfuatano wa maneno waweza kuwa wa sauti za Kiingereza, nambari za Kiswahili na maneno ya Kiswahili (Kiingereza + nambari + Kiswahili). Kwa mfano:

Jedwali (3.37)

Kiswahili/ Kiingereza na nambari	Maana kamili
Ctaenda au 6enda	Sitaenda
Nakuci	Nakusihi
Nac	Naona
2kaswim/ tukaswim	Tukaogelea
2	Tu/mbili
Tulichat/2lichat	Tulizungumza
Ctugo /C2go	Si twende
TuliZbuy	Tulizinunua
Kila kitu C mine	Kila kitu is changu
Amedecide	Ameamua
Kukupay	Kukulipa

Kwa kawaida, hakuna sauti **C** katika lugha ya Kiswahili kama inavyotamkwa kwa Kiingereza.

Kwa hivyo watumiaji wanaivuta sauti ya Kiingereza ili itamkike kama **SI** ya Kiswahili ili kuleta maana inayokusudiwa. Kwa mfano:

Jedwali (3.38)

Ctakucheki	Sitakuona
Ctakam	Sitakuja
C u kam?	Si u come/ si uje

Matukio ya kuchanganya msimbo miongoni mwa sentensi au neno ndiyo yanayotumika kwa kiasi kikubwa katika mawasiliano ya kimtandao. Berk-seligson (1986) anasema kuwa kuchanganya msimbo huku ikihusishwa na lugha moja ambayo haijaoeleka au kuwa inatawaliwa na nyingine. Hali nchini Kenya ni kuwa, lugha ya Kiingereza inaonekana kama inayoitawala ile ya Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha rasmi. Vilevile ndiyo inayotumika katika shughuli nyingi za kiserikali, kufundishia, utoaji wa hotuba na katika shughuli za bunge. Kwa sababu hiyo, Kiingereza hutumiwa sana na washiriki wa kimtandao ili kujitambulisha nayo. Kuchanganya msimbo ni jambo la kawaida (Habwe, 1999, Romaine 1989). Misimbo ambayo huchanganywa mara nyingi katika mawasiliano ya kimtandao ni Kiswahili na Kiingereza ingawa wakati mwingine watu huchanganya msimbo wakitumia lugha zao za kwanza na sheng.

Jedwali (3.39)

Kuchanganya sheng	Maana kamili ya maneno
Nitakushow	Nitakwambia
Kam	Kuja
Unaduu?/ unado?	Unafanya?
Nitatry	Nitajaribu
Unaniboo	Unaniudhi

Amego	Ameenda
Nimemada	Nimemaliza
Amededi / amedie	Amekufa
Kurelax	Kutulia

3.4 Utata Unaozuka katika Matumizi ya Lugha Mtandao

Wakati mwingine watumiaji wanakumbwa na utata fulani hasa wanapowasiliana kwa vile vifupisho vinaweza kuwa na maana zaidi ya moja kwa mfano:

Maneno kama vile:

Jedwali (3.40)

Maneno yenye Utata	Maneno kamili
Bb	Bibi
Bb	Baba
Ktk	Katika
Ktk	Kutoka
Mch	Mchana
Mch	Msichana

Matumizi ya nambari wakati mwingine huleta utata kwa wapokezi kwa sababu hawafahamu kama wataisoma nambari kwa Kiswahili au Kiingereza. kwa mfano, nambari 2 itatamkwa kama tu au mbili. Tazama mifano hii:

Mfano (3.41)

2kimo- **mbilikimo** ama **tukimo**

Jil- **jione** ama **jimoja**

Kulingana na sheria za ufupishaji matumizi ya nambari mbili haikubaliki. Mtumiaji anastahili kutumia tu nambari moja na neno. Utata ni kuwa ni nambari ipi itatumika, ya kwanza au ya pili?

Kwa mfano:

Mfano (3.42)

Tumbili (22)- **2mbili** ama **tu2**

Sabasaba (77) - **7saba** ama **saba7**

Kusitasita (ku66)- **sita6** ama **6sit**

3.5 Sababu za Kufupisha

Kuna sababu kadha wa kadha ambazo zimefanya watumiaji wa kimtandao kufupisha maneno katika mawasiliano ya kila siku. Zifuatazo ni baadhi ya sababu hizo:

3.5.1 Kuokoa muda na kuhifadhi kawi

Jambo ambalo linafanya watumiaji kufupisha maneno hasa ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao ni kuokoa muda. Hii ni kwa sababu baadhi ya maneno ya Kiswahili yana silabi zaidi ya mbili kwa hivyo wanapofupisha wanaokoa muda; vilevile wanaamini kuwa maneno ya Kiswahili ni marefu sana kwa hivyo wanatafuta istilahi toshelevu ambazo wanaweza kuandika

kwa urahisi. Mawasiliano ya mtandaoni huwa ya moja kwa moja kwa hivyo watumiaji wanastahili kujibu ujumbe huo kwa muda mfupi iwezekanavyo. Wakati mwingine kupiga chapa ujumbe mrefu huchosha kwa hivyo watumiaji wanafupisha ili kuhifadhi kawi. Kwa mfano unapopiga chapa neno:

Mfano (3. 43)

- **Mtz** ni rahisi kuliko kuandika sehemu yoye ya neno **matumizi**
- **Flani** badala ya neno **fulani**
- **Nn** badala ya **nini**
- **Zimb** badala ya neno **Zimbabwe**

3.5.2 Kutumia Idadi Ndogo ya Maneno

Jambo jingine ambalo linawafanya kufupisha maneno ni kutaka kuwasilisha ujumbe mwingi kwa nafasi ndogo. Kwa hivyo wanafinyanga maneno fulani ili kuwasilisha dhana ndefu kwa kutumia maneno machache. Wanapotumia maneno mengi huchukua muda mrefu na nafasi kubwa kuandika. Kwa mfano:

Mfano (3.44)

- Swa- Kiswahili
- Daro – darasani
- Mch- mchana
- Uji – huji

3.5.3 Kupunguza Gharama ya kutuma Ujumbe

Haja muhimu ya kufupisha maneno katika mawasiliano ya kimtandao ni kupunguza gharama ya kutuma ujumbe. Hii ni kwa sababu unapotumia vifupisho kuandika ujumbe unatumia idadi

kubwa ya maneno katika nafasi ndogo na kwa hivyo kupunguza gharama ya kutuma ujumbe. Gharama ya kutuma ujumbe ni ghali sana kwa hivyo watumiaji wanafanya kila wawezalo ili kuipunguza.

3.5.4 Kuwa Mbunifu

Hii ni hali ambayo mhusika anavumbua maneno mapya na kisha kuyapa maana fulani. Wale ambao wanatumia vifupisho wanaweza kuimarisha matumizi yao katika lugha. Hii ni kwa sababu mara nyingi wanazipanga zile fonimu za lugha kulingana wa ujenzi wa maneno ya lugha husika ili kuunda neno ambalo halipo katika lugha hiyo.

3.5.5 Upigaji chapa kwa haraka

Matumizi ya vifupisho huwawezesha watumiaji kuwasiliana kwa haraka. Hii ni kwa sababu ni rahisi na haraka kupiga chapa au kuandika neno ambalo limefupishwa kuliko kuandika kishazi kizima. Kwa mfano, KTK badala ya katika au kutumia akronimu *swa* au *hosi* kuliko kuandika neno kamili *Kiswahili* au *Hospitali*. Kwa hivyo vifupisho vimewawezesha watu kuwasiliana kwa njia ya kipekee na kutuma ujumbe kwa haraka.

3.6 Sheria za Lugha Mtandao katika Mawasiliano

Lugha mtandao au Netspeak ina sheria au kaida zake ambazo hazina budi kufuatwa ili kuleta maana tarajiwa. Ni sheria kama hizi ambazo zinamlazimisha mtumiaji kuzifuata ili kukubaliana na utumiaji huu. Wataalamu wengine wanadai kuwa lugha mtandao hujitokeza kiholelaholela na ni lugha ambayo haina maana na inalenga kuharibu lugha rasmi. Madai haya hayana msingi kwani lugha mtandao ina kaida zake (Mutembei, 2011).

Sheria hizi zimewekwa kwa lengo la kuwalinda watumiaji wasipite mipaka na kufupisha maneno kiholela. Kama vile lugha ya Kiswahili ilivyo na sheria za kuongoza katika uundaji wa msamiati, ndivyo ilivyo katika vifupisho vya kimtandao. Watumiaji wanastahili kufuata sheria hizo kwa njia ya kipekee. Kwa mfano:

3.6.1 Sheria ya Konsonanti Konsonanti (KK)

Ni bayana kuwa wahusika wengi wanapofupisha maneno ya Kiswahili wanazingatia sheria ya konsonanti konsonanti na hakuna mtumiaji ambaye amekiuka sheria hiyo. Kwa mfano:

Mfano (3.45)

Neno katika- ktk- KK na hakuna mtumiaji ambaye ameandika neno hilo kuwa kta

Au

Matumizi- mtz-KK- siyo mtzi

Matamshi- mts- KK- siyo mtsh

Kutoka- ktk- KK- siyo kta

3.6.2 Sheria ya Kubadilisha Konsonanti

Kwa mfano, kuwa asimilia kubwa ya watumiaji wanabadilisha konsonanti **x** na **s**.

Mfano (3.46)

sasa –xaxa

Sambaza- xambaza

3.6.3 Kudondosha Vokali Katikati mwa Konsonanti mbili

Watumiaji wengi wanadondosha vokali ambayo huja katikati mwa konsonanti mbili, hii ni kwa sababu ya kaida kuwa vokali hiyo haina maana yoyote na ujumbe huweza kukamilika bila kuwepo kwa neno hilo. Kwa mfano:

Mfano (3.47)

Anakuja- ankuja

Tulienda- tlienda

Amelia-amlia

Anitaji- anahitaji

3.6.4 Kukubali Mfumo wa Sauti kutoka Lugha nyingine

Sheria au kaida nyingine ni ile inayokubali matumizi ya 'sauti' kutoka lugha moja katika mfumo wa sauti ya lugha nyingine. Matumizi haya yanaweza kuambatana na nambari au bila nambari na bado yakaleta maana. Kwa mfano, matumizi ya sauti **G** badala ya **JI** au **C** ambayo inatamkika **SI**, na kuunda sentensi ya ukanushi inayojitokeza katika uchanganyaji msimbo na watumiaji wengi wanapofupisha hufuata sheria hii. Kwa mfano:

G-tete- jitete

C- si

3.6.5 Nambari Mbili kutokea kwa Pamoja

Sheria nyingine ambayo hudhihirika katika lugha ya mtandao ni kuwa, iwapo patatokea nambari mbili katika sentensi moja zinazofuatana au maneno mawili yanayofuatana na yote yanaweza kubadilishwa kuwa nambari, neno moja kati ya maneno hayo lazima libadilike kuwa nambari na

jingine libaki kuwa neno. Kwa mfano, neno *tumbili* lina nambari mbili na linaweza kuandikwa kama 22 lakini sheria inasema kuwa neno moja liwe nambari na jingine liwe neno kwa hivyo watumiaji wanachagua lile ambalo linachukuwa nafsi ndogo zaidi na kuwacha nafasi kubwa ya maneno zaidi katika mawasiliano. Maneno yote mawili yana uwezo wa kubadilishwa kuwa nambari lakini watumiaji wana uhuru wa kuchagua neno gani watafanya kuwa nambari na nyingine kubaki kuwa neno. Kwa mfano:

Mfano (3.48)

Tumbili- 2 kutoka kwa neno la Kiingereza two- 2mbili

Au

Tumbili- tu2

Tulisita-tu6

Au

2sita

Kwa ujumla, sifa hizi za lugha mtandao zimedhihirisha kuwa kuna aina tofauti za mbinu za lugha mtandao zinazotumiwa na wahusika katika mawasiliano ya kimtandao. Utafiti huu umebainisha kuwa, kupitia sifa za lugha mtandao watumiaji ndio wanaochagua mbinu ambazo wangependa kutumia katika mawasiliano yao. Ni dhahiri kuwa watumiaji wa lugha ya kimtandao huunda mbinu zao za kipekee kwa ajili ya mawasiliano. Kwa hivyo, watumiaji hao wana uwezo wa kuunda mbinu hizo za kimawasiliano kwa hiari yao. Kutokana na sababu hizi ni dhahirisho tosha kuwa utamaduni wa kimtandao ni wa jamii ambayo watumiaji wana uhuru katika mawasiliano.

3.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia mbinu mbalimbali ambazo zimetumika na watumiaji kufupisha maneno katika mitandao ya kijamii, sifa za lugha mtandao (Netspeak), sababu na utata unaojitokeza. Uchunguzi imedhihirisha kuwa vifupisho vinatumika kwa kiwango kikubwa na vijana. Mifano kadha wa kadha ya vifupisho iliorodheshwa kupitia kwa majedwali. Sura ya nne imeshughulikia athari mbalimbali ambazo hutokana na matumizi ya vifupisho vya kimtandao.

SURA YA NNE

ATHARI ZA VIFUPISHO AU LUGHA MTANDAO KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

4.0 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuangazia athari mbalimbali zinazosababishwa na vifupisho katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na kuongezeka na kuimarika kwa matumizi ya vifupisho hivyo, tumeshuhudia kuwa lugha mtandao imeweza kuathiri viwango vyote vya maisha hususan kitengo cha isimu kama vile mofolojia, fonolojia, sintaksia na hata semantiki. Lugha mtandao kwa ujumla imezua athari chanya na hasi kwa lugha ya Kiswahili na hata lugha zingine. Hii ni kwa sababu wanaotumia lugha hii hawazingatii sheria au taratibu zozote ambazo zinatawala lugha. Katika kubaini athari hizi, vigezo vya kifonolojia vilituongoza. Vigezo hivi ni silabi na mpangilio wa konsonanti- vokali. Kwa ujumla athari hasi ni nyingi kuliko athari chanya kama inavyoonyeshwa katika sehemu zifuatazo.

4.1 Athari hasi zinazotokana na Lugha Mtandao

Matumizi ya vifupisho katika mitandao ya kijamii yamezua athari mbalimbali katika lugha ya Kiswahili kote ulimwenguni. Sio lugha ya Kiswahili pekee ambayo imeathiriwa na lugha mtandao bali hata lugha zingine kama Kiingereza. Utafiti huu umeweza kudhihirisha waziwazi kuwa, kuna athari hasi na chanya zinazotokana na lugha tandawazi hasa kwa mustakabali wa lugha ya Kiswahili. Ni kweli kwamba kuenea kwa programu kama vile simu na tarakilishi ambazo watu wanaweza kujisajili na mitandao ya kijamii kumezidisha matumizi ya Kiswahili na kurahisisha mawasiliano. Aidha ni kweli kuwa, matumizi hayo yanakuza Kiswahili lakini lugha inayotumika ni lugha tandawazi au 'Netspeak' ambayo ina athari kubwa katika lugha ya Kiswahili. Athari ilibainishwa kwa kutumia vigezo vya kifonolojia vya Silabi, konsonanti - vokali na mofolojia.

Mofolojia huchunguza maneno ya lugha fulani na aina za maneno, hasa upande wa upangaji wa mofimu mbalimbali zitumikazo kwa ajili ya kuunda maneno. Maneno ni matokeo ya muungano wa fonimu mbalimbali ambazo pia huungana na kuunda silabi na hatimaye neno. Yaani, Fonimu ---> Silabi ---> Neno. Katika lugha ya kimtandao, watumiaji huunda maneno bila kuzingatia kanuni za kimofolojia. Mara nyingi watumiaji wanaweza kuchukua silabi au sauti kutoka lugha ya Kiingereza au sheng na kuifanya kuwa ya Kiswahili. Kwa mfano, sauti /x/ ya Kiingereza na /s/ ya Kiswahili kubadilishana nafasi kwa sababu sauti hizo hukaribiana kimatamshi.

Udondoshaji ni kanuni inayohusu kuachwa kwa sauti fulani katika matamshi au uandishi na hudhihirika sana katika mawasiliano ya kimtandao. Jambo hili limeweza kuathiri lugha ya Kiswahili kwa sababu katika sheria za Kiswahili, mofimu mbili zinapokaribiana katika mazingira sawa moja hudondoshwa. Jambo hili ni kinyume katika udondoshaji wa kimtandao. Imebainika kuwa watumiaji wanapotumia vitenzi wanaacha irabu ambayo inatokea katikati mwa konsonanti mbili kwani wao huamini kuwa sentensi huweza kukamilika bila kuwepo kwa sauti hii. Hili ni jambo ambalo linatia wasiwasi kwa vile hudidimiza ukuaji wa lugha hii. Kwa mfano:

- Tlkunywa- irabu mbili 'u' na 'I' zimedondoshwa- **Tulikunywa**
- Amlia- irabu 'e'- **Amelia**
- Atenda- irabu 'a'- **ataenda**
- Wncheza – 'a'- **wanacheza**

Udondoshaji huzua athari kwa kuvunja mfululizo wa konsonanti au irabu.

Ubadilishaji wa fonimu ni mbinu ambayo sauti isiyopatikana katika mfumo wa lugha fulani inabadilishwa na sauti nyingine au sauti inayokaribiana nayo. Hili linatokea katika maneno mengi ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha mtandao. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha ubadilishaji wa fonimu zifuatazo:

i. Kutumia /z/ x/ badala ya /s/

Utafiti huu umeonyesha ya kwamba fonimu /x/ inachukuwa nafasi ya fonimu /s/ katika jumbe nyingi za Kiswahili hususan wanapoandika maneno ya Kiswahili katika mawasiliano ya kimtandao. Matokeo hayo yanaweza kuelezwa kutokana na dhana kuwa, lugha ya Kiswahili haina fonimu (x). Lakini watumiaji wa kimtandao hubadili sauti /s/ na pahali pake kuchukuliwa na /x/. Hivyo basi sauti /z/ inapotokea nafasi yake inachukuliwa na /s/ na kuleta athari katika Kiswahili. Maneno yafuatayo yalithibitisha hali hii:

- Xaxa badala ya sasa
- Xai badala ya saa hii
- Xw badala ya sawa
- Xambaza badala ya sambaza

ii Kutumia / G/ badala ya /ji/

Watumiaji wengi wa kimtandao wanapoandika ujumbe wanahamisha silabi kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Jambo hili hutendwa kwa vile wao huamini kuwa silabi za Kiingereza ni fupi kuliko za Kiswahili. Kutokana na sababu hii inabainika kuwa lugha ya Kiswahili inapewa hadhi ya chini ikilinganishwa na ya Kiingereza ambayo hupewa hadhi ya juu. Kwa kawaida lugha moja inapopendelewa huwa inazua athari kwa lugha ambayo inadunishwa kwa sababu inazuia ukuaji na maendeleo yake. Mfano:

- G-one- jione
- kuGenjoy- kujienjoy
- G-cho- jicho
- Gwe- jiwe
- G-tete- jitete

iii Kutumia /Q/ badala ya /kiu/

Mabadiliko ya sauti yana nafasi kubwa katika lugha ya Kiswahili. Viambishi awali na viambishi tamati huathiriwa na sheria za mabadiliko ya sauti. Sheria hizo huathiri irabu na konsonanti. Sheria hizi za mabadiliko ni pamoja na ufupishaji na udondoshaji. Kudondoa sauti fulani kutoka kwenye neno ni jambo la kawaida katika mawasiliano ya kimtandao. Sauti ya Q haipatikani katika lugha ya Kiswahili na watumiaji wanapokopa kutoka kwa lugha ya Kiingereza hudhihirisha kuwa Kiswahili hakijitoshelezi katika mahitaji yake hivyo kuathiri maendeleo yake.

Mifano:

- Qno- kiuno
- Q- kiu
- Qnzi- kiunzi

iv Kutumia /c/ badala ya /si/

Matumizi ya silabi C badala ya 'si' ni njia maarufu inayotumika katika mwasiliano ya kimtandao. Jambo hili huhatarisha lugha ya Kiswahili kutokana na sababu ya kuwa neno kutoka lugha ya Kiingereza hukopwa na kufanywa litamkike kama la Kiswahili. Kwa kawaida mfumo wa sauti za Kiswahili unaruhusu tu konsonanti za aina fulani kufuatana kwa idadi na kwa

mpangilio maalum katika silabi. Yaani sauti zinafuata utaratibu maalum katika uundaji wa maneno. Kutokana na lugha ya mtandao inadhirihika kuwa hakuna mfumo maalum ambayo hufuatwa na watumaji hivyo jambo hili imeathiri umilisi wa lugha na kanuni ambazo zinatawala matumizi ya lugha. Kwa mfano:

- Co- sio
- Cji- siji
- Ctwende- sitwende
- Ctaki- sitaki
- Uengizi- usingizi

Lugha mtandao imeathiri sintaksia ambayo ni taaluma ya isimu inayojihusisha na uchunguzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Sintaksia vilevile huchunguza sheria au kanuni zinazofuatwa katika kuyapanga maneno ili yalete maana kubalifu na inayoeleweka katika lugha husika ili kukamilisha mawasiliano. Lugha ya mtandao hubuniwa tu bila kuongozwa na kanuni au sheria za Kiswahili. Maneno mengi ambayo hutumika katika mawasiliano ya kimtandao hayaleti maana kwa wasiofahamu lugha hiyo. Kwa mfano;

- M4t4ko- Matako
- M4v1- Mavi
- W3w3-Wewe
- M4l4y4- Malaya
- Ktk- Katika
- Nn- Nini

Matumizi ya lugha mtandao au 'Netspeak' katika lugha ya Kiswahili yamekiuka sheria na kanuni za kuunda sentensi kama vile matumizi ya viakifishi na uandishi wa maneno katika herufi kubwa. Hii ni kwa sababu watumiaji hawajali tena sheria za Kiswahili kwa mfano mpangilio wa konsonanti- vokali (KV) bali wao wanapofupisha hutumia konsonanti pekee. Kama vile:

Mfano (4.1)

- Katika- ktk ambao ni KKK
- Muziki- mzk- ambao ni KKK
- Labda- lbd- ambao ni KKK
- Vipi- vp- ambao ni KTK
- Nini- nn ambao ni KTK

Wanapoanza sentensi hawatumii herufi kubwa kama ilivyo sheria katika lugha ya Kiswahili hasa unapotua au kuanza sentensi lazima uanze na herufi kubwa. Wao wanaweza kuanza kwa herufi ndogo na katikati herufi kubwa. Sababu hii imepelekea watumiaji kuathirika sana hadi kukosa kufahamu mahali pa kutumia viakifishi.

Lugha mtandao vile vile imepotosha lugha ya Kiswahili, hata wengine wameita lingua franka ya mtandao, hii ni kwa sababu kwanza vifupisho huzalishwa tu ovyoovyo bila kuzingatia sheria za kuzalisha msamiati au kuunda sentensi. Hali hii imeathiri sana lugha ya Kiswahili na kuirudisha nyuma. Asimilia kubwa ya watumiaji wa vifupisho ni vijana ambao wanadidimiza lugha ya Kiswahili badala ya kuikuza ilhali wao ndio viongozi wa kesho. Kwa hivyo kufikia miaka ijayo,

huenda ikawa lugha ya Kiswahili haitakuwa ikitumiwa kabisa kwa vile vifupisho vitakuwa vinatumika kwa wingi na vitakuwa vimechukua nafasi yake.

Lugha mtandao kwa ujumla imeathiri namna watu wanavyotumia lugha hasa lugha maandishi. Sababu hii hupelekea watu ambao wamezoea kufupisha sana hadi wameathirika na hivyo hawawezi kutofautisha matumizi yake kwenye lugha rasmi na isiyo rasmi. Mara nyingi wanafunzi wanapoandika insha, kwa mfano, baadhi yao wanachanganya vifupisho visivyo rasmi na rasmi. Athari nyingine ni kuwa, sio vijana pekee ambao wameathirika na lugha hii ya mtandao bali jamii yote kwa ujumla hasa mazungumzo ya kila siku katika vyombo vya habari.

Athari nyingine hutokana na hali ya kufupisha vitenzi katika vishazi vya Kiswahili. Watumiaji wanapodondosha herufi au silabi fulani katika neno maana huweza kupotea, hivyo kuathiri lugha na matamshi. Maana inapopotea watu waweza kufasiri ujumbe kwa njia isiyofaa na hata kuibuka na istilahi potovu. Teknoiojia hii ya mtandao imebadili maumbo ambayo tunatumia hasa tunapotumia ufupishaji na akronimu. Kwa mfano

Mfano (4.2)

- Swahili- swa
- Vipi- vp
- Zote-zte
- Katika- ktk

Manufaa yake kwa watumiaji ni kuokoa muda katika kuandika ujumbe lakini matumizi ya mbinu hizi za ufupishaji hudunisha lugha ya Kiswahili kwa kutozingatia tahajia sahihi.

Lugha hii vilevile imeathiri namna watu wanavyotumia lugha katika mawasiliano kwa mfano, katika lugha maandishi watumiaji huunganisha maneno pamoja ili kuokoa muda na kuhifadhi nafasi. Hii imeathiri mpangilio na muundo wa maneno. Kwa hivyo athari za kifonolojia na kimofolojia inabainishwa.

Nekesa (2010) anasema kuwa kifonolojia, maneno ya Kiswahili yanastahili kutamkwa au kuandikwa kwa kuzingatia kanuni na sheria ya konsonanti na vokali (KV). Kuna aina tano za vokali katika Kiswahili: [a], [e], [i],[o] na[u]. Watumiaji wengi wanapofupisha au kuandika maneno kimtandao hawafuati sifa za konsonanti na vokali, wao huandika konsonanti mbili zikifuatana ua konsonanti peke au vokali pekee. Wanaunda na kuandika maneno kulingana na jinsi yanavyokaribiana au kuhusiana kisauti. Wakati mwingine wanaacha silabi fulani katika neno kwa sababu wao wanaamini kuwa maana ya neno huweza kuwakilishwa bila kuwepo kwa fonimú fulani. Jambo muhimu kwao ni kuwakilisha ujumbe wenye maana hata kama watapuza sheria fulani. Mifano:

Mfano (4.3)

- Ktk badala ya katika
- Mresh badala ya mrembo
- Hosi badala ya hospitali
- Jmb badala ya Jambo
- Deree- dereva

- Mcto badala ya mzito

Kama wasemavyo Massamba na wenzake (2009) fonolojia huchambua mfumo wa sauti katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, vitamkwa au sauti za lugha huungana ili kujenga maneno yanayokubalika katika lugha. Kupitia kwa vifupisho vya kimtandao sauti mbalimbali zinazotumika hazina maana yoyote, angalia mfano (4.3). Watumiaji kwa hivyo huunganisha vitamkwa ili kujenga maneno yasiyokubalika katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu vifupisho vingi havifuati mpangilio sahihi wa vitamkwa.

Lugha hii ya mtandao huhusu matumizi ya sarufi isiyo sahihi, makosa ya tahajia na uakifishaji ambayo ni kinyume katika lugha ya Kiswahili. Matumizi ya tahajia, sarufi sahihi na uakifishaji ni jambo muhimu katika lugha ya Kiswahili. Watumiaji wanapotumia viakifishi vingi mahali ambapo havitakikani au kutotumia viakifishi kabisa huvunja sheria za lugha hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili. Lengo kuu la watumiaji ni idadi ya maneno, kuokoa muda na kuandika maneno mengi kwa wakati mmoja na kutuma ujumbe kwa haraka. Kwa mfano:

Mfano (4.4)

- Unaenda???????????????
- KimBILIA
- anaENDa
- Niaje kujifeel hivyo???!!!
- Haiya!!!

Jambo jingine ambalo limefanya watumiaji kuhamisha vifupisho kutoka lugha moja hadi lugha ya Kiswahili ni kuandika ujumbe kwa haraka na shinikizo la kujibu ujumbe huo kwa haraka iwezekanavyo. Wanapohamisha lugha mtandao hadi Kiswahili wanapuuza sheria zote zilizoundwa ili kutawala muundo wa sentensi na mpangilio wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. kwa mfano:

Mfano (4.5)

- Kujaring- kwenda
- Kaming – kuja
- Buyie- kununua
- Sendie- tuma
- Aliadmitiwa- alilazwa

Watumiaji vilevile wanaamini kuwa matumizi ya mbinu za ufupishaji wa kimtandao huwasaidia kukuza, kuendeleza na kuimarisha ujuzi wao wa uandishi jambo ambalo si kweli. Hii ni kwa sababu imeathiri namna tunavyotumia maneno fulani ya Kiswahili. Wengine wanasahau na kufupisha hata katika muktadha rasmi. Hili limeathiri namna watu wanavyotumia tahajia, sarufi na hata wamekosa kutumia viakifishi kabisa.

Kufikia sasa, lugha mtandao imeathiri lugha karibu zote ulimwenguni, teknolojia inapoendelea kuimarika maneno mapya ya kimtandao yanaendelea kuzalishwa na kukua. Namna lugha inavyokua na kuimarika ndivyo lugha ya Kiswahili inavyoendelea kuathiriwa na mitandao ya kijamii. Mtandao wa Twita ulianzisha dhana ya 'tweet' au 're-tweet' kama tendo lakini kufikia

sasa watu wameingiza kwenye msamiati katika lugha na kufanya kuwa kitenzi. Wataalamu mbalimbali wanasema kuwa mitandao ya kijamii inaendelea kuua lugha zetu kwa ujumla na kuathiri namna tunavyotumia lugha kujieleza. Lugha mtandao imefanya watu kuunganisha maneno au vishazi na kuacha nafasi na pia kutumia herufi kubwa katikati ya maneno ambayo ni kinyume katika lugha ya Kiswahili

Lugha mtandao vilevile ni lugha huru na hutumika katika mawasiliano ambayo si rasmi, haizingatii kanuni za matamshi na mpangilio wa maneno. Hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili kwa sababu maneno ya kimtandao yanazalishwa na kuundwa tu ovyoovyo bila kuzingatia taratibu za kuzalisha msamiati, haifuati sheria za tahajia na kanuni za Kiswahili kwa ujumla. Watumiaji wengi vilevile hawajali kuangalia muundo sahihi wa sarufi, hawafuati mtindo rasmi wa uandishi na wanapuuza matumizi ya kaida za upole katika mawasiliano. Wakati mwingine wanatumia lugha isiyo sahihi, rasmi na hata kuhamisha na kutumia katika sajili rasmi.

Vifupisho vikiendelea kutumika kwa muda mrefu vitakuwa na athari hasi katika matumizi ya tahajia katika maneno hivyo kuathiri ukuaji wa lugha. Hii ni kwa sababu matumizi ya tahajia sahihi katika neno ni njia mojawapo ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Vifupisho vinaweza kumfanya mtumiaji au msomaji hasa yule ambaye hafahamu vyema vifupisho kufasiri vibaya ujumbe hivyo kutofanikisha mawasiliano. Kwa mfano, kuna maneno katika lugha ya Kiswahili ambayo watumiaji wakifupisha huwa na idadi sawa ya maneno na huwa yanafanana kwa hivyo mtumiaji anapopatana na neno kama hilo iwapo hafahamu vyema anaweza kufasiri ujumbe huo kwa njia isiyofaa. Maneno yafuatayo yanapofupishwa huzua utata kama vile:

Mfano (4.7)

- KTK – huweza kumaanisha ‘kutoka’ au ‘katika’
- BB- huweza kuwa ‘bibi’ au ‘baba’
- MCH-huweza kuwa ‘mchana’ au ‘msichana’
- KM- huweza kuwa ‘kama’ au ‘kwa mfano’

Vifupisho vikiendelea kutumika kwa muda mrefu kuna uwezekano wa neno kamili kupotea/kudidimia au kufa na neno ambalo limefupishwa likabaki na kuwa neno kamili. Maneno yote yanayotumiwa katika lugha hupatikana kwenye kamusi hata hivyo vifupisho vikiendelea kutumika maneno ya Kiswahili ambayo hupatikana kwenye kamusi yatatupiliwa mbali na mahali pake kuchukuliwa na vifupisho.

Matumizi ya kuchanganya lugha mbili husababisha athari kubwa katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha mbili zinapotumika kwa pamoja katika mawasiliano kuna uwezekano wa lugha moja kupewa hadhi ya juu na nyingine kupewa hadhi ya chini. Lugha hizo mbili zinapotumiwa kwa muda huathiriana kwa sababu lugha iliyopewa hadhi ya juu huathiri ile ambayo imepewa hadhi ya chini. Katika uhusiano huu, lugha yenye hadhi ya chini huazima maneno kutoka kwa lugha yenye hadhi ya juu. Kwa mfano, katika mawasiliano ya kimtandao lugha ya Kiingereza hupendelewa sana na watumiaji kuliko lugha ya Kiswahili kwa vile wao huamini kuwa ni maarufu na wanaotumia ni watu wa tabaka la juu. Kwa hivyo kuchanganya Kiswahili na Kiingereza kutaathiri Kiswahili kwa mfano:

- Kiswahili hakitaimarika na kuendelea na jambo hili litazuia uundaji na uzalishaji wa msamiati mpya kwa hivyo kutasababisha uhaba wa msamiati.

- Msamiati uliopo usipotumika kwa muda mrefu huweza kufifia na hata kufa na ule ambao umezoeleka na hutumika kila wakati utaibuka.

Watumiaji vilevile wanapochanganya msimbo wao hupuuza na kuepukana na matumizi ya sarufi sahihi hivyo huathiri wale ambao wanasoma na kujifunza lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mbinu zote za kimtandao hutumiwa sana na vijana ambao ni asimilia kubwa katika jamii. Hii itaathiri ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Mbinu hizi za kimtandao kama vile kuchanganya msimbo zitaathiri tajriba ya watumizi. Kutokana na sababu hii zikitumika kila siku watumiaji wachanga watazoea kuzitumia na hivyo kudhani kuwa mambo hayo ni kawaida na watajihusisha na lugha hii ya mtandao na kupuuza kaida na sheria zinazofuatwa katika lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya mtandao kwa muda mrefu yatawafanya watumiaji kuamini kuwa makosa ya lugha ambayo yanafanywa hasa wanapowasiliana ni sahihi hivyo kuathiri ukuaji wa lugha na hata kuififisha kabisa.

Athari nyingine ni tafsiri isiyo sahihi ya maneno kutoka lugha moja hadi nyingine, tahajia na sarufi isiyo sahihi na matumizi ya maneno vibaya huathiri lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, juhudi za kuunda ukurasa wa Kiswahili katika Facebook, zinaonyesha kwamba waanzilishi walitafsiri sisi maneno ya Kiingereza hadi Kiswahili ambapo maneno mengine ya Kiswahili hayaleti ujumbe uliokusudiwa hivyo kupoteza maana.

Matumizi ya herufi kubwa katikati mwa neno au mahali ambapo hapahitajiki huweza kuathiri ukuaji wa lugha. Hii ni kwa sababu matumizi haya huweza kuwachanganya watu hadi wakashindwa kufahamu jinsi ya kutumia herufi sahihi katika neno. Tunapotumia herufi kubwa

mwanzoni mwa neno ni jambo la kawaida na sahihi katika Kiswahili lakini inapobadilishwa na kuingizwa mwishoni mwa neno au katikati huathiri lugha ya Kiswahili.

4.2 Athari Chanya zinazosababishwa na matumizi ya Vifupisho

Mbali na athari hasi zinazotokana na vifupisho vya kimtandao tumebainisha kuwa lugha mtandao huweza kurutubisha lugha hii ya Kiswahili. Yafuatayo ni manufaa yake katika lugha ya Kiswahili:

Mbinu za ufupishaji huweza kuleta athari chanya katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mbinu hizi zikiendelea kutumika huweza kuimarisha lugha ya Kiswahili. Matumizi ya vifupisho vya kimtandao huweza kukubalika hivyo msamiati kuongezeka na hata huweza kuingizwa katika kamusi za Kiswahili.

Kwa mfano:

N.K- Na Kadhalika

K.M- Kwa Mfano

K.V Kama Vile

Matumizi ya mitandao ya kijamii yanatajwa kuinufaisha lugha ya Kiswahili kwa kupata kwake jukwaa pana zaidi la kujitangaza, kujitanua na kujieleza kwa ulimwengu. Hii ni kwa sababu Kiswahili kinapotumika mtandaoni huwa na nafasi kubwa zaidi ya kufikia wasomaji wa lugha ya Kiswahili. Kuna juhudi kadha wa kadha ambazo zimefanywa ili kuimarisha lugha ya Kiswahili mtandaoni. Hata kama mitandao inadhuru lugha ya Kiswahili kwa kiasi fulani imeweza

kuinufaisha. Matumizi ya vifupisho, akronimu, mchanganyiko wa nambari na herufi na tahajia za kifonetiki hupunguza makosa ya kitahajia katika upigaji chapa.

4.3 Hitimisho

Athari mbalimbali ambazo husababishwa na mitandao ya kijamii imebainishwa. Kuna athari hasi na chanya zinazotokana na kuongezeka kwa vifupisho katika lugha ya Kiswahili. Katika kubainisha athari hizi, tuliongozwa na vigezo vya kifonolojia na mofolojia. Athari hizi zimeathiri sekta zote za maisha na zinasababishwa na vijana ambao ni viongozi wa kesho. Athari hizi zimedidimiza na kuzuia kuendelea kwa lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Hii ni kwa sababu lugha mtandao imefanywa kuwa kama lahaja ya mtandao. Sura ya tano itatoa muhtasari wa utafiti, utoshelevu wa nadharia, changamoto, na mapendekezo kwa minajili ya utafiti wa baadaye.

SURA YA TANO

HITIMISHO LA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho, matokeo ya utafiti, utoshelevu wa nadharia pamoja na mapendekezo ya tafiti zaidi. Haya ni baada ya kupitia sura za kwanza nne. Sura ya kwanza ilionyesha usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia matumizi ya Kiswahili katika mitandao mitatu ya Kijamii: Facebook, Twita na Wikipedia. Katika sehemu hii historia fupi ya mitandao mitatu ilianguziwa. Kupitia kwa mtandao wa Facebook inadhihirika kuwa, kuna jitihada kadha ambazo zimefanywa ili kukuza lugha ya Kiswahili hasa kupitia kwa mradi wa kuunda ukurasa wa Facebook katika lugha ya Kiswahili kwa kutafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hadi ya Kiswahili. Pili imebainika kuwa, Kiswahili hakijaachwa nyuma sana katika matumizi yake katika mtandao huu ambapo mashirika ya utangazaji, biashara na ya usomi yakitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano ya kawaida. Tatu, imedhihirika kuwa kuna mijadala mbalimbali ambayo imeanzishwa ili kuimarisha lugha ya Kiswahili. Katika mtandao wa Twita lugha ya Kiswahili imekuzwa na kuendelezwa pia kupitia kwa mashirika ya utangazaji kama vile redio na televisheni. Watu wamechangia katika mijadala mbalimbali kupitia kurasa za Twita kwa mfano, kituo cha redio cha KBC, QFM, Redio Maisha na jukwaa la kimtandao la Swahilithub wameshirikisha lugha ya Kiswahili kupitia mijadala mbalimbali kuhusu lugha, isimu jamii, isimu na fasihi. Mtandao wa Wikipedia vilevile umeweza kuwa kitovu cha Kiswahili kwa sababu hutumiwa kuhifadhi mamilioni ya tafiti katika lugha ya Kiswahili. Mtandao huu hutuwezesha kupata makala mbalimbali ya Kiswahili kama vile ya sayansi na teknolojia, fizikia, saikolojia na fasihi ya

Kiswahili. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili imekuzwa na kuendelezwa kupitia kwa mitandao ya kijamii na kufikia wapenzi wengi wa Kiswahili kote ulimwenguni.

Sura ya tatu imebainisha lugha mtandao ambayo huitwa 'Netspeak, kwa msingi wa nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU). Sura hii vilevile imeangazia matini ya usemi ambayo yamefupishwa. Utafiti huu umeangazia sifa za ufupishaji kwa ujumla na kubaini kuwa, vifupisho vinatumika kwa wingi na vimesambaa kotekote. Sura ya nne imeangazia athari mbalimbali ambazo husababishwa na vifupisho vya kimtandao katika lugha ya Kiswahili.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mbinu zinazotumika kufupisha maneno katika mitandao mitatu ya kijamii hasa Facebook, Twita na wikipedia. Sababu za kufanya hivyo zilikuwa kutathmini mbinu zinazotumiwa kufupisha maneno katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili. Malengo makuu matatu ya utafiti huu yalikuwa: kwanza, kujadili matumizi ya Kiswahili katika mitandao mitatu ya Kijamii. Pili, kubainisha namna mbinu za ufupishaji zimetumika katika mitandao ya kijamii. Lengo la mwisho ni kuchunguza athari za vifupisho hivyo katika lugha ya Kiswahili.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Mtandao wa Facebook ulibainika kuwa maarufu zaidi katika matumizi yake ya kimawasiliano. Facebook ni mtandao ambao umetengenezwa kwa ubunifu wa hali ya juu, na unaotoa huduma nyingi zaidi kuliko mitandao mingine kama vile Twita, Linked In, My space na mingine mingi. Ilishuhudiwa kuwa, Facebook ni mtandao ulio na asimilia kubwa ya watu wanaoutumia na vijana

ndio wengi. Uchunguzi huu vilevile ulibaini kuwa vifupisho vya Kiswahili vinatumika sana katika mtandao huu. Asilimia 86 % ya mbinu ambazo zinatumiwa ili kurahisisha mawasiliano ni vifupisho. Aina mbalimbali za vifupisho zilijadiliwa na kutolewa mifano katika majedwali. Jambo jingine ambalo lilishuhudiwa ni kuwa, lugha ya Kiswahili haitumiwi sana katika mtandao wa Facebook na inapotumika watu hawazingatii kanuni au sheria za Kiswahili kama vile matumizi ya sarufi sahihi na tahajia.

Kupitia kwa mtandao wa Twita ilibainika kuwa mtandao huu ndio chanzo cha ufupishaji hasa inapojulikana kuwa lugha inayotumika pale ni ya mkato. Kuna msamiati ambao ni maarufu sana katika mtandao huu ambao huitwa 'Tweets'. Neno hili hutumiwa kwa maana la kufupisha. Asilimia 60% ya maneno ya Kiswahili yanayotumika katika mawasiliano ya kimtandao ni vifupisho.

Mtandao wa Wikipedia ndio mtandao maarufu sana kote ulimwenguni na ilibainika kuwa vifupisho ambavyo vinatumika pale ni vile ambavyo vimekubalika katika lugha ya Kiswahili na hata kuingizwa katika kamusi zetu. Hivyo kubainisha tofauti zilizopo baina ya mitandao miwili ya Facebook na Twita. Wikipedia ni mtandao wa watu maarufu na hutumiwa na wataalamu au wasomi kupitisha ujumbe ambao ni faafu. Mtandao wa Wikipedia ni tofauti na mitandao ya Facebook na Twita ambayo hutumiwa sana na vijana kwa shughuli zisizo rasmi. Kwa hivyo mtandao wa Wikipedia umeweza kunufaisha lugha ya Kiswahili kupitia mapitio mbalimbali ya makala yanayohifadhiwa pale. Jambo jingine tuliloweza kubainisha kupitia kwa mitandao hii ni kuwa, mitandao ya Facebook na Twita hutumiwa kwa ajili ya kutuma picha, habari na kuwasiliana na marafiki lakini mtandao wa Wikipedia hutumiwa kwa ajili ya kiakademia.

Utafiti huu umebainisha ya kwamba Kiswahili kimeendelezwa kwa kiasi kidogo katika mitandao ya kijamii. Utafiti pia umedhihirisha kuwa vifupisho vinatumika sana katika mitandao ya kijamii. Ilibainika kuwa, idadi kubwa ya vifupisho ni vile vinavyohusu udondoshaji wa herufi katikati mwa neno au sentensi. Ikifuatwa na kuchanganya msimbo na mwisho mchanganyiko wa nambari na maneno. Idadi kubwa ya watumiaji ni vijana ambao wanataka kuwasilisha ujumbe haraka iwezekanavyo. Kitandazi cha Facebook ndicho kinachoongoza katika matumizi ya vifupisho kikiwa na asilimia 60% ya vifupisho kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza kikifutwa na Twita na asimilia 30% na mwisho Wikipedia ambayo ni 10%. Katika mtandao wa Wikipedia ni dhahiri kuwa vifupisho ambavyo hutumika ni vile ambavyo vimekubaliwa na hata kuingizwa katika lugha ya Kiswahili.

Vifupisho vinavyotumika katika mitandao mitatu ya kijamii vilibainishwa kwa kusakura na kuwahoji watumiaji. Vifupisho vilinakiliwa kwenye daftari na kisha kudondoa msamiati msingi. Msamiati msingi ulifafanuliwa zaidi kwa misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU). Utafiti huu pia umeweza kubainisha kwamba vifupisho vimeathiri mpangilio wa konsoñanti- vokali na silabi hivyo tukabainisha athari za vifupisho vya kimtandao katika lugha ya Kiswahili.

Vigezo vya kijamii vilichunguzwa kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi. UTU hutambua kwamba, ufasili wa maana hutegemea vikwazo vya kijamii. Vigezo hivi ni pamoja na umri, jinsia, elimu, tabaka na umilisi wa lugha. Vigezo hivi viligunduliwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuathiri ufasili wa ujumbe. Kigezo cha umri kilibainika kuathiri sana matumizi ya vifupisho vya kimtandao. Ni dhahiri kuwa vijana ndio waliokuwa asilimia kubwa

kwa kutumia vifupisho kwa vile wanataka kupata majibu ya moja kwa moja. Wanafanya hivyo ili kujiweka katika tabaka fulani na kuficha siri au ujumbe.

Mhimili wa matini katika nadharia ya Uchanganzi Tahakiki Usemi ulituongoza kwa sababu matini yalitambulika na matini yenyewe yalikuwa vifupisho vya kimtandao na kigezo hiki kiliingiliana na lengo letu la pili la kubainisha mbinu zilizotumika kufupisha maneno ya Kiswahili katika mitandao mitatu ya kijamii.

Vigezo vya kifonolojia vya silabi na konsonanti- vokali vimetuongoza katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu kupitia kwa mpangilio wa konsonanti na vokali, vifupisho ambavyo vimekiuka kanuni hii vilikusanywa. Vifupisho vingi vya kimtandao havizingatii sheria hii kwa sababu baadhi ya watu wanapotupisha wanadondosha vokali zote au vokali iliyo katikati mwa konsonanti mbili. Wakati mwingine wanafupisha kwa kuchukua konsonanti pekee. Jambo lingine ambalo ilishuhudiwa ni kuwa, wanachukua sauti kutoka lugha moja au sauti ambayo hufanana na sauti nyingine kimatamshi. Katika uchunguzi wetu ilidhihirika kuwa baadhi ya maneno huazimwa kutoka lugha ya Kiingereza na kuswahilishwa kulingana na matamshi hasa ikiwa sauti moja hukaribiana au kuathiriana na nyingine. Kwa mfano, sauti **C** ya Kiingereza hutumiwa kama silabi **SI** ya Kiswahili na sauti **G** pia ya Kiingereza hufanywa kuwa **Ji** ya Kiswahili. Vilevile kimofolojia ilibainika kuwa, vifupisho vinakaidi taratibu za kuunda sentensi kwa sababu watumiaji wanafupisha kiholehola. Hii ni kwa sababu watumiaji wanaweza kuchukua herufi za mwanzo au za katikati na mwisho ili kuunda neno. Katika muundo wa kifonolojia mtafiti alichanganua mpangilio wa konsonanti- vokali na ule wa silabi. Utafiti huu

ulidhihirisha kwamba kunapotokea tofauti ya sauti moja maana ya neno huweza kubadilika na hivyo kuathiri uarifu wa habari.

Sifa hii ya ufupishaji ni matokeo ya lugha mtandao. Vilevile ilibainika kuwa watumiaji wameibuka na njia nyingine ya kudondosha herufi fulani mwanzoni au mwishoni mwa neno na nafasi yake kuchukuliwa na nambari. Nambari hutumiwa ili kurahisisha upigaji chapa wa ujumbe, kuokoa muda na kupunguza gharama. Hii ni kwa sababu kwenye mawasiliano ya kimtandao, watumiaji hawataki kupoteza muda wowote kwa sababu mawasiliano ni ya moja kwa moja. Ni bayana kuwa viakifishi sahihi ni nadra sana katika mitandao ya kijamii. Sifa hii hutumiwa ili kusisitiza jambo au kutilia mkazo. Kikomo na alama za mshangao hutumiwa sana ili kuonyesha hisi au mkazo wa neno. Haja ya watumaji ni kupitisha ujumbe na maana.

Athari chanya na hasi zinazosababishwa na mitandao ya kijamii katika lugha ya Kiswahili yalibainishwa. Kutokana na athari chanya, vifupisho vimekuwa na ushindani wa kipeke katika masuala mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Hivi leo katika ulimwengu wa teknolojia ya kimtandao, lugha ya Kiswahili inaonekana kuwa na mshiko mkubwa ikilinganishwa na lugha nyingine za kibantu. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazokubalika katika matumizi yake ulimwenguni. Hii imebainika waziwazi kutokana na idadi kubwa ya watumiaji wa lugha hii. Watu wengi hutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano, biashara, dini, shughuli za kijamii, shughuli za kidiplomasia na elimu. Hivyo basi, hali hii imekifanya Kiswahili kuingia katika mitandao ya kijamii kwa minajili ya kuunganisha jamii mbalimbali ulimwenguni. Hali kadhalika mitandao ya kijamii imesaidia kuongeza msamiati na istilahi katika lugha. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zilizonufaika na matokeo yake. Leo hii lugha ya Kiswahili

imefumbata istilahi kemkem zinazotokana na mitandao ya kijamii hasa katika kitandazi cha Facebook, hususan katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, siasa, utamaduni na uchumi. Kwa mfano; tunashuhudia maendeleo ya sayansi na teknolojia jinsi yalivyosababisha mfumuko wa istilahi nyingi za kimtandao katika lugha ya Kiswahili.

5.3 Mchango wa Utafiti

Mradi wa Kiswahili Facebook umepanua matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa watumizi ambao huenda hawafahamu Kiingereza, unakuza Kiswahili kwa kuweka maneno mapya ya kiteknolojia ambayo yanawapa watumizi nafasi ya kuyafahamu yanapoibuka katika mfumo wa kiteknolojia. Kwa mfano, network- mtandao, logout- ondoka na password- neno siri. Mradi huu umehakikisha kuwa Kiswahili kinaendelea kukua kwa njia iliyo huru bila kutegemea ukopaji wa maneno kutoka kwa lugha ya Kiingereza au zingine ili kujitosheleza na kukidhi mahitaji ya watumiaji wake. Kwa hivyo, mchango unaenda sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia. Hii ni kwa sababu ukuaji wa lugha ya Kiswahili unawiana na ukuaji wa kiteknolojia, hivyo kurutubisha na kuimarisha ushindani wake kama mojawapo ya lugha ambazo zinaendelea kuathiriwa na teknolojia na kutandawazika kila uchao. Mradi wa Kiswahili Facebook ulitafsiriwa moja kwa moja kutoka lugha ya Kiingereza. Kwa maoni yangu ni vema wataalamu wa lugha kuungana ili kuunda mradi ambao ni chasili na wala si tafsiri.

Kuingizwa kwa Kiswahili katika mitandao ya kijamii ni hatua kubwa sana inayoonyesha kuwa, Kiswahili kinaendana na hali ya kiteknolojia. Hii ni kwa sababu watu hupata habari ambazo zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kufanya watu wanaoienzi lugha hii kusoma makala mbalimbali katika mitandao ya kijamii.

5.4 Changamoto za Utafiti

Ingawa utafiti huu ulifaulu katika kutimiza malengo yake, kulikuwepo na changamoto kadha ambazo kwa kiasi zilitatiza utafiti wetu. Kwanza kabisa, utafiti huu ulikumbwa na tatizo la ukosefu wa tafiti za kutosha zilizofanywa kuhusiana na swala la matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Udurusu wetu wa maandishi uligundua kuwa, kuna tafiti chache tu zilizofanywa kuhusiana na swala hili. Kiasi kikubwa cha tafiti hizi kinahusu mapendekezo tu ya kukitumia Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Kutokana na sababu hii, utafiti huu ulipungukiwa katika kuzipata kazi za kurejelea ili kupata msingi dhabiti wa kuuegemeza utafiti wenyewe.

Tatizo lingine lilikuwa lile la ukusanyaji wa data katika mitandao ya kijamii, kwani maelezo mengi juu ya Kiswahili yametawanyika kotekote mtandaoni na hivyo ilikuwa vigumu kuyapata maelezo ya kina kwa haraka. Vitabu vya karne hii ambavyo vimo maktabani ni vichache mno kwa hivyo ilibidi kuvitafuta kwenye mtandao na havina mengi kuhusu teknolojia ya mitandao.

5.5 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi iliyotuongoza ilitosheleza katika uchanganuzi wa data. Hii ni kwa sababu kupitia kwa nadharia hii tuliweza kuchanganua data na kupata matokeo mwafaka. Katika nadharia ya UTU jambo muhimu ni matini andishi na mazungumzo, kwa hivyo ilitosheleza mahitaji ya utafiti huu. Utafiti wetu vilevile ulihitaji nadharia nyingine ya kuonyesha kuwa vifupisho husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Kwa upande huu, nadharia ya UTU ilipungukiwa kwa kiasi fulani kwa sababu haikutusaidia katika kuonyesha kuwa vifupisho husambazwa kutoka jamii moja hadi nyingine au kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

5.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulijikita katika mbinu za kufupisha maneno ya Kiswahili pekee na siyo lugha nyingine, pia ulijifunga kwenye suala la isimujamii. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha haja ya tafiti zaidi kufanywa ili kubainisha masuala mengine ya kiisimu ambayo huweza kuathiri lugha ya Kiswahili hasa katika enzi hizi ambazo teknolojia ya mitandao imeathiri sekta zote katika maisha ya binadamu. Masuala haya ni pamoja na fonolojia, mofolojia na sintakisia. Mitandao zaidi ya kijamii pia inaweza kuchunguzwa kwa mfano, linkedIn, Qeep, 2Go, My Space na Blogu. Mbinu mbalimbali za lugha mtandao (Netspeak) pia zaweza kufanyiwa utafiti kwa vile tuliweza kuchunguza mbinu moja pekee ambayo ni ufupishaji. Vigezo vya umri, tabaka na elimu vilitiliwa maanani. Tafiti zingine zinaweza fanywa hasa kwa kuchunguza mbinu mbalimbali ambazo zilitumika katika kutafsiri lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili katika mradi wa Swahili Facebook. Mawasiliano-jamii kama vile kamera za mtandao (Youtube), na pia blogu na vyumba vya 'chat' au kupiga gumzo pamoja na simu za mkono na 'vitanzu vyake' vya hivi sasa vinatumika sana, athari zao kwenye matumizi ya lugha ya Kiswahili na mazingira yake hazijachunguzwa kwa undani mpaka sasa.

Pana haja ya utafiti wa kina kufanywa ili kuibuka na kamusi ya vifupisho ambayo itatumika katika kuwaongoza wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kutumikiza vifupisho katika mitandao ya kijamii. Utafiti huu utasaidia katika kutoa mwongozo wa kuwawezesha watu kutumikiza vifupisho ambavyo 'vimesanifishwa'. Yaani, wanaweza kutumia vifupisho sawa katika mawasiliano licha ya kuwa maeneo mbalimbali ya kijiografia.

Uundaji wa msamiati katika mradi wa Kiswahili Facebook umeweza kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Jambo hili litasaidia kutoa istilahi nzuri na zinazoeleweka kwa urahisi kwa

watumiaji. Baada ya kuundwa istilahi hizi inatakiwa zisambazwe kwa watumiaji kwa kiwango kinachoridhisha ili waweze kujifunza na kuzifahamu na hatimaye kuzizoea katika matumizi yao ya kila siku katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Nasema hivi kwa sababu usambazaji wa istilahi hizi umekuwa haufanywi kwa kiwango kinachohitajika, na katika usambazaji, vyombo vya habari vipewe kipaumbele, kwani istilahi hizi zikitumiwa na vyombo vya habari itakuwa rahisi sana kwa watumiaji wengine kuzitumia. Wazungumzaji wa Kiswahili pia wawe tayari kutumia istilahi hizi au programu za Kiswahili katika matumizi yao ya kompyuta. Mradi wa Kiswahili Facebook umeandikwa kwa Kiswahili lakini wazungumzaji wengi wa Kiswahili bado wanatumia miradi iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Ukurasa wa Facebook unapatikana kwa Kiswahili lakini nina wasiwasi kuwa miongoni mwetu hakuna mtu hata mmoja anayetumia Kiswahili Facebook. Kwa hivyo tunapendekeza suala hili litiliwe maanani, kwa kuwa sisi tumejitolea kueneza na kuienzi lugha ya Kiswahili. Pia ni jukumu letu kuchangamkia fursa kama hizi, tuwe wa kwanza kutumia miradi kama hii kwa Kiswahili pindi inapotokea. Katika kufanya hivi, tutakuwa tunakienzi Kiswahili na kukikuzi kwani watu wanaotuzunguka watakapotuona tukitumia Kiswahili Facebook watahawishika kuitumia. Hivyo, kwa njia hii tutakuwa tumefanikiwa kukuza na kuienzi lugha ya Kiswahili. Matumizi ya mitandao ya kijamii imebadili maisha ya watu wengi sana, haswa namna ya upashanaji habari. Taarifa zimekuwa zikiwafikia watu wengi sana kwa muda mfupi.

Watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii ni vijana na wengi wao hutumia mitandao hii kwa ajili ya kupiga gumzo, kutuma picha ambazo hazina mantiki na zisizo maadili. Jambo hili linawapotezea muda mwingi, kuharibu fikra zao na kupunguza uwezo wao wa kujikita katika masuala ya msingi kama vile ya kiakademia na ya kijamii. Matokeo ni kuwa na vijana wengi

wasiojali maendeleo yao ya kibinafsi na ya kijamii. Kuna fursa nyingi sana kwenye mitandao ya kijamii, iwapo tu mtumiaji ataamua kutumia mitandao hii kama sehemu ya kujiendeleza. Hii ni kwa sababu watumiaji hawa wanaweza kutumia mitandao kutafuta taarifa zenye mwelekeo na maarifa ili kuleta maendeleo katika nchi badala ya kutafuta taarifa ambazo hazina faida na za kupotosha kimaadili. Mitandao ya kijamii imejaa maarifa ya kiakademia kutoka kwa taaluma tofauti tofauti ambazo hufanya dunia kuwa kijiji kimoja.

Wito kwa vijana ni kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujitengenezea fursa za maendeleo. Wasipoteze muda kwenye masuala ambayo si ya msingi pindi wanapokuwa mtandaoni bali watumie muda wao kujifunza na kudadisi masuala ya msingi yanayoweza kuwaletea maendeleo. Licha ya majukwaa ya Facebook, Twita na Wikipedia kudumisha matumizi ya Kiswahili, hayajatiliwa maanani na kupewa umuhimu wowote hasa kuhusu mchango wao katika uendelezaji na ukuzaji wa lugha hii. Ni majukwaa ambayo yatahakikisha ukuaji wa Kiswahili iwapo tu yatatiliwa maanani na kutumiwa kwa ajili ya maendeleo kwa lugha hii hasa katika enzi hizi za TEKNOHAMA. Hii ni kwa sababu matumizi ya mitandao ya kijamii na teknolojia kwa jumla yameibuka na kuwa na msukumo mkubwa katika ushinikizaji wa masuala yanazozikumba jamii zetu. Ni dhahiri kuwa, kwa sasa kuna mpangilio wa kitandazi ambacho kina lugha ya Kiswahili pekee, kando na kitandazi cha lugha ya Kiingereza.

Nafasi ya Kiswahili inapozungumziwa katika mabadiliko ya kisasa, hatuna budi kusema kuwa Kiswahili pia kinabadilika na nafasi yake katika mchango wa maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi bado utaendelea kuwepo tu. Jinsi mitandao ya kijamii ya Facebook,

Twita na Wikipedia inavyotumika katika shughuli kama biashara na elimu, ndivyo lugha ya Kiswahili inavyopata nafasi kubwa ya kujiendeleza. Kwa hivyo, bado kuna nafasi kubwa sana ya Kiswahili katika ulimwengu ambao unazidi kuyashuhudia mabadiliko muhimu yanayoletwa na mitandao ya kijamii. Shida iliyopo ni kwamba, kurasa nyingi zilizoko kwenye mitandao ya kijamii hasa Wikipedia zinahitaji kuhaririwa kwani zimejaa makosa hasa ya kisarufi.

Marejeleo

- Appel, R. na Muysken P. (1987). *Language Contact and Bilingualism*. London: Edward Arnold.
- BAKITA, (2004) “ Makala ya siku ya Kiswahili na Utandawazi”, Dar es salaamu.
- Baron, N. S (2001). Language of the Internet. *In The Stanford Handbook Language for Engineers*, Ali Farghali (ed). Stanford California. CSLI Publications 1-63. Available at [http:// www. American. Edu/cas/ Faculty/nbaron.Cfm](http://www.American.Edu/cas/Faculty/nbaron.Cfm).
- _____ (2010). *Discourse Structures in Instant Messaging: The Case of Utterance Breaks*. Available at: (www.languageatinternet.de, urn:nbn:de:0009-7-26514, ISSN 1860-2029).
- Bauer, Lauri (1983). *English Word-formation*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Batul, F. (2009). *Chatspeak; Linguistic Evolution or Devolution*. New York: Pergamon Press.
- Berk-Seligson, S. (1986). Linguistic Constraints on Intersentential Codeswitching: A Study of Spanish/ Hebrew Bilingualism. *In Language and Society* (pp.331-338).
- Bieswanger, M. (2007). 2 abbrevi8 or not 2 abbrevi8: A contrastive analysis of different space-time-saving strategies in English and German text messages. *Texas Linguistics Forum*. 50, 1-12. Also available online at: <http://studentorgs.utexas.edu/salsa/proceedings/2006/Bieswanger.pdf>.
- Bodomo, A. (2009). *Computer mediated Communication for Linguistics and Literacy: Tcchnology and Natural Language Education*. Her-shey: Information Science Publishing.
- Bokamba, E. (1989). Are there Syntactic Constraints on Code-mixing? *World Englishes* 8(3): 277-292.
- Boyd, D. & Ellison, N. (2008). “Social network sites”: Definition and conception. *Journal Of Computer Mediated Communication*, 13 (1), 210-230.
- Brown, G. and G. Yule (1983). *Discourse Analysis*: Cambridge. University Press.
- Chandler. D (1997). *Simotics for beginners*. Available at:

[http:// users.aber.ac.uk/dgc/Document/S4B](http://users.aber.ac.uk/dgc/Document/S4B).

Crystal, D. (2001). *Language and the Internet*. Cambridge: Cambridge University Press.

_____ (2004). *Language and the Internet*. Cambridge: Cambridge University Press. (2003). Site search and Instant Messaging Reference: A Comparative Study. *IRSQ: Internet Reference Services Quarterly* 8(1/2), 167-182.

_____ (2006). *Language and the Internet*. 2nd ed. New York: Cambridge University.

_____ (2008a). Text Messages. *ELT Journal* 62(1): 77-83.

_____ (2008b). *Txting: the gr8 db8*. Oxford: Oxford University Press.

Fagan, J.C. and Desai, C.M. (2003). SiteSearch and Instant Messaging. Reference: A Comparative Study. *IRSQ:Internet Reference Services Quarterly* 8 (1/2), 167-182.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. New York. Longman. Arnold.

_____ (1992). *Discourse and Social Change*. London. Polity. Grammer (3rd edition. London:

Fairclough, N. na Chouliaraki, L. (1999). *Discourse in Late Modernity: Rethinking Critical Discourse Analysis*. Edinburgh University Press.

Gikambi, H. (2014). 'Mgeni Njoo Mwenyeji Atambe'-Athari Za Facebook, Twitter Na Youtube Katika Vyombo Vya Habari Vitumiavyo Kiswahili. Makala kwenye Kongamano la Swako.

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html.

Habwe, J.H (1999). *Discourse Analysis in Swahili Political Speeches*". Phd Thesis.

Hanson, J. (2007). *24/7: How Cellphone and the Internet Change we Live, Work and Play* Westport, CT: Praeger Publishers.

Hudson, Grover (2000). *Essential Introductory Linguistics*. Oxford: Blackwell.

Hymes, Dell H. (1974). *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*.

Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Ingo. P. (2003). *Word- Formation in English*. Cambridge: Cambridge University Press.

Jagero, J. A. Mohochi, E. S. na Indede, F. (2013). "The Usage of Kiswahili in Blog

Discourse and the Effects on Its Development". *International Journal of Humanities and Social Science*. VOL. 3 NO. 14 (Special Issues- July 2013) 192-199.

Javanovic. D (2013). A qualitative Study of the use of Netspeak in English Language in classroom.

Implementation of Netspeak in High school and University. Masters thesis.

Kamau, S.N. (2005) *Matumizi ya Kiswahili katika Tarakilishi*, Masters Thesis (Unpublished): Kenyatta University.

Kaplan A. M., & Haenlein, M. (2010). "Users of the world, unite! The challenges and opportunities of Social Media". *Business Horizons*, 53, 59-68.

Khayesi, M.K. (2002) "Kiswahili and Information Technology (I.T): Challenges in

Public University Libraries in Kenya' katika *Kiswahili Juzuu 65 Dar- es – Salaam*, T.U.K.I. uk. 24 – 31.

Kimani. N, A. Mwhaki na A. Buliba (2006). *Sarufi ya Kiswahili Uchanganuzi na Matumizi:*

JKF Press.

King'ei, K.(2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Kinsella, N (2010): Btw its just netspeak lol

KIE.(2002). *Ministry of Education Secondary Education Syllabus Vol.1*. Nairobi: KIE.

Kothari, C. R. 2004. *Research Methodology. Methods & Techniques*. New Delhi: New International (P) Limited, Publishers.

MacMahon, A. M. S. 1994. *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Maina, Rachel (2013). Makundi ya Lugha na Fasihi katika Facebook. Makala kwenye Kongamano la Chakita .

- Mann, C. na Stewart. F (2000). *Internet Communication and Qualitative research: A Handbook for researching online*. London: Sage.
- Massamba, D.P.B na wenzake (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA)*. Sekodari na Vyuo. TUKI, Dar es Salaam.
- Mcfedries, P. (2004). *Word spy: the word lover's guide to modern culyure*. New York: Books.
- McGregror, L. T. na Mitstifer D. I. (eds) 2003 *Critical Science and Critical Discourse Analysis*. Nu FORUM (Vol. 15, No.1). East Lansing: Kappa Omicron.
- Mohochi, E. S. (2002) "Teknolojia ya Mawasiliano na Nafasi ya Kiswahili Ulimwenguni" (Communication Technology and the state of Kiswahili in the World), University Press., Eldoret, pp. 219-224.
- Moraa Jackline (2012) Matumizi ya Kiswahili katika Mradi waMicrosoft East Africa 2004-2009. Masters Thesis (Unpublished): Kenyatta University.
- Muysken, P. 2001. *Bilingual speech. A typology of code-switching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mugenda, O.M and A.G. Mugenda (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: African Center for Technology Press.
- Mugenda, A. G. 2013. *Qualitative Research Methods Introduction*. Nairobi: ARTS Press.
- Mutembei, A. (2011). Kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: tafakari kuhusu Isimujamii. *SWAHILI FORUM 18 : 198-210*.
- Nekesa, S. B. (2010). Language, Mobile Phones and Internet: A Study of SMS Texting, Email, IM and SNS Chats in Computer Mediated Communication (CMC) in Kenya. LOT Publishers: Neiterlands.
- Nielson (2009, March). "Global Faces and networked places": A Nielson report on social Networking's new footprint. Retrieved 27/05/2014.

http://blog.nielsen.com/nielsenwire/wpcontent/uploads/2009/nielsen_gloalfacesmar09.pdf

- Pfaff, C.W. (1979). Constraints in Language Mixing in *Language* 55 pg 291-318.
- Richard. J. et al (1985). *A longman Dictionary of Applied Linguistics*. London; Longman.
- Romaine, S (1989). *Bilingualism*. Oxford: Basil Blackwell.
- Rúa, L. (2005). Shortening devices in text messaging: a multilingual approach. *Neuphilologische Mitteilungen*. 16, 139-155.
- Urban Dictionary. Available at <http://www.Urbandictionary.Com>.
- Varnhagen .C. K., G.Peggy McFall, Nicole Pugh. Lisa Routledge. Heather Sumida-MacDonald. Trudy E. Kwong (2009). "lol: new language and spelling in instant messaging". Published online: 2 Springer Science+Business Media B.V. 2009.
- Van Dijk, T. A. 1985. Semantic Discourse Analysis. In T. Van Dijk (Ed), *A Handbook of Discourse Analysis* (vol. 2). London: Academic Press.
- Van Dijk, T. A. 1993. 'Principles of Critical Discourse Analysis' in: *Discourse and Society*. Sage: London.
- Van Diik, 2001. *Multi- Disciplinary Discourse Theory (Critical Discourse Analysis)*; in R. Wodak and M Meyer (eds) *Methods of Critical Discourse Analysis*. Sage Publications: London.
- Van Dijk, T. A. 2008. *Discourse and Power*. Houndsmills: Palgrave.London.
- Wamitila, K.W.2003. *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*.Nairobi: Focus Books.
- Werry, C. (1996). Linguistic and interactional features of Internet relay chat. In S. C. Herring (Ed.), *Computer-mediated communication: Linguistic, social, and cross cultural perspectives* (pp. 47-63). Amsterdam: John Benjamins.
- William, F. P., "Social networking sites ": How to Stay Safe Sites: Multi-State. InformationSharing& Analysis Center (MS-ISAC). Retrieved 27 May 2014 <http://www.msisac.org>, 2009.

Wodak, R. na Meyer (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis*: Publishers. London.

Wodak, R.(2002). “*Aspects of Critical Discourse Analysis.*” ZfAL 36: 5-31.

[Alexa.com](#)

[Facebook/ Kiswahili Facebook.com](#)

[Kiswahili goes.com/ swahilihub.com](#)

[Tweetnet.com \(2011\)](#)

[www.Twitter.com](#)

KIAMBATISHO

Yafuatayo ni baadhi ya maneno ambayo yamefupishwa kutoka kwa kitandazi cha Facebook na mtandao wa Twita.

1. Hey hamkunimiss **io** muda yote?????

Hey hamkunimiss hiyo muda yote?

2. Hakuna **uengizi mko** wapy

Hakuna usingizi muko wapi?

3. Ni baridi **zna nni** ako **krb** na nandi/hillz

Ni baridi sana nani ako karibu na

4. **Nn** sasa acha kunisumbua

Nini sasa wacha kunisumbua

5. Imagine **cna** sahi

Imagine sina saa hii

6. **Cujipange 2twende** sasa

Si ujipange twende sasa

7. Huyo dame amebeba **qno** bwana.

Huyo msichana amebeba kiuno bwana

8. Tunasoma **Q** sasa hivi

Tunasoma kiu sasa hivi

9. **Ninaq** maze

Nina kiu

10. **Xaxa**

Sasa

11. Hiyo stori **ilikua vp?**

Hiyo stori ilikuwa vipi?

12. Lets go **pa1** at **3**

Twende pamoja saa tatu

13. **Cutaninulie ka1**

Siutaninulie kamoja

14. Yaani **wana1a** tena?

Yaani wanawania tena?

15. Niaje **1adia?**

Niaje Wanadia?

16. **2kutane** saa ngapi?

Tukutane saa ngapi?

17. Mjinga kama **22** kabisa

Mjinga kama tumbili kabisa

18. Siamini kuwa anatoshana na **2kimo**

Siamini kuwa anatoshana na mbilikimo

19. Wee ni **m2** wa aina gani sasa

Wewe ni mtu wa aina gani sasa

20. **Ki2** gani?

Kitu gani

21. **2ko2** poa

Tuko tu poa

22. Kwani unataka **nikuki2e**

Kwani unataka ni kukimbilie

23. Yule **msee amea3wa** sana na ulevi.

Yule mzee ameathiriwa sana na ulevi.

24. **C 2taenda** na **ma3** ama?

Si tutaenda na matatu ama?

25. Sijakwambia ninilala **444** jana, I was so tired.

Sijakwambia nililala fofofo jana, nilikuwa nimechoka sana.

26. I like muziki wa **ku4ka4ka** na wewe je? (muziki wa bongo flava)

Napenda muziki wa kufokafoka na wewe je?

27. **C 2kutane juma5**

Si tukutane jumatano

28. **Mfua5** wa magari nayo.

Mfuatano wa magari nayo

29. **6ki** ujinga wako.

Sitaki ujinga wako

30. Wacha **ku66** na useme kama unasema

Wacha kusitasita na uongee kama unaongea

31. Ati? Kwa **7bu** ya???

Ati? Kwa sababu ya nini?

32. Kikundi cha **77?** Gani hiyo tena?

Kikundi cha sabasaba ni gani hiyo tena

33. Twende **2m7hi** mama

Twende tumsabahi mama

34. Bye. **2o8** baadaye

Kwaheri tuonane baadaye.

35. **M4v1** ya kuku **w3w3**

Mavi ya kuku wewe

36. Wachana na huyo yeye ni **m4l4y4** wa kupindukia

Wachana na huyo yeye ni Malaya wakupindukia

37. **c** yule dame ako na **m4t4ko?**

Si yule binti ako na matako.

38. Haki **c** aliny**4m6a** kwa **mat.**

Haki si alinyamba kwa matatu

39. Yea.. **sku** mob.. **nko** Nai.

Siku mob niko Nairobi

40. **xmart xana**

Smart sana

41. Haha **c** unajua **2** @yvonne, ndalo utachapwa na **iy**o rungu yako,nimekaa kwa hi kichaka hadi nimekua **ivo,uyu** ndo mimi @Joan! Hahaha this is me @ Maurine!

42. Utafanyia **nn** **iy**o doo ukiwa single

Utafanyia nini hiyo doo ukiwa single

43. i hp umeiget

44. **Cwezi** vumilia zaidi nimeenda

Siwezi

45. **Mm c** semi ki**2**

46.Mimi si semi kitu

47. Inbox nkupe a hint ukipenda **ntakupea** more en more

48. **Tlkunywa** videadly!

Tulikunywa sana

49. **Nlimcheke** jana

Nilimcheke jana

50. **Wnacheza** na watu

Wanacheza na watu

51. **Amsema** vipi?

Amesema vipi?

52. **Ntachukua 2** haina **waz**

Nitachukua tu haina wasiwasi

53. **Alnchukiza 2** sana

Alinichukiza tu sana

54. Twende **2zbuy**

Twende tununue

55. It is almost **usku** (usiku)

56. By the way **2naeza** ishia kesho

Tunaweza

57. Mambo. **Nimsota** vibaya

Mambo. Nimesota vibaya

58. **WACHA????** kuonyesha mshangao

Wacha???

59. Haki **NISAIDIE 2**

Haki nisaidie tu

60. **Unaduu nn** kesho aftee?

Unaduu nini

61. Kumbe uko **hpa** kwetu..Ntaku'vst thn

Kumbe uko hapa kwetu.. nitakuvisit then

62. **Lkn** kwa tweeter **nilikuona** uko

Lakini kwa tweeter nilikuona uko

63. **2ma** cnta

Tuma

64. Pole roba **xna** cpy man

Sana

65. **Cwezi** round hii imezidi

Siwezi

66. **Vp** daktari?

Vipi daktari

67. **Uko sawa kbs**

Uko sawa kabisa

68. Mrng pals....**c 2patane** kwa job,,

Si tupatane

69. **Aki** urembo nayo....

Haki

70. unlike ile time **2likam** kwenyu...

Tulikuja

71. **Gpange** umpatikana

Jipange umepatikana

72. Hudson wee **ulikua** hapa juzi **csakumiss**

Hudson wewe ulikuwa hapa juzi sijkumis

73. **2mbo** itakumalisa wacha hiyo tabia ya ulavi?

Tumbo itakumaliza wacha hiyo tabia ya ulavi

74. hahahaaaa...!! Samson **nljua 2 ww n** mlavi.

Nilijua tu wewe ni mlavi.

75. Huhuhu mwanaume nikupitia mingi ...**ucjale** ata usiokoke **2ko pa1**

Usijali hata usiokoke tuko pamoja

76. **Hyo ni qali m2 wngu!**

Hiyo ni kali mtu wangu!

77. Ulivuka border **lkn?**

Lakini?

78. Unazd **kpndeza 2 xana**

Unazidi kupendeza tu sana

79. **Kwn** leo wanaume wameenda wapi kwa hii group ama vile ni father's day mmegoma?

Kwani

80. Hart **ndo nn?**

Ndiyo nini?

81. **Mm n** chiz!

Mimi ni mwendazimu

82. **nko.... juu cko** kimandazi mandazi... nimejibeba

Niko juu siko

83. **Pndeza rfki**

Pendeza rafiki

84. **C** naona iko **bna**

Si naona iko bwana

85. **Iyo ilikua** demonstration **2 n bdo**

Hiyo ilikuwa demonstration tu na bado

86. Unkaa we **c mxharp**

Unakaa wee si msharp

87. Nko ajez **lkn**???Stupidness ix allowed 4 thos who r olwaiz xtupd.Na **2xhawazoea**...!

Niko aje lakini???

88. Iko **wpi** hii

Iko wapi hii.

89. **Nn** ameamka **sai ka mm**? **xema** gudmorning

Nani ameamka saa hii kama mimi? Sema gudmorning

90. Hy pals drop manangoz **znu n** wa add whatsapp

Zenu ni

91. **Hk kwe2 jmn** yani vindege vinalia hadi raha **asbuh** ya leo. Kweli ijumaa imeanza vyema kwetu sote?

Haki kwetu jamani asubuhi

92. Pliz **cna uengic bana nidu**? Nani anaipea campo

Pliz sina ucingizi bwana nifanye?

93. Yah leo walstrike cjuu ju mode antaka kutransrwa...bt I thnk wamesort

Yah leo walstrike sijui juu mode anataka kutransfriwa

94. Na c umeloxt xna qwani uko apy

Na si umelost sana kwani uko wapi?

95. Ghai, nmepatkana

Ghai, nimepatikana

96. Unawaza nani mm ama?

Unawaza nani mama ama?

97. Nko shgli tu uko while going wit chuo

Niko shughuli tu

98. aja 2,

Wacha tu

99. Nlikua na2mia mse flani

Nilikuwa natumia mtu fulani

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY